BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	**Mhe.**	**Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe.**	**Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe.**	**Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe.**	**Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe.**	**Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe.**	**Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe.**	**Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe.**	**Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na**

			Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii,**
			na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**

19.	**Mhe.**	**Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe.**	**Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe.**	**Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe.**	**Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe.**	**Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe.**	**Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe.**	**Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe.**	**Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe.**	**Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe.**	**Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari,**

			Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake
29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Uwezeshaji,**	**-**	**Naibu Waziri wa Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe. Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe. Abdalla Maulid Diwani**	**-**	**Jimbo la Jang'ombe**
36.	**Mhe. Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
37.	**Mhe. Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
38.	**Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
39.	**Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
40.	**Mhe. Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
41.	**Mhe. Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
42.	**Mhe. Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
43.	**Mhe. Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
44.	**Mhe. Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
45.	**Mhe. Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
46.	**Mhe. Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

47.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
48.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
49.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
50.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
51.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
52.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
53.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
54.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
55.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
56.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
57.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
58.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
59.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
61.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
62.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
63.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
64.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
66.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
67.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
68.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
69.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
70.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
71.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
72.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
73.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
74.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
75.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
77.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
78.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
80.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**

81.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
82.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
83.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
85.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
86.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
87.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

Ndg. Raya Issa Msellem **-** **Katibu**

Kikao cha Tatu – Tarehe 11 Mei, 2018

Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba kuweka hati mezani ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Panya Ali Abdalla: (Kny. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa naomba kuweka hati mezani, Hotuba ya Kamati ya Kusimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2018- 2019. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 125

Maafa Yanayotokea Msimu wa Mvua Za Masika

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:**

Pamoja na jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwasaidia wananchi wake pale yanapotokea maafa kama mvua kubwa na kuporomoka kwa milima, lakini maafa haya ya mvua yamekua kila ikifika mvua za masika yakijirudia kwa sababu ama za kujenga katika njia za maji au miundombinu ya maji kushindwa kutoa maji kwa kasi.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa wale waliojenga katika njia za maji.

(b) Je, yapo maeneo yaliotengwa au kujengwa kwa ajili ya waathirika wa maafa ya mvua.

(c) Je, Serikali imeshaweka vifaa na fedha za dharura kwa ajili ya kuyahami maafa hayo yasilete usumbufu na kusababisha maafa mengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 125 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali imeshawatahadharisha wananchi wote waliojenga maeneo hatarishi yakiwemo mabondeni na njia asili za maji pamoja na kuwataka wahame katika maeneo hayo kutokana na athari zinazowakumba takribani kila mwaka katika msimu wa mvua.

(b) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Umoja wa Falme za Kiarabu kupitia Shirika la Mwezi Mwekundu *Emirate Red Cressent* imeshafunga Mkataba juu ya ujenzi wa nyumba za makaazi kwa waathirika wa Mvua za Masika. Nyumba hizo zinatarajiwa kujengwa katika maeneo ya Tumbe kisiwani Pemba na Nungwi katika kisiwa cha Unguja. Ambapo lengo ni kuwahamisha baadhi ya watu wanaoishi maeneo hayo.

(c) Mhe. Spika, Serikali imeshaweka vifaa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wanaoathirika na maafa mbalimbali, vifaa hivyo ni kama vile, mahema, magodoro, mabati, vyandarua, vitanda vya kipindupindu. Vifaa hivyo, vimehifadhiwa katika ghala la Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Saateni na Maruhubi kwa Unguja na Gombani kwa upande wa Pemba. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Spika, nami nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake ambayo yana matumaini lakini nimuulize Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kwamba:-

(a) Je mtu binafsi anaweza kuhama mwenyewe katika maeneo ambayo hatarishi wakati ambapo yeye ikipita mvua anarejea tena maeneo yale yale lakini mtu huyu akifikwa na tatizo je italaumika serikali au atalaumika yeye mwenyewe.

(b) Je mtu aliyehamishwa au atakaehamishwa Kwerekwe mjini au maeneo yeyote yanayoingia maji hapa mjini kweli utampeleka Nungwi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, suala la mtu binafsi kuhama katika mazingira kwanza tangu katika kipindi hiki Serikali ilipotoa tamko la watu kuhama na kuondoka katika maeneo hatarishi watu wengi katika maeneo mengi wameweza kutii amri ya Serikali na ndio maana ukaona mpaka hivi sasa bado Serikali hatujafungua *Camp* au *Station* ya aina yoyote kwa ajili ya kuwachukuwa waathirika wa watu ambao wameathirika na mvua. Sasa katika mwaka huu watu wameweza kuitikia wito wa Serikali na amri ya Serikali na tulitowa agizo lile katika Mikoa yote na Manispaa na Halmashauri zote watu wote walikuwepo katika maeneo hatarishi walipaswa kuondoka.

(b) Lile suala alilosema mtu ambae tunaweza tukamhamisha mjini tukampeleka Nungwi Mhe. Spika, Serikali ikiamua katika jambo lolote inakuwa imeshaamuwa na hii haitokuwa mara ya kwanza katika miaka ya nyuma watu walihamishwa katika maeneo ya Amani kwa wazee pale na wakapewa viwanja katika eneo la Mpendae kwa hio si jambo la kwanza na haitokuwa mara ya kwanza lakini serikali inafanya hivyo kwa kutizama maisha yao na maeneo ambayo wanakaa kwamba hayastahiki na maeneo ambayo ni hatari, kwa hiyo kinachofanya serikali ni kuwapeleka sehemu ambazo zitakuwa salama kwa maslahi yao na afya zao. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nami napenda kumuuliza swala moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b)) Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iliunda ume ya Wataalamu au Kamati ya kuratibu kushughulikia na kutoa ushauri kwa serikali kwa maafa hayo yanayotokezea mara mara.

(a) Je nini hatma ya Tume ile ilioweza kuona katika kuyachunguza matatizo yale

(b) Naomba nijue ni changamoto gani ambazo Tume ile imepambana nazo na imeziona na ikazigundua pamoja na kuwashauri wananchi kuyakwepa majanga haya ya mara kwa mara mvua zinaponyesha.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu**:**
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hamad Abdalla Rashid swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Serikali iliunda Kamati ya Wataalamu iliyojumuisha Wataalamu kutoka taasisi na maeneo mbali mbali dhamira ya serikali ilitaka kujua nini hasa ambacho kinasababisha kwa maeneo yetu mengi kuwa na athari hizi hasa inafika wakati wa mvua za masika na hata katika kipindi mvua za vuli. Taarifa ile wataalamu wale wameweza kuandaa taarifa yao taarifa imewasilishwa serikalini, Serikali imeshapokea taarifa yao na ushauri wao maelekezo ya serikali tutengeneze mazingira kwanza haitokuwa busara tukaenda tukawaondoa wale watu wote moja kwa moja ndio maana tayari serikali kupitia Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais tumeshasaini mkataba na wenzetu wa *Emirate Redicrising* ili tutakapoweza sasa kukaa nyumba zile kukawa kuna maeneo yale ambayo hatarishi moja moja ambayo yamekuwa yakiathiri tutaweza kuwahamisha watu wale kuwapeleka katika makaazi haya lakini ripoti ya Kitaalamu ipo imeshatoka na mda wowote serikali sasa itakapoamua kwenda kuifanyia kazi itafanyiwa kazi na watu wale na maeneo mengi ambayo wataaalamu wamepita walishawapa *warning* watu ambao wanaendelea kutaka kuendelea na majenzi ili wasiendelee tena na ujenzi kwa sababu tayari isharipotiwa.

Mhe. Spika, lakini pia changamoto ambazo tunakubaliana nazo tunakiri kwamba katika zoezi hili hasa la kuratibu maafa tunakabiliwa na changamoto nyingi wakati mwengine uwelewa kwa wananchi unakuwa kidogo siwezi kusema mdogo lakini kidogo kutakuwa kuna uwelewa lakini uwelewa wenyewe unatokana na hali zetu ambazo tumekumbana nazo kwa maana hiyo kuna changamoto ambazo bado serikali inaendelea kupambana nazo kadri ambavyo tunakuwa tunakutana nazo. Lakini pia tuendelee kuwaomba Wananchi na Waheshimiwa Wawakilishi kwa pamoja na hili tuliseme hapa Mheshimiwa Spika, kwa sababu sheria yetu ya kukabiliana na maafa inawajumuisha Waheshimiwa Wawakilishi ambao nao ni Wajumbe wa Kamati ya Maafa katika Wilaya zao na Halmashauri zao. Hivyo ni vyema wakajenga utaratibu, haitokuwa busara kuwa wanasema wakati wanafursa ya kurudi kushauri katika Halmashauri na Wilaya zao kwa hiyo turudi katika Wilaya zetu ambao sisi sote ni wajumbe tukaulize, tukashauri tuweze kupanga mipango itakayostahiki kabla ya kipindi cha mvua za masika na kabla kipindi hali yoyote ya hatari itakapotokea. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu**:**

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea jibu la nyongeza kwa Mhe. Hamad Abdalla Rashid kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba Kamati ile ya Wataalamu ilishatoa ripoti yake na serikali imeipokea na imetoa maelekezo na hivi sasa mambo mbali mbali yanafanyiwa kazi, yako mambo ya muda mfupi ya muda wa kati na muda mrefu na Waheshimiwa ni mashahidi katika hatua ambazo zimeanza kuchukuliwa hasa za kuondoa maji katika maeneo mengine ambayo yalikuwa yakituwama maji kumeanza kupatikana unafuu na jana nilisema mfano wa Karakana na maeneo mengine.

Mhe. Spika, hivi sasa serikali inampango kupitia mradi ZUSP kuondoa maji katika bwawa lile la Mwanakwerekwe kwa kupitia Sebleni, Saateni mpaka baharini ambao ni mradi mkubwa sana ni mradi utagharimu fedha nyingi. Vile vile serikali ina mpango wa kujenga barabara ya Mwanakwerekwe katika eneo lile ikiwa kwa kuongeza kiwango cha juu pamoja na kulijenga daraja kubwa kule Kibonde mzungu, hata hivyo hivi sasa pia serikali imepanga mipango ya kuanzisha miji mipya na kuanza ujenzi wa mji mpya katika maeneo ya mijini na maeneo mengine yalopangwa ni na dhamira ni kuhakikisha kwamba ujenzi wote unafanyika katika maeneo yaliyopimwa na yanafuata taratibu na kupitia kikao hichi kitukufu Mheshimiwa Spika naomba nitoe wito kwamba wananchi waache kabisa kujenga kiholela na wajenge kwa kufuata utaratibu za ujenzi ili kuepuka athari zinazotokea wakati wa mvua na wakati mwengine. Lakini nia ya serikali ni kuliondoa kabisa tatizo hili ili lisiweze kujirudia katika maeneo yote ni vizuri kwa wananchi kuunga mkono jitihada hizi za serikali ili wakati huu tunachukua hatua hizo kuhakikisha madhara haya hayatokei. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Nam. 43

Uboreshaji wa Huduma za Meno katika Kituo cha Afya Kojani

Mhe. Ali Khamis Bakar: Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kujenga Kituo cha Afya kwa wananchi wa Kojani Kisiwani Pemba ili kuwapunguzia kutembea masafa marefu kufuatia huduma ya afya. Hata hivyo, Kituo cha Afya Kojani ninakabiliwa na ukosefu mkubwa wa vifaa na madaktari.

(a) Je, ni lini Wizara itakipatia Kituo cha Afya Kojani Darubuni (*microscope*) kwa ajili ya uchunguzi wa wagonjwa mbali mbali.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kupeleka daktari wa meno atakayehusika na matitabu ya meno katika kituo hicho ili kuondoa tatizo liliopo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Alijibu:

Mhe. Spika, Kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar swali lake namba 43 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kuhusu kupatiwa darubini kituo cha Afya Kojani ni kwamba kituo hicho kilipatiwa darubini hiyo mara tu yalipokamilika matengenezo ya jengo kupitia mradi wa matengenezo ya Vituo vya Afya chini ya Wizara ya Afya kwa mashirikiano na Benki ya Maendeleo ya Afrika *ADB.* Aidha Mtaalam wa Maabara katika kituo hicho pia yupo na anaendelea na kazi zake katika kituo cha Afya cha Kojani.

(b) Mhe. Spika, kituo cha Afya Kojani ni miongoni mwa Vituo vya Afya vya Daraja la pili (*PHCU+)* ambacho pamoja na huduma nyengine kinapaswa kutoa huduma za tiba ya meno. Lakini kwa sasa hivi ni kweli kituo hakina Mtaalam wa memo *Dental therapist*. Hata hivyo, ni dhamira ya serikali kumpeleka Mtaalamu huyo katika kuhakikisha kuwa huduma hiyo inapatikana kituoni hapo. Tayari kiti maalum pamoja na vifaa vyengine vya kutolea huduma hiyo vimeshapelekwa kituoni.

Mheshimiwa Spika Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya itafanya kila liwezekanalo katika kutimiza dhamira hiyo ya serikiali ya kuhakikisha huduma ya meno inatolewa kituoni cha Kojani. Kwa kuanzia huduma hizo zitatolewa angalau mara mbili kwa wiki na kwa kuanzia Mtaalamu kutoka katika Hospitali ya Wilaya ili kuihami hali hiyo.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza, Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, lakini Mhe. Spika, niseme tu kwamba jibu la jawabu langu la (a) mimi sikubaliani nalo kama alivyolieleza kwa sababu Mhe. Spika, mimi hapa nina kitabu cha ripoti ya Wizara ya Afya cha Februari, 2018 ripoti ya Kamati, yasema hivi naomba niinukuu:-

(a) "Kamati iliagiza Wizara ya Afya kufanya matengenezo ya mashine ya kusafishia picha katika Hospital ya Chake chake ili kuondoa usumbufu wanaoupata wananchi wanaohitaji huduma hiyo"

(b) "Kamati ilitoa agizo kwa Wizara ya Afya kufanya utaratibu wa kununua darubini ya uchunguzi kwa jina jengine *microscope* katika kituo cha Kojani" Aidha Kamati iliagiza kupelekwa kwa Daktari wa meno katika kituo hicho.

Mhe. Spika, hapa Kamati iliiona hili jambo kama halipo na jawabu lilikuja kwamba anasema Mheshimiwa hili jambo lilipatikana baada tu ya kituo kujengwa inaonesha dhahiri kama majibu haya hayana uhakika, Je ni lini *microscope* hii itapelekwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Alijibu:

Mhe. Spika, Kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar swali lake la nyongeza ambalo kidogo ameonesha kuwa na shaka juu ya majibu yangu ambayo nimeyatoa.

Mhe. Spika, naomba nirejee jibu langu la msingi ambalo nimelitoa, Kituo cha Afya cha Kojani tayari kina huduma hiyo na *microscope* ambayo ndio kitu ambacho anakilalamikia Mheshimiwa Mwakilishi tayari mashine hiyo imeshapelekwa na inafanyakazi na Mheshimiwa si kwamba nimepewa taarifa ni karibuni tu nimefika mwenyewe katika kituo cha Kojani na nimeshuhudia hicho na mashine bado ipo na mpaka sasa hivi Mheshimiwa naomba, Mheshimiwa Mwakilishi afanye utaratibu awasiliane pia na Mwakilishi wa jimbo husika na vile vile na wataalamu wengine kuthibitisha hicho ambacho nakizungumzia, Mheshimiwa kwa hiyo huduma hiyo ipo na inaendelea kufanyika katika kutuo cha Afya cha Kojani.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swala dogo la nyongeza, Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri yenye ukakasi ukakasi kidogo. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema kwamba itajenga vituo vya afya kila penye kilomita 5 nashukuru sana ilani ya Chama cha Mapinduzi na ndio ilani pekee yenye kusema hivyo kwenye vyama vyote vya siasa lakini Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu na Ziwani kuna vituo vya afya Ndagoni, Wesha, Ziwani na Mbuzini vina uhaba sana vifaa tiba pamoja madawa jee ataniambia nini Mhe. Waziri kuwahakikishia wananchi wangu hao kama wanapata dawa za uhakika na vifaa tiba katika vituo hivyo vya afya katika jimbo langu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kutoa majibu ya nyongeza ya Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani Mhe. Suleiman Makame Ali kama ifuatavyo:

Mhe. Spika kwanza naomba nipokee pongezi ambazo mheshimiwa amezitoa juu ya ilani nzuri ya Chama cha Mapinduzi, nikubaliane na hilo lakini sambamba na hilo mheshimiwa amesema kwamba majibu yetu ambayo kidogo yana mashaka lakini naomba niseme mheshimiwa kwamba majibu ambayo tumeyatoa ni majibu yenye uhakika na hayana shaka yoyote na hatuwezi kuliambia Baraza lako tukufu majibu ambayo yana hofu ndani yake au yana ukakasi.

Hivyo kuhusu swali lake kwamba ni lini au ni kwa utaratibu gani ambao tutaweza kuufanya katika kuona wananchi katika jimbo lake hususan katika kituo kile anachokipigia kelele sana Ndagoni naomba nimuhakikishe Mhe. Mwakilishi kwamba dhamira ya serikali kujenga vituo vya afya sio kuweka majengo tu, badala yake ni kwamba ni kuhakikisha huduma au dhamira ya afya inapatikana katika wananchi wetu waweze kupata huduma pahala popote walipo.

Hivyo nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba tutajitahidi kuendelea kushirikiana na Wizara ya Afya kwa kila linalohitajika katika maeneo ya vituo vya afya hivyo ambavyo vimejengwa, basi tuone huduma zile ambazo zimekusudiwa ziweze kupatikana wakati wowote na nakuomba mheshimiwa tushirikiane tupitishe muda utakapofika bajeti yetu tuone tutafanya nini katika kuhakikisha kwamba huduma zinapatikana katika vituo hivyo.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri mimi naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza kama ituatavyo:

Kwa kuwa azma ya serikali ni kuendeleza afya katika vijiji vyote vya Unguja na Pemba na hivi sasa katika kambi ya KMKM iliyopo Tundauwa tayari wananchi pale wamejitolea kuanzia kituo cha afya ambayo hivi sasa wanapata tiba ingawa si sahihi sana.

Je, Mhe. Waziri yuko tayari kukimalizia kituo hicho pale mfuko wangu wa jimbo utakapokiendeleza. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chonga Mhe. Shaibu Said Ali swali lake la nyongeza kama ifutavyo:

Mheshimiwa ni kwamba juhudi za Mhe. Mwakilishi wa jimbo hili tumekuwa tukizishuhudia mara kwa mara namna ambavyo amekuwa akitoa juhudi zake katika kuhakikisha maendelea ya watu wa Jimbo la Chonga yanapatikana siku hadi siku.

Lakini pamoja na hayo juhudi katika Kituo cha Afya hicho ambacho amekizungumzia cha Tundauwa tayari ofisi yangu kupitia Baraza za Mji Chake Chake tayari kimeanza kuchukua hatua ya kukifanyia ukarabati kituo hicho ili kiweze kutoa huduma kama vile ambavyo zimekusudiwa na serikali. Niseme tu Mhe. Spika tuko tayari kwa sababu tayari huduma zetu tumeshaanza kuchukua hatua hatua kwa vituo mbali mbali na sio cha Tundauwa na vituo vyengine tumeshaanza kuchukua hatua katika kuvikarabati na kuona

ni namna gani tunaweza kupeleka huduma kama zile ambazo tunatakiwa sisi tuweze kupekela.

Nam. 34

Matumizi ya Nyumba ya Kulelea Watoto Mazizini

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Aliuliza:

Mhe. Rais wa awamu ya kwanza ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alianzisha nyumba ya kulelea watoto waliokuwa wakiishi katika mazingira magumu huko Forodhani, hadi miaka ya karibuni watoto hao walipojengewa nyumba mpya na ya kisasa katika eneo la Mazizini. Pamoja na hatua hiyo nzuri ya Serikali, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba baadhi ya vyumba vya nyumba hiyo hufungwa hivyo kusababisha usumbufu kwa watoto hao.

a) Kwa kuwa wananchi wengi walifurahia watoto hao kupelekwa katika nyumba hiyo, Serikali ina kauli gani kutokana na madai hayo.

b) (b) Ni watoto wangapi wanaoishi katika nyumba hiyo katika kipindi hiki.

c) Je, watoto wanaoishi katika nyumba hiyo wanaruhusiwa kuishi humo hadi wafikishe umri wa miaka mingapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza naomba nianza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametuweza asubuhi hii tukaweza kufika hapa katika Baraza lako tukufu tukiwa wazima na wenye afya nje.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu sasa Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi Saada Ramadhan Mwendwa nafasi za wanawake swali namba 34 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli Serikali imewahamisha watoto kutoka Forodhani kuja Mazizini kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo kuchakaa kwa jengo na usalama wao. Nyumba ya Watoto Mazizini ina jumla ya vyumba 26 ambavyo vyote viko huru vinatumika isipokuwa vyumba viwili tu ambavyo ZAYADESA wameweka vifaa vyao tangu mwanzo kabla watoto hao hawajahamia hapo. Vyumba vilivyobaki vinawatosha watoto waliokuwepo kituoni hapo ambapo vyengine vinatumika kama ghala na vyengine wanaishi walezi wao. Kiujumla nyumba ya Mazizini ina uwezo wa kuchukua watoto 104 lakini hadi hivi sasa Mhe. Spika tuna watoto 42 tu.

(b) Mhe. Spika, nyumba ya Mazizini ina jumla ya watoto Arubaini na Mbili (42) wanaoishi hivi sasa Wanawake ni 20 na Wanaume ni 22.

(c) Mhe. Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Uanzishaji wa Makazi ya Sheria ya Mtoto; Mtoto akifika umri wa miaka 18 anatakiwa aondoke kwenye Kituo. Watoto hawa huwa wanaunganishwa na familia zao na utaratibu huu huanza mapema kwa watoto kuunganishwa na familia zao kwa kupelekwa kutembea ili wazoee mazingira ya familia zao. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa: Ahsante Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nilitaka kujua tu.

(a) Kama kutotokea mtoto hana familia mfano kama aliyeokotwa hana familia Serikali inampeleka wapi.

(b) Nataka kujua hii nyumba inayolelewa watoto ni ya Serikali au ni ya ZAYADESA na kama ni ya serikali kwa nini hivyo vyumba wasitowe vitu vyo ikaachiwa wazi ili ikaendelea serikali kuwahudumia watoto wa pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:

(a) Mhe. Spika, kuhusiana na watoto ambao hawana wazazi jee serikali inawapeka wapi watoto hawa. Napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi na wananchi wote kwa ujumla, wale watoto ambao hawana maakazi basi serikali hukaa nao pale tukawasomesha wale na hatimaye watoto wale wakaolewa wakawa na kazi zao.

(b) Mhe. Spika, swali lake la pili waheshimiwa walikuwa wakigonga sana sikuweza kulisikia naomba alirudie.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa: Ahsante Mhe. Spika, swali langu la pili lilikuwa linasema hivi nataka kujua ile nyumba ni ya serikali au ni ya ZAYADESA na kama ni ya serikali kwa nini vile vyumba viwili bado vimeendelea kukaa na vitu wasiovitoa wakaichukua wenyewe serikali, ili serikali ikaendekea kwa mambo mengine. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la pili kama ifuatavyo.

Napenda Waheshimiwa Wawakilishi wafahamu kwamba nyuma ile ya serikali na kuhusiana hivyo viwili anavyozungumzia kwamba kwanini ZAYADESA wameweka vitu vile huu ni utaratibu, lakini ikiwezekana na wala hapana sababu ikashindwa kama tukafika tukazungumza na mhusika aliyeweka vitu vyake akaja akatoa na tukaweza kutumia.

Lakini kama nilivyosema vyumba vilivyopo hivi sasa vinakidhi mahitaji ya kutumia watoto wetu pamoja na walezi wao. Ahsante.

Mhe. Spika: Mheshimiwa swali hili nitawapa wanawake tu. *(Makofi)*

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri napenda kumuuliza swali dogo kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika majibu yake amesema kwamba kwa mujibu wa Kanuni ya Uanzishaji wa Maakazi ya Sheria ya Watoto. Mtoto akifika umri wa miaka kumi na nane atakiwa aondoke katika kituo hicho, nataka kujua kwamba ni watoto wangapi ambao wameshatimia umri ya miaka kumi na nane na hivi sasa wameshakabidhiwa katika familia zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, watoto waliolelewa katika nyumba ya mazizini ambao wamefikia miaka kumi na nane na kurudishwa katika familia zao ni watoto wengi kwa hivi sasa hatuwezi kuwajua, kwa sababu kama nilivyotangulia kusema mwanzo wengine tayari wameshaolewa wanajitegemea na wengine bado tunao pale kama nilivyotatngulia kusema kwamba wale ambao familia zao ni duni hazina uwezo basi serikali wanaendelea kukaa nao.

Lakini kwa mwaka huu watoto ambao tumeweza kuwakabidhi katika familia zao ni watoto sita ambao familia zao zinajiweza kwa kuweza kuwahudumia watoto wale.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Spika kwa kuniona, kwanza nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya ufasaha kabisa.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri umekiri kwamba nyumba hii ya serikali na siyo ya ZAYADESA lakini pia kwa kuwa sote tunafahamu vyumba hivi viwili vimezuwiwa muda mrefu na taasisi ya ZAYADESA jee naomba utuambie na utuhakikishie wananchi ambao wanatusikiliza vyumba hivi viwili ni lini vinakabidhiwa kwa serikali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, niendelee kusema tena kwamba nyumba vilivyokuwepo ishirini na sita vinatosheleza kwa mahitaji yetu ya kusema watoto nakuja....

Mhe. Spika: Waheshimiwa tusikilizane endelea Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kama nilivyotazngulia kusema kwamba vyumba ishirini na sita vilivyokuwepo vinatosheleza kwa mahitaji yetu ya kuweka watoto, walezi pamoja na wengine lakini kutoka na suala la vyumba viwili ambavyo Mhe. Mwakilishi anavizungumzia kwamba ni lini ZAYADESA watakabidhi vyumba vile kwa serikali naomba nimuhakikishie ikiwa mimi ni mshirikiaji wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto nawahakikishia Waheshimiwa Wawakilishi kwamba tutalifuatilia hili tutakaa na wenzetu ZAYADESA ili kuhakikisha kwamba vyumba vile viwili walivyovifungia na kuweka vitu vyao wanatoa na kutupatia ili tuendelee kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa nina swali la upendeleo Mhe. Bihindi Hamad Khamis.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Spika kwa kunipa nafasi ya upendeleo, Mhe. Naibu Waziri napenda kukuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Waziri kuna wafanyakazi wangapi kwenye ile nyumba ya kulelea watoto ambao wanawahudumikia watoto kwa umri wa mwaka mmoja mpaka kufika miaka mitano lakini je, wafanyakazi hao ambao wanahudumikia watoto wana umri ya miaka gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, nyumba ya mazizini tuna wafanyakazi thelathini na mbili ikiwa wafanyakazi kumi na mbili ndiyo wanaotulelea watoto lakini alitaka kufahamu hao walezi wana miaka mingapi ambao wanatulelea watoto wetu.

Mhe. Spika, ikiwa hili Baraza laki ni tukufu na utakiwa uzungumze kitu cha ufasaha sio kudanganya nimuhakikishie kwamba Mhe. Mwakilishi siwezi kujua umri hivi sasa wa walezi wale naomba swali lake hili niweze kumjibu kwa maandishi.

Nam. 188

Mashine za Kupimia Kiwango cha Unyevu wa Karafuu

Mhe. Asha Abdalla Mussa – Aliuliza:

Katika kulinda ubora wa karafuu Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) limenunua mashine za kupimia kiwango cha unyevu wa karafuu.

(a) Je, ni mashine ngapi zimenunuliwa.

(b) Je, fedha zilizotumika katika ununuzi wa mashine hizo kila moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Asha Abdalla Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa suala Nam. 188 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika kulinda ubora wa Karafuu, na katika kukidhi matakwa ya soko Shirika limenunua mashine sita za kupimia unyevu wa karafuu.

(b) Kila mashine moja (1) ilinunuliwa kwa Euro 267 sawa na TZS. 720,900 hivyo, kwa mashine sita (6) zilinunuliwa kwa Euro 1,597 ambapo ni sawa na TZS. 4,325,400.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa mashine hizi bado zinatumia mfumo wa kizamani jee wizara yako ina mpango ya kuhakikisha kwamba zinapatikana mashine ambazo zinatumia mfumo wa kisasa ili tupate karafuu ambazo zilokuwa bora zaidi ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mheshimiwa naomba aseme tena tutatumia mfumo.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Kwa kuwa mashine hizi zilonunuliwa zinatumia mfumo wa kizamani ambazo zinatumia nguvu nyingi kwa ajili ya kupimia karafuu hizi wizara yako ina mpango wa kuhakikisha kwa sasa zinapatikana mashine ambazo zinatumia mfumo wa sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wza Biashara na Viwanda naomba kumjibu Mhe. Asha Abdalla Mussa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mheshimiwa mashine hizi zimenunuliwa kwa kufuata viwango vyote na ndizo mashine zinazotumiwa na hata nchi za wenzetu kwa sababu ndio mashine bora sasa hivi zinazokwenda na wakati.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kumuuliza swali Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa watetezi wa wakwezi na wakulima wa nchi hii nashukuru sana Shirika lako kununua mashine hizi kwa ajili ya kupimia ubora wa karafuu, lakini zamani kulikuwa hakuna mashine hii.

(a) Je kulikuwa na umuhimu wa kiasi gani kuweza kununua mashine hizi wakati hapo zamani tulikuwa tunaangalia karafuu kwa kuikata.

(b) Imetoa ufanisi gani ambayo tunaweza kujivunia baada ya kupata mashine hizo kuona kwamba karafuu yetu imekuwa bora kuliko pale mwanzo ilivyokuwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe Mhe. Abdalla Maulid Diwani kama ifuatavyo.

Mheshimiwa umuhimu upo kwa sababu karafuu tunauza kwa mujibu ya matakwa ya soko la dunia ni lazima zipimwe ubora kwa hivyo umuhimu upo.

Mheshimiwa kuhusu ufanisi mheshimiwa narudia tena ni matakwa ya soko la dunia kwa maana hiyo unapotaka kuuza kitu chako katika soko la dunia lazima upate vielelezo ambavyo vinatokana na soko la dunia inahitajika kitu gani kwa hivyo uliopatikana wateja wetu wanazinunua karafuu zetu kwa wingi kwa sababu zinapimwa kwa mujibu wa matakwa ya soko la dunia lilivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri mwenyewe majibu ya nyongeza.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Naibu Waziri majibu aliyoyajibu ni sahihi lakini tukizungumzia faida Mhe. Spika, huko nyuma tulikuwa tukipokea kesi nyingi sana za karafuu kuambiwa serikali ilipe fidia kwa sababu karafuu zilikuwa zina unyevu ambao haurishi kuna kesi mimi nakumbuka kama miaka kumi na tano nyuma ilikuwa tulipe fidia zaidi ya shilingi dola laki moja na kwa ajili ya karafuu zilikwenda unyevu ulikuwa mkubwa zaidi kuliko unavyotakiwa.

Lakini naomba niseme kwamba kipindi cha miaka hii yote hatujapokea kesi kutoka kwa mteja yoyote kusemba kwamba karafuu zimepelekwa zina unyevu ambao hauridhishi akataka alipwe fidia. Kwa hiyo haya ni mafanikio makubwa na ambayo vile vile Naibu Waziri ameyazungumza na tutaendelea kuhakikisha kwamba karafuu kutoka Zanzibar zinakwenda kwa ubora unatakiwa na akiwemo vile vile unyevu kwamba karafuu zinazotoka Zanzibar zinakwenda kwa ubora unaotakiwa na ikiwemo vile vile unyevu kwamba karafuu zinazotoka ni kavu na zinaridhisha ubora unaotakiwa. Ahsante.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona ukaweza kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri kuna malalamiko ambayo yanatoka kwa wananchi. Pamoja na kuwa Mhe. Waziri kasema kama hakuna mwananchi ambaye amewasilisha lalamiko lake, lakini kuna malalamiko ambayo kuwa yanatoka kwa wananchi kuhusiana na mashine hizo kwamba zinazidi kilo katika upimaji wake ni bei. Kwa hiyo, Mhe. Waziri wizara yako mnalijua hili, na kama mnalijua ni hatua gani za kisheria ambazo mmezichukua ili kurekebisha mashine hizi na kuweza kuondosha kero ambazo wananchi wanazilalamikia.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mhe. Mwakilishi kama sikosei amechanganya suala la kupimia unyevu na suala la kupimia karafuu kwa kilo. Lakini nitaomba kumjibu ni kweli mheshimiwa malalamiko hayo niliyapata kupitia Mwakilishi wa Jimbo la Gando, Mhe. Mariam Thani Juma na hatua niliyoichukua kwa haraka tarehe 1, 2 na 3 nilikuwa Pemba nilikwenda *ZSTC* kwa wataalamu kwamba kuna lalamiko dhidi ya suala la karafuu kupimwa, mashine zinalalamikiwa kwamba ni mbovu.

Mhe. Spika, nashukuru sana *ZSTC* wamechukua hatua bora mashine zote tunazopimia karafuu *ZSTC* zinatoka India tumenunua vipuri vipya na kuzi-*repair* mashine zote za kupimia karafuu Pemba. Kwa maana hiyo, ni matarajio yangu mheshimiwa malalamiko hayo hayatakuwepo tena kazi tumeifanya na ni nzuri na kama utayasikia malalamiko ya aina hiyo mheshimiwa naomba uniletee ili Wizara ya Biashara na Viwanda iyafanyie kazi. Ahsante.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu kwa majibu yake mazuri, lakini katika majibu yake amekiri kwamba mashine wamezinunua India na kulikuwa kuna tatizo wakafika kununua vipuri kuzifanyia marekebisho. Maana yake kama wamefanya marekebisho inaonekana kwamba huko nyuma zilikuwa zina matatizo, na kama zilikuwa zina matatizo maana yake kuna wananchi ambao wamewadhulumu.

Je, wale wote ambao walilalamika na wao wenyewe wizara wakabaini kufanya marekebisho kuna fidia yoyote ambayo wamewalipa wale waliolalamika.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, mashine zilikuwa nzima na zinafanya kazi, lakini malalamiko ni jambo la kawaida. Kwa mfano, mwananchi anachukua karafuu zake nyumbani anapima kwa kutumia pishi, na pishi anayoitumia ni pishi ya kileo, pishi ya zamani kama unaikumbuka mimi bibi yangu alikuwa nayo ni pishi ya shaba. Pishi ya shaba na pishi ya leo ni tofauti unapozipeleka *ZSTC* unategemea zikapimwe kwa pishi ya shaba ambayo haipo.

Kwa hivyo, mheshimiwa *ZSTC* tunanunua karafuu kutumia kilo, lakini mashine zilikuwa zinalalamikiwa kwa sababu kumbuka kipindi cha msimu wa karafuu, karafuu zinazopelekwa ni nyingi. Kwa hivyo, mashine lazima zitakuwa zimechoka kupima karafuu kwa kipindi kile, kwa hivyo kila mwaka tutapomaliza msimu lazima mashine zile tunazifanyia *repair*. Kwa hivyo, tumezifanyia *repair* na hiyo inaendelea kila mwaka tunapomaliza na sasa hivi mashine zote ni nzima na huo ni utaratibu wa kawaida kwamba kila tunapomaliza msimu lazima mashine zile za kupimia unyevu na kila kitu tuzifanyie *repair*.

Mhe. Spika, kama malalamiko kama yalikuwepo ni mambo ya kawaida lakini malalamiko hayo kama Wizara ya Biashara na Viwanda ni kuyachukua na kuyafanyia kazi. Kwa hiyo, mheshimiwa hata wewe ukiyakuta tuletee lakini sisi kazi yetu ni kuyafanyia kazi malalamiko tuliyoletewa.

Nam. 131

Uchimbaji wa Visima vya Maji kwa Watu Binafsi

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendeleza jitihada za kuleta huduma za Maji. Na kutoa ruhusa ya kuchimba visima kwa watu binafsi katika majimbo yao.

(a) Je, kuna utaratibu gani unaotumika mpaka mtu akapata kibali cha kuchimba kisima au kila mtu anachimba tu.

(b) Ni umbali gani unaohitajika kuwepo baina ya kisima kinachochimbwa na shimo la choo.

(c) Je, maji yanayotoka katika visima hivyo yanakaguliwa kabla ya kutumika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 131 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji ina utaratibu maalum kwa watu wanaochimba visima binafsi, utaratibu huo unamtaka mwananchi kuandika barua kwa Mamlaka kabla ya kuchimba kisima hicho, baadae Mamlaka inapeleka maafisa kwa ajili ya kukagua eneo linalotaka kuchimbwa kisima na baada ya ukaguzi huo wanatoa ushauri wa kufaa au kutofaa kwa eneo husika kuchimbwa kisima, na baadae kutoa kibali maalum cha kuchimba kisima kwa muhusika.

(b) Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria Nam.4 ya 2006 ya Mamlaka ya Maji inaruhusu kuchimba kisima umbali wa mita 100 kutoka mashimo ama makaro.

(c) Mhe. Spika**,** baada ya kupata taarifa ya kukamilika kwa kisima kutoka kwa mwananchi, *ZAWA* humtaka mwananchi huyo kujisajili na kushauriwa kuchukua dawa kwa ajili ya kutibu maji.

Mhe.. Spika, *ZAWA* inapenda kuchukua fursa hii kuwaomba wananchi wanaotaka au waliokwisha kuchimba visima kufika Mamlaka ya Maji na kusajili visima vyao pamoja na kupata ushauri wa ubora wa maji wanaotumia sambamba na kupata dawa ya kutibu maji hayo ambayo inatolewa bure bila ya malipo yoyote kwa mwananchi.

Kwa watu wanaoufata utaratibu wa kuomba kuchimba visima, kupitia maji yao yanafanyiwa ukaguzi na kupatiwa majibu na kushauriwa njia nzuri ya kutumia maji hayo ikiwa ni pamoja na kupatiwa dawa ya kutibu maji. Ahsante sana mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi nashukuru sana majibu ya Mhe. Naibu Waziri, mimi nimwambie tu kwamba katika swali lake la (b) ni kwamba kisima kinachimbwa mita 100 umbali wa makaro au mashimo. Lakini takriban visima vingi vinachimbwa katika miji ambayo ndio tatizo kubwa la maji, na hakuna kiwanja sifikirii kama kinazidi mita 50 na kila nyumba ina kisima, pengine mpaka huu tu kachimba mashimo mpaka wa ndani mwako wa mtu mwengine pana karo.

a) Sasa namuuliza Mhe. Naibu Waziri hii sheria bado inafanya kazi au hii sheria itabadilishwa kwa sababu kwa mita 100 kwa Mjini ni eneo kubwa sana halikidhi haja hiyo.

b) Mhe. Spika, lakini nimuulize tena Mhe. Naibu Waziri kwamba kwa swali (b) *ZAWA* ndio waliopewa mamlaka ya kuhakikisha kwamba Zanzibar inapata maji safi na salama. Watu wanaochimba visima kutokana na shida ya maji, wamechimba kutokana na *ZAWA* kutokutosheleza maji. Sasa je, *ZAWA* wanapitia watu majumbani kuvikagua visima, kuviweka dawa au bado *system* ni kumsubiri mtu aende akapeleke malalamiko yake ndio atibiwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b).

Mhe. Spika, ni kwamba sheria ipo na sheria kilichozingatia ni usalama wa watumiaji wa maji hayo. Sasa kinachoshauriwa ni vyema mtu akaja akajisajili kusudi wataalamu waende lakini pia walileta maji Mamlaka kwa ajili ya kupima, tunachokitaka wananchi watumie maji safi na salama inawezekana hata haikufika mita 100 lakini kama maji yako salama yatakuwa yanafaa kutumia, ndio maana tunashauri na kusisitiza kwamba maji ni muhimu yatufike kwa ajili ya kuyapima na tuyape dawa inayohusika. Ahsante sana lakini la swali la (b) ningeomba urejee.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nashukuru narudia swali (b) nasema *ZAWA* ndio wenye mamlaka ya kuwapa Wazanzibari maji safi na salama, sasa *ZAWA* wamesema kwamba wanamtaka mtu aende katika ofisi ili akaeleze matatizo yake na kuchukua dawa. Hawaoni kwamba ni muhimu wa *ZAWA* kupita kila nyumba yenye kisima kwa kuyafanyia matibabu na kumpa mwelekeo yule mwenye kisima ili kuweka katika hali ya maji safi na salama kuliko mtu yule kuja ofisini kwamba unaweza ukampa hizo dawa na azisifikishe katika mazingira hayo. Hawaoni umuhimu *ZAWA* kutenga kitengo maalum cha kupitia visima kuvitibu na kuweza kutoa maelekezo kuhusu kisima kile.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza la (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, umuhimu tunauona na ndio maana tunasisitiza lakini umuhimu huu upo kwenye pande zote mbili husika kwa Mamlaka lakini pia kwa mwananchi. Mamlaka wanajitahidi kupita lakini inawezekana wasijue kama nyumba fulani ina kisima. Ni wajibu wako wewe sasa kwenda kusema hapa kisima kipo na watimize wajibu wao kukuletea dawa ama kwenda kuchukua dawa, ni pande zote mbili husika. Ahsante sana.

Mhe. Machano Othman Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Zanzibar ni kisiwa na katika tafiti za zamani ilionesha kwamba uchimbaji wa visima vingi ni hatari sana kwa nchi yetu ya Zanzibar, lakini kutokana na matatizo ya maji yanayowakabili wananchi wa Zanzibar hivi sasa tumekuwa na visima kila jimbo visivyopungua kumi mpaka ishirini pamoja na serikali kuchimba visima 150 kupitia Ras al-Khaimah. Je, serikali haioni hatari ya Zanzibar kuja kuharibika baadae kutokana na wingi wa visima.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Cha msingi kwanza tunachozingatia ni upatikanaji wa maji na nilivyosema kwamba Mamlaka *ZAWA* imechimba visima 150 lakini sio hivyo tu ina takriban visima 400 kwa ujumla wake yote ni jitihada ya kuhakikisha kwamba maji yanafika. Lakini pia wananchi au viongozi wa majimbo wanajitahidi kuchimba visima kwa ajili ya urahisishaji wa upatikanaji wa maji. Lakini tunakuja ile hoja ya mwanzo kwamba ipo haja ya kabla ya kuchimba tukapata ushauri kusudi kulikimbia hilo, hilo la kwamba si kila pahala pachimbwe tu kisima, lakini pia maji ambayo yanapatikana baadae yawe safi na salama. Ahsante sana.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, tangu nimechaguliwa katika Baraza hili la Wawakilishi katika eneo la Mjonga eneo la Tunguu pamoja na Ungujaukuu Kaibona tumekuwa tuna visima ambavyo vilichimbwa vyengine vipo vilichimbwa na wachina lakini vyengine pia vilichimbwa na Kampuni ya Ras al-Khaimah na matangi kujengwa.

a) Je, ni lini Mhe. Naibu Waziri visima hivi vitaanza kutoa huduma kwa wananchi, maana yake hata wewe mwenyewe Mhe. Naibu Waziri umeshafanya ziara.

b) Katika Mkoa wa Kusini, kisiwa cha Uzi, kijiji cha Ng'ambwa najua kumekuwa na ukakasi mara nyingi viongozi kufika hasa mawaziri bado hawajafika katika eneo lile, lakini kwenye tatizo la maji ni wakichimba visima wanapata maji ya chumvi. Je, serikali ina mpango gani kuwasaidia wananchi hawa hasa kwa vile utaalamu ambao wizara na taasisi yenyewe ya *ZAWA* kuweza kuwasaidia wananchi wa kisiwa cha Uzi hasa kijiji cha Ng'ambwa ili kuondoka na kaadhia hii ya kukosa maji safi na salama. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali la nyongeza. Ni kweli kwamba maeneo ya Mjonga kuna kisima na mimi pia nimefika kwa ajili ya kuviona tunatafuta nguvu ya kuviunganisha visima vile. Lakini nimuhakikishie kwamba ikiwa hapa kati hatujapata nguvu za kuviunganisha kwenye mradi ule wa India vile visima vyote

vitakuwa vimeingizwa kwa sababu tayari tumempitisha mshauri muelekezi tumempitisha katika *zone* ambazo tunataka ule mradi uzingatie ikiwemo katika eneo lile.

Mhe. Spika, lakini tukija katika swali (b) hivi sasa tuna mazungumzo na marafiki zetu kuhusu kuweka mitambo ya kubadilishia maji ya chumvi kwenda maji ya kunywa katika maeneo yale ya mkakati kama eneo ambalo amelitaja. Wacha nikakae na Mamlaka tuone huko tunakuzingatia vipi kuhusiana na hili. Ahsante sana.

Nam. 278

Malalamiko ya Upotevu wa Dawa za Serikali Unaofanywa na Baadhi ya Wafanyakazi

Mhe. Rashid Makame Shamsi – Aliuliza:

Pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na serikali kupitia Wizara ya Afya katika kuimarisha huduma na Afya husunan katika kupunguza tatizo la upatikanaji wa dawa katika hospitali zetu, bado kuna malalamiko kuwa wapo baadhi ya wafanyakazi wasio waaminifu wanaiba na kuziuza dawa za serikali katika maduka binafsi ya dawa.

(a) Je, jambo hili lina ukweli na uzito wa kiasi gani.

(b) Je, kama ni kweli, huoni kuwa tatizo hili linarejesha nyuma juhudi za serikali sambamba na kupunguza imani ya wananchi kwa serikali yao.

(c) Je, ni juhudi gani wizara inachukua kuona tatizo hilo liondolewa na wahusika kuchukuliwa hatua zinazostahiki.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 278 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa niaba ya Wizara ya Afya napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa msimamo madhubuti alionao wa kusimamia na kutekeleza, Sera na maagizo ya Muasisi wa Afro Shirazi Party, na Rais wa Kwanza wa Zanzibar Marehemu Abeid Amani Karume ya kutoa huduma za matibabu kwa wananchi wote bila ya malipo.

Mhe. Spika, kutokana na wizara yangu kupokea malalamiko na shutma ya uuzwaji wa dawa za serikali katika maduka na hospitali binafsi, na kwamba wahusika ni baadhi ya wafanyakazi wetu, wizara imechukua hatua za kufanya uchunguzi kwa lengo la kupata ukweli wa shutuma hizi pamoja na kuwabaini wafanyakazi wanaohusika.

Hivyo, napenda kulieleza Baraza lakotu kwamba mfanyakazi yeyote atakayebainika kuhusika kuuza dawa za serikali aidha kwa maduka, hospitali binafsi au kwa mgonjwa hatutomvumilia na hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja dhidi yake.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba kujibu swali (a) linalosema je jambo hili lina ukweli…

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri samahani usiyarudie maswali jibu tu moja kwa moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: *Okay*, ahsante nakushukuru.

Mhe. Spika, Waswahili wanasema kwamba 'liambiwalo lipo na kama halipo lipo linakuja'.

a) Na ndio maana kwa kuthamini msemo huu Wizara ya Afya tukaunda na tukaamua kufanya uchunguzi wa jambo hili. Sasa ukweli wa jambo hili waheshimiwa utapatikana baada ya kukamilika kwa uchunguzi huo unaoendelea kama nilivyoeleza awali na tunakiri kwamba uzito wa jambo hili ni mkubwa na kwa sababu linagusa haki za msingi za wananchi za kupata matibabu bila ya malipo na bila ya ubaguzi wowote.

(a) Wizara inawaomba wananchi waendelee kuwa na imani huku wakijua kwamba serikali haiko pamoja na yeyote atakayebainika kuhusika na ubadhirifu huu. Tunaomba mashirikiano ili kuwatambua.

(b) Katika kudhibiti ubadhirifu na wizi wa dawa wizara inachukua juhudi mbali mbali zikiwemo za kufungwa *CCTV camera* katika maeneo ya kuhifadhia madawa (BOHARI KUU) na *store,* pia kuunda kamati maalum ili kuangalia mwenendo mzima wa dawa hadi kumfikia mgonjwa pamoja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na wakustukiza bila ya kujali siku au wakati.

Mhe. Spika, hatua nyengine tuliyoichukua ni kuweka mabango maalum katika baadhi ya hospitali yanasomeka "SI RUHUSA KUUZA AU KUNUNUA DAWA KATIKA ENEO LA HOSPITALI". Lengo la wizara ni kuweka mabango hayo katika hospitali na vituo vyote vya afya Unguja na Pemba ili kuwasaidia wagonjwa kutokununua dawa ambazo zipo kwa ajili yao na wanastashiliki kuzipata bila ya malipo yoyote. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019, tumeandaa mpango maalum wa kuweka dawa zote za serikali nembo maalum ya kuonesha kwamba dawa hizo ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, wizara inawaomba wananchi kutokua wepesi kununua dawa ziuzwazo katika hospitali na vituo vya afya, kwani dawa hizo ni haki yao na walipaswa wapewe bila ya malipo yoyote. Na watapo baini dalili za kuuziwa dawa hizo tunawaomba wasisite kutoa taarifa kwa viongozi wanaohusika. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza, lakini pamoja na majibu mazuri sana ambayo yamepangika ya Mhe. Naibu Waziri kupitia Wizara yake ya Afya, kwanza nimpongeze kwa hilo.

Mhe. Spika, waziri katika jibu lake la (a) amesema kwamba ukweli wa jambo hili utapatikana baada ya kukamilika kwa uchunguzi ambao unaendelea.

Swali langu la kwanza ni kwamba, uchunguzi huu umeanza lini na Baraza hili pamoja na wananchi watarajie matokeo ya uchunguzi huu lini?

Swali la pili, kutokana na jawabu ya Mhe. Waziri ni kwamba juu ya suala zima la kutoa taarifa kwa wale ambao watakumbwa na kadhia hizi kwa wahusika, kwa nini wizara isiweke nambari maalumu ya simu ya mhusika wa Wizara ya Afya ili wananchi wenye malalamiko katika huduma za afya iwe rahisi kwao kuweza kuripoti matukio haya, kama yalivyo katika Zimamoto au katika Polisi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi swali lake la nyongeza (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Suala hili la kutaka kujua mipango hii imeanza lini, mara tu tulipopata uteuzi wa waziri mpya katika wizara yetu tulikaa na kupanga mipango mbali mbali ya kuhakikisha huduma za afya zinapatikana vizuri katika hospitali zetu. Kwa hivyo, moja tulilolipanga ni hili la kuhakikisha tunawadhibiti hawa wanaouza dawa. Kwa hivyo, kuanzia hapo tulipanga mkakati maalum na sasa hivi unashughulikiwa unakwenda vizuri na baada ya muda mfupi Waheshimiwa wategemee kwamba wataona matokeo.

(b) Kuhusu hawa wahusika kuwa watoe taarifa vipi, mara nyingi tunapokwenda kwenye mikutano mbali mbali na hata ya hadhara mfano ya uchangiaji wa damu, basi nalieleza jambo hili na tunatoa nambari za simu za viongozi ambao wanapaswa wapigiwe kama litatokea tatizo hilo. Tumeshaanza kupokea simu mbali mbali za malalamiko na kuanza kuzichukulia hatua. Sasa kama utaniruhusu Mheshimiwa niwape hapa hapa niwatajie baadhi ya nambari za simu ambazo waheshimiwa na wananchi wazitumie Mheshimiwa *I'm read.*

Kwanza ni nambari ya Mhe. Waziri wa Afya ambayo ni 0773-865662, lakini ya pili ni nambari ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya 0777-497883, lakini ya tatu ni ya Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ambayo ni 0777-432465. Nyengine ni nambari ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya ambayo ni 0777-423165, nyengine ya Naibu Katibu Mkuu ambayo ni 0777-412512, nyengine ni ya Mkurugenzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo ni **055-554065**. Mheshimiwa naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mhe. Rashid Makame Shamsi nimekuona samahani, kama hukuridhika nafikiri akirudi hebu jaribu kuzungumza naye hapo kama hukuridhika na majibu. Mhe. Nadir Abdul-latif tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Spika, mimi nitaomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri wa Afya swali la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Kwa kuwa ametueleza kwamba sehemu zinazotoa dawa wamefunga *CCTV* ni vituo vingapi vinavyotoa dawa kwa wananchi Unguja na Pemba na ambavyo vimeshafungwa *CCTV Camera* ambazo zinarikodi.

(b) Ni nani anaye *control* hizo *CCTV Camera* kuweza kuwakamata hao wezi kwa njia hiyo, kwa sababu inarikodi masaa 24.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa hatua za awali tumefunga katika ghala kuu la madawa (Bohari Kuu) iliyopo Maruhubi na ambaye anaratibu pale ni Mkurugenzi husika ambaye yupo pale. Lakini pia kuna mfanyakazi maalumu ambaye yupo anashughulika na *CCTV machine* ile, tunategemea sana kupata matokeo mazuri.

Pili, Mheshimiwa naomba arejee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, swali la (b) nimemuuliza kwa kuwa *CCTV Camera* inarikodi masaa 24 nani anaweza kui-*surveillance* ile *camera* ambaye ataweza kukamata sehemu zote, nani katoa kwa njia ya magendo na nani kauza.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, pale anayehusika ni Mkurugenzi wa Bohari, lakini anayeangalia kwa masaa 24 pia yuko mfanyakazi anayefanya hivyo ambaye kachukua magendo, hilo jambo halijatokea. Kwa hivyo, hatujawahi kuliratibu.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi tena ya kuweza kuuliza swali. Mhe. Naibu Waziri katika vijiji vyetu kuna maduka ya chakula asilimia 90 dawa hizi zinapatikana zikiwemo *panadol*, dakika tatu, dawa za kifua na nyenginezo. Je, suala hili analijua? Kama analijua ni hatua gani ambazo wamezichukua.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli anavyosema Mhe. Ali Khamis Bakar kwamba yako maduka madogo madogo hasa vijijini na kweli wanauza dawa za binadamu. Hatua ambayo tunaichukua taasisi yetu ya ukaguzi wa dawa, chakula na vipodozi huwa inapita katika maduka na ikikuta kwa kweli hatua kali zinachukuliwa pamoja na kufungiwa kuuza dawa. Isipokuwa baadhi ya vijiji wanafanya jambo hili kwa siri. Lakini kama ana ushahidi wa duka ambalo analijua wanaendelea kuuza kwa sababu tunalikemea basi atueleze ili taasisi hii inayohusika ipite na naomba kutoa wito kwa wananchi kwamba, dawa zile zinazouzwa katika maduka yale madogo madogo si salama. Kwa sababu wanauza dawa ambazo zimeshapitwa na wakati. Ahsante Mheshimiwa.

Nam. 60

Usajili wa Bodaboda Nchini

Mhe. Said Omar Said – Aliuliza:

Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa naomba nifanye masahihisho tu kidogo katika *paragraph* ya mwisho inayosema 'kwenda na kurudi muafaka' isomeke hivi, 'kwenda na kurudi kwa wakati muafaka'. Baada ya marekebisho hayo naomba sasa nijibiwe swali langu nambari 60.

Kwa kuwa baadhi ya maeneo hayajafikiwa na huduma za usafiri wa daladala kutokana na kukosekana kwa miundombinu ya barabara hususan maeneo yaliyo kando na miji yetu na kupelekea usumbufu mkubwa wa usafiri kwenda na kurudi kwa wakati muafaka katika shughuli zao za kimaendeleo ya maisha.

Je, serikali ina mpango gani wa kusajili usafisi wa pikipiki (bodaboda) katika maeneo hayo ili ziweze kuwahudumia wananchi.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa tena ya kujibu maswali ya Mhe. Said Omar Said kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa maisha tunayoishi sasa usafiri ni jambo muhimu kwa kila mtu, ukiwemo usafiri wa barabarani. Usafiri huo una sheria na taratibu zake na kuna vyombo maalumu ambavyo vimeruhusiwa kufanya kazi hiyo na huwa vinapewa leseni na kurasimishwa. Usafiri wa pikipiki (maarufu kama bodaboda) kwa kusafirisha abiria haumo katika vyombo vya moto vilivyoruhusiwa na kurasimishwa Zanzibar. Ingawa Mheshimiwa amependekeza usafiri huo utumike Zanzibar hasa katika maeneo yaliyokuwa hayana usafiri wa daladala, wazo lake lingekuwa na mantiki kama tu, kungekuwa na sheria inayounga mkono pendekezo hilo ili itekelezeke kwa mujibu wa sheria hiyo.

Mhe. Spika, ingawa kuna nchi nyingi zimefanya hivyo na pikipiki kuwa ni vyombo vya biashara, lakini zinazofanya vizuri ni zile ambazo sheria za usalama barabarani zinafuatwa na usafiri huo umekuwa na tija kwa wananchi wake. Lakini kwa nchi ambazo sheria za barabarani hazitiliwi mkazo ipaswavyo na wananchi wake hawazifuati na rushwa ikawa ndio maisha ya kawaida kwao, basi usafiri huo umekuwa ni janga la kitaifa.

Mhe. Spika, kwa kutilia maanani ombi hilo, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar imeiagiza Bodi ya Usafiri Barabarani, imepewa jukumu la kufanya utafitiili kuangalia faida na hasara za usafiri wa bodaboda kwa kwenda kuangalia sehemu ambazo usafiri huu unatumika ili iweze kumshauri waziri ipasavyo.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa serikali haijaamua kusajili bodaboda ikapata faida tatu, moja ikapata kodi, pili kuwasaidia wananchi na tatu ajira. Je, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia jamii kupata usafiri wa uhakika katika barabara za ndani. Kwa mfano, Wingwi Mapofu kuelekea Shumbaviamboni, Mzambarautakao kuelekea Finya na kwengineko. Mheshimiwa nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Said Omar Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Faida tatu alizozitaja kweli zingepatikana kama bodaboda zingesajiliwa, tungepata kodi, tungewasaidia wananchi na ajira pia. Lakini hakuna kitu kisichokuwa na taratibu na kwa kweli kwa vile watu wa usafiri wa ndani wanapata shida barabara zile na leseni kila mwaka zinarekebishwa. Kwa hivyo, barabara zikiwa zinapitika leseni zinatolewa kwa barabara zile, sasa kama barabara hizo zitaingia kwenye *list* ya zile ambazo zinapitika na wale watu wa leseni wakakubali kwamba hizo barabara zinaweza kupelekewa daladala watapewa leseni watapiutisha daladala katika sehemu hiyo.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kituo cha daladala cha Kijichi kiko chini ya kilima ni hatarishi kwa waendesha gari, lakini pia kwa wanaosubiri gari kwenda mjini. Manispaa ya Magharibi 'A' iliomba kituo kile kihamishiwe kipelekwe Mndo lakini ofisi yake bado inakuwa nzito kukikubalia kituo kile kupelekwa Mndo.

Ni lini kituo kitahamishwa pale ili tusisababishe ajali kwa wananchi. Hilo la kwanza.

La pili, daladala za Kianga zinaishia Dole, lakini daladala zile wananchi walitaka kifikishwe Mndo na pale itasaidia wafanyakazi wa Kituo cha Kilimo Kizimbani, lakini Askari wa Magereza na wanafunzi wa Chuo cha Kilimo cha Kizimbani. Je, ni lini wizara yake itakubali daladala zile za Kianga zifike Mndo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Bububu swali lake kama hivi ifuatavyo. Watu wa leseni wanapopanga njia za kupita daladala na kuweka vituo huwa kuna taratibu nazo ambazo wanazifuata, si suala tu la kila mwananchi kutaka kuhamisha hapa peleka pale. Lakini kama anavyosema kama kituo cha Bububu kinahatarisha maisha na tukawa na uhakika kwamba kweli tukifanya utafiti tukakuta maisha mengi yamehatarishwa. Mimi mwenyewe nitachukua dhamana kuwaambia kwamba hiki kituo hapa kiondosheni kwa sababu hatutaki wananchi wetu wapate matatizo wala kufariki. Lakini hilo kwanza itabidi nikalifanyie utafiti niwe na uhakika nalo ili kuweza kutoa ruhusa hiyo. Kwa sababu wao nao wana vigezo vyao kwa nini wanaweka hivyo.

Pia daladala za Kianga kuishia Mndo hivyo ndivyo anavyotaka yeye lakini taratibu ndio hizo kama nilizosema mwanzo. Kuna maelekezo na sababu maalumu kwa nini wanatoa ruhusa kutoka sehemu moja kwenda nyengine. Sasa si suala tu la kutaka, lakini hata hivyo, nitawauliza kama wataweza kuwasaidia tufanye hivyo na kama kutakuwa hakuendani kinyume na hizo sheria zao.

Mhe. Spika: Waheshimiwa kwa sababu ya muda nitaenda kwenye swali linalofuata kwa wizara hii hii. Swali linaulizwa na Mhe. Bahati Khamis Kombo.

Nam. 89

Ujenzi wa Barabara Kutukuu – Wambaa

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawasaidia wananchi kuleta maendeleo nchini. Aidha, wawakilishi katika kusimamia vyema Ilani ya Chama cha Mapinduzi husaidia kutengeneza miundombinu ya maji na barabara. Hata hivyo, miundombinu hiyo kutokufikia kiwango kutokana na uwezo mdogo wa kifedha katika utekelezaji wa kazi hizo.

Je, wizara itawasaidia vipi wananchi wa Kutukuu - Wambaa ili waweze kuondokana na tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:

Mhe. Spika, naomba ruhusa yako kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 89 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji si mmiliki wa barabara za vijijini kutokana na mambo ya ugatuzi, bali barabara hizo ziko chini ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Kwa vile Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ni wizara mama na barabara ndio vilio vyote vinaelekezwa kwake. Ushauri na maelekezo tuliyonayo sote wenye barabara ni kwamba, tukutane wizara zote wenye barabara hizo ikiwemo Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Wizara ya Kilimo ambao wana barabara za *MIVARF* zinazotoa mazao shambani kupeleka barabara kuu pamoja na Wizara ya Tawala za Mikoa wenye barabara za vijijini, Wawakilishi na Wabunge wa sehemu husika wenye barabara hizo, ili kwa pamoja tutengeneze kamati ambayo inatakiwa ipange mikakati na mipango halafu tuifanye kazi na kuhakikisha ufanisi wa miundombinu ya barabara katika vijiji vyote vya Unguja na Pemba. Tukiungana kwa pamoja kila mmoja kwa nafasi yake hili suala la barabara za vijijini zitakamilika kwa kiwango kinachotakiwa. Sasa haya yatatekelezeka kulingana na upatikanaji wa fedha. Hivyo, tunapenda kuwaarifu wananchi wa Kutukuu – Wambaa na wengineo wote wastahamili, kamati inaundwa na tutalisimamia kulishughulikia tatizo hilo.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye ufasaha ambao ufasaha huo nadhani wananchi wa Kutukuu - Wambaa utawapa matumaini mazuri. Lakini naomba kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mhe. Waziri barabara hii ya Kutukuu - Wambaa wananchi waliiomba zamani kabla ya ugatuzi na sasa hivi barabara hii inapelekwa Tawala za Mikoa na nikiwa mwakilishi husika wa jimbo lile tayari Mfuko mzima wa jimbo ambao ni shilingi 20 milioni zote nilizielekeza Wambaa.

Je, Mhe. Waziri hatuoni kwamba wananchi hawa hatutowatendea haki ikiwa hivi sasa barabara hii bado haijamaliza kutengenezwa na tayari tunaipeleka Wizara ya Tawala za Mikoa. Tukiangalia Tawala za Mikoa bado wana matatizo makubwa ya barabara zote za Mkoa wa Kusini Pemba zilizoko ndani. Je, Mhe. Waziri utaratibu gani utatumika ili kuweza kuwasaidia tena wananchi wa Kutukuu - Wambaa. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, suala la barabara katika suala la ugatuzi hilo haliepukiki, kweli walipoleta lilikuwa kwetu, lakini madhali limeshapelekwa kwenye ugatuzi na huko ndiko linakostahili kuwa itabidi tukubaliane nalo, kwa sababu hizo ni barabara za vijijini na zote ziko chini ya utawala wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kweli lililetwa kabla hizo hazijenda huko zilipokuwa mikononi mwetu, lakini nimeshasema kwamba na mimi nimo humo humo kwenye kamati na Tawala za Mikoa na watu wa kilimo. Sasa tutajaribu kuangalia kuzipa kipaumbele zile za mwanzo ambazo zilikuja mwanzo kwetu halafu na nyengine zitafuata. Hilo tu ndilo nitakaloweza kumsaidia Mheshimiwa ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi tena kuweza kuuliza swali. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Waziri ni lini barabara ya jimbo langu la Tumbe kutoka Kizota hadi Finya itajengwa kwa kiwango cha lami ikiwa barabara hii haiko Tawala za Mikoa.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, tunapojenga barabara kuna mambo yanaangaliwa na uwezo pia tulionao, barabara aliyoitaja tunaifahamu tunayo kwenye *list* yetu na mipango tunapanga. Tunaangalia kwanza tunapopeleka barabara ile inasaidia vipi wananchi wengi kwa kipindi kile na shida zilizoko pale. Bara bara yako imo nimeshakwenda kuiona kwa macho yangu kwa hiyo nafikiri katika barabara ambazo zitafanyiwa kazi na hiyo imo.

Nam. 86

Tatizo la Mishahara kwa Wafanyakazi wa Mashamba ya Mipira Pemba

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa wafanyakazi wa mashamba ya mipira kwa upande wa Pemba hawaendelei kugema kutokana na matatizo ya mishahara ya wafanyakazi hao, tatizo ambalo limekuwa likijirudia rudia kila mara kati ya wafanyakazi na kampuni zinazopewa au kukodishwa mashamba hayo.

(a) Je, nini hasa tatizo la msingi linalosababisha wafanyakazi hao wa mashamba ya mpira kutolipwa mishahara yao kwa wakati.

(b) Je, kampuni iliyopewa au iliyokodishwa mashamba inamilikiwa na nani.

(c) Je, ili kuhakikisha kwamba mashamba ya mpira yanatoa mazao kama ilivyokusudiwa, serikali ina mkakati gani kwa kampuni zinazokodi mashamba hayo kuweza kuyaboresha ili yaweze kuzalisha zaidi kinyume na hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu**:**

Mhe. Spika**,** kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 86 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Lakini kabla sijajibu swali napenda niseme yafuatayo:-

Kwanza kabisa namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa salama, Mwenyezi Mungu huyu mwenye wingi wa Rehma, Aza wa Jaala anaetupa neema zote tuzijuazo na tusizozijua, tunazoziona na tusizoziona, tunazozifikiria na tusizozifikiria na tuzihisizo na tuzizozihisi.

(a) Mhe. Spika, mashamba ya mipira kwa Unguja na Pemba yamekuwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha na Mipango baada ya kuwekeana mikataba na Makampuni ambayo yalikodishwa mashamba hayo kwa nyakati tofauti. Hivyo, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaendelea kutafuta taarifa sahihi za wakati huo kuhusiana na malipo ya mishahara ya wafanyakazi waliajiriwa na Makampuni yaliyokodishwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha.

(b) Mhe. Spika**,** umiliki wa Makampuni yaliyowahi kukodishwa mashamba ya mpira ni kama ifutavyo:

Jina la Kampuni	Asili	Mwaka
Compass Holdings Company Ltd.	Kenya	1991 – 1995
Mercantile Freighters Ltd	Kenya	1995 – 1996
A.K. Rubber Ltd	Zanzibar	1996 - 2002
Agrotex Company Ltd	Zanzibar	2003 – 2016

(c) Mhe. Spika, kama tulivyoeleza hapo awali, mashamba ya mipira yalikuwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha na Mipango hadi tarehe 07/08/2017 ambapo ndio yamekabidhiwa kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Aidha, napenda kumfahamisha mjumbe kwamba mashamba ya mipira kwa Unguja na Pemba yamepungua uzalishaji yamepungua uwezo wake kiuzalishaji kiuchumi. Kwa hiyo, Wizara Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi tayari imeshaandaa rasimu ya mpango wa usimamizi wa mashamba hayo unaolenga kuyaendeleza maeneo yote yenye mipira, ikiwemo kupanda miti ya biashara, viungo na miti ya asili ya misitu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo kwa niaba ya Waziri wake swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza ni jambo la kusikitisha sana kusema kwamba Wizara ya Serikali haina taarifa juu ya hilo ni jambo la kusikitisha sana. Lakini napenda niulize kwa sababu katika Jimbo langu la Konde yapo mashamba ya Mipira na wananchi wangu bado wanaendelea kulalamika kwamba mashamba hayo wamiliki waliokodishwa hawawalipi mishahara kwa wakati na bado hayo mashamba huo utaratibu haujafikia.

Mimi nilitaka nijue ni lini watakaa na hawa ambao sasa hivi wanaigema ile mipira na wanafanyisha kazi watu, watakaa chini kuwalipa mishahara yao tena kwa wakati. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi : Ahsante sana Mhe. Spika, kusema kwamba wafanyakazi hao wametelekezwa na Wizara pengine ya Kilimo sio sahihi kwa sababu ni Wizara ya Fedha ndio iliyokuwa inashughulikia watu hawa wakati huo. Pia Wizara ya Fedha iliwakodisha watu ambao ndio waliohusika na kuwalipa mishahara.

Sasa hivi wizara yangu imo katika mikakati ya kurekebisha hali hiyo kwa kuyahuisha yale mashamba upya ili yaweze kutoa mazao yenye tija. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mjumbe kwamba mashamba haya ya mpira kwa kweli yamegemwa vibaya sana, wamegema maeneo ya karibu na barabara kule ndani hayajawahi kugemwa hata siku moja. Kwa hiyo, bado tuna tana kubwa sana mipira hii inaweza ikatoa mchango katika uchumi wa taifa. Ahsante sana.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa amekiri kwamba mashamba haya hivi sasa hayana uzalishaji na wana mpango wa kupanda mazao mengine. Lakini kutokana na serikali kupitia wizara zake huwa na Mipango Miji naamini kwamba mashamba haya kwa mipango hii tunaweza kuingia humu kwa awamu tatu bila ya kufanyiwa kazi.

Je, wizara yako ina mpango wa kuyafanya mashamba haya kuwapa wananchi na kuyaendeleza katika kipato hichi ili serikali ipate tija. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumjibu kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa mashamba haya yanahitaji utaalamu wa hali ya juu kuwakabidhi wananchi wayaendeleze chini ya usimamizi inawezekana ikawa si tatizo lakini ni tatizo kubwa. Kwa hiyo, mashamba haya tunaona sisi kwanza tuyaendeleze na tuyakabidhi kwenye kampuni ambazo zitakuwa tayari kuekeza na kuyaendeleza mashamba hayo ili tuweze kupata tija zaidi. Ahsante sana.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Spika, pamoja na majibu mwanana kabisa kutoka kwa Mhe. Naibu Waziri napenda kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Mhe. Waziri mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo utakubaliana na mimi kwamba mashamba haya ambayo umeyatamka bayana kwamba hayana mkataba sasa hivi yako *free* yako chini ya serikali kwamba bado yanavunwa mpira mpaka leo

(b) Hawa wanaovuna kwa sababu na mimi ni Mjumbe wa kamati tulikwenda kukaa pamoja na uongozi wa wizara wakakubali kuvuna na kulipa mishahara pamoja na kukabidhiwa mashamba yale kimakosa. Ni lini mtazuia uvunaji ule wa mipira ili fedha zile zifaidike kwenda serikalini kuliko kwenda mikononi mwa watu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza nakubaliana nae kwamba bado mashamba hayo yanavunwa na yanavunwa kinyume cha utaratibu. Lakini bado nasisitiza kwamba mashamba hayo hayajakuwa kwenye dhamana yetu kwa sababu tumepewa barua ya kukabidhiwa kimaandishi, tunataka wakatukabidhi *physical* kule tuone nini kipo nini hakipo wafanyakazi wangapi wapo ili tuweze kuweka rekodi ya mashamba haya vizuri zaidi.

Huyu anaevuna mipira hii anaitwa "Jiwezeshe". Sasa nafikiri kajiwezesha kweli kweli maana kila unapouliza kapewa na nani hupati jibu sahihi. Sasa sisi tunavyopanga sasa hivi tunapanga mipango ya kuendeleza mipira hii kumuondoa kabisa muwekezaji huyu kuorodhesha wafanyakazi waliopo, kuorodhesha mashamba yote yaliopo pamoja na kuchukuwa kama nilivyosema kabla ya jana pale tutachukuwa *inventory register* kwa sababu hii ni mali ya serikali. Kwa hiyo, tukishafanya hivyo tutakaribisha tenda kama ilivyokawaida kuyakodisha mashamba haya ili yaweze kuleta tija kwa serikali yetu. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe huo ndio mwisho wa maswali yetu. Kabla sijamwita Katibu kutaja shughuli yetu inayofuta kuna matangazo kidogo tangazo la mwazo ni tangazo la wageni ambao wametufikia leo hapo ukumbini.

Wageni wa mwanzo ni wageni wa Mhe. Iss Haji Ussi Gavu Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Wageni wenyewe ni kama wafuatavyo:

1. Bwana Omar Mouline - Kutoka Moroco. *Omar Mouline you are most well come to the House of Representatives*
2. Ndg. Juma Mohammed Salum - Naibu Mkurugenzi Habari na Maelezo
3. Ndugu Hassan Diaspora – kutoka Italia ana pacha wake humu Barazani bahati nzuri sana
4. Nd. Ibrahim Mitawi - Mkurugenzi *Show Time Entertainment LTD*
5. Ndg. Ali Makame Issa - Yeye huyu ni Mwanaharakati, wanaharakati wengi sana siku hizi, naomba usimame, hayupo hapo.
6. Ndg. Mbarouk Zahor Salum - kutoka CANADA nafikiri itakuwa katika hiyo Diaspora pia.

7. Ndg. Issa Ali Seif – Kutoka CANADA pia
8. Ndg. Said Nassor Hemed - Kutoka UK
9. Ndg. Mohammed Y. Mohammed - Kutoka UK nae namuona hapo
10. Ndg. Yussuf Said Ali - Kutoka CANADA
11. Ndg. Hafsa Hassan Mbamba - Kutoka Denmark
12. Ndg. Ali Abdirahman Hassan - Kutoka UK
13. Ndg. Dhayya Rashid Abdalla - Kutoka Denmark.

Waheshimiwa Wajumbe wageni wengine ni mgeni wa Mhe. Simai Mohammed Said kutoka Jimbo la Tunguu. Mgeni wenyewe ni mgeni kutoka Hoteli ya LA GEMMA Nungwi anajulikana kwa jina la Mr. Meinrad Schibler, *you are most well come* akiongozana na mkewe wake Madam Irina, *you are most well come to the Zanzibar House of Representatives*. (*Makofi*)

Mr. Meinrad maarufu kama Jimmy anajishughulisha na kutoa taaluma ya uendeshaji wa Hoteli za Kimataifa kwa wazawa wa Zanzibar katika kukabiliana na tatizo ya ajira kwa vijana.

Wageni wa Mhe. Shamata Shaame Khamis huyu ni Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni. Wageni wenyewe Waheshimiwa Madiwani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ambao ni kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Omar Issa Kombo - Mwenyekiti ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni (Diwani wa Wadi ya Sizini). Karibu sana.
2. Mhe. Salma Khamis Tumu - Diwani wa Wadi ya Tumbe
3. Mhe. Bakar Mjaka Faki - Diwani Wadi ya Micheweni
4. Mhe. Hassan Ameir Ali - Diwani Wadi ya Wingwi.

Karibuni Waheshimiwa, karibuni sana kwenye Baraza la Wawakilishi.

Waheshimiwa tangazo jengine ni tangazo la uchangiaji damu. Waheshimiwa Wajumbe tunakumbushwa kwamba ile shughuli yetu ya uchangiaji wa damu iliyokuwa ifanyike Makunduchi sasa itafanyika hapa hapa Chukwani katika viwanja vya Afisi za Baraza la Wawakilishi kesho Jumamosi kuanzia saa 3.00 asubuhi.

Waheshimiwa Wajumbe sote kwa pamoja pamoja na wafanyakazi wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi tunaombwa sana kuhudhuria kwa wingi na kuchangia damu kwa kadiri itakavyowezekana hapo kesho.

Vile vile wananchi wote wanakaribishwa kuhudhuria na kuchangia damu ili kulihami tatizo la upungufu wa damu katika benki yetu hasa katika kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Ahsanteni sana.

Waheshimiwa baada ya hapo nina matangazo mawili tangazo la mwanzo linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ambaye alikuwa anaomba Wajumbe wa kamati yake

wakutane kwa ufupi tu mara baada ya kusikia hili tangazo yaani baada ya kusikia hili tangazo tutakapokuwa tunaendelea na jambo jengine la Bajeti ya Wizara ya Nchi.

Pia Mhe. Hamida Abdalla Issa watakuwa wanajijua hakutaja kamati gani baada ya maswali na majibu nae alikuwa anaomba kukutana na kamati yake. Huo ndio mwisho wa matangazo ambayo tunayo hapa leo. Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 - Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Mhe. Spika: Waheshimiwa naomba sasa nimwete Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili aje awasilishe Bajeti yake, karibu sana Mheshimiwa. Mheshimiwa ni mshabiki mkubwa sana wa Yanga kwa hiyo vielelezo vyake vinaonekana karibu. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma. Lakini Mhe. Spika, naomba muda wako dakika mbili tu.

La kwanza niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe Watanzania, Wazanzibari na wanamichezo wenzangu. Nichukuwe nafasi hii kiipongeza kwa dhati *Simba Sport Club* kwa kupunguza ukame wa vikombe katika Mtaa wa Msimbazi. Hongereni kwa kupata kikombe cha *Vodacom* na niwaahidi *Yanga African* tutakutana mwakani. Nawaomba msije mkatupiga mabuti mengi maana kitabu chetu kina rangi ya Yanga. (*Makofi*)

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba nichukue nafasi kuweza kuwasilisha Makadirio na Mapato ya Bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu, likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili, kuzingatia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Spika, awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, muumba wa mbingu na ardhi kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa katika afya njema na furaha. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kutudumisha katika amani na utulivu nchini petu. Atuzidishie imani thabiti ya kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015- 2020 katika kuwatumikia wananchi wetu kufikia maendeleo tuliokusudia.

Mhe. Spika, naomba kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa umahiri wake wa kuiongoza nchi yetu na kusimamia ipasavyo utekelezaji wa majukumu ya Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufuata Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020 na Mipango Mikuu ya Kitaifa.

Mhe. Spika, tabia ya uwazi na uadilifu ya Mheshimiwa Dk. Shein katika uongozi wake ni miongoni mwa mambo yanayoimarisha uwajibikaji na kuharakisha maendeleo kwa wananchi wa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba siku hadi siku. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie hekima na busara katika kuwatumikia wananchi, ili tuendelee kufaidika na uongozi wake uliotukuka.

Mhe, Spika, nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi, naibu wako Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Wenyeviti wa Baraza lako Tukufu, Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Mheshimiwa Shehe Hamad Mattar kwa kuliongoza vyema Baraza hili. Katika uongozi wako tumeshuhudia uendeshaji wa mijadala iliyo wazi katika nidhamu ya hali ya juu ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako.

Mhe. Spika, shukrani maalum ziende kwa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mwenyekiti; Mheshimiwa Omar Seif Abeid, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Konde. Kamati hii, kwa kipindi chote ambacho tumefanya kazi nayo, imekuwa ikishirikiana nasi pamoja na ushauri ambao imeuwezesha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, kwa kuwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zimefikia ukomo kwa mujibu wa kanuni zetu, nachukua fursa hii, kabla ya kuziunda upya Kamati hizi, kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii kwa uweledi wao waliotuonesha wakati wakifanya kazi nasi. Nawatakia kila la kheri na kuwaahidi kuwa tutakuwa nao pamoja katika kazi zetu na tutaendelea kusikiliza ushauri wao.

Mhe. Spika, sambamba na hilo, naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati nyengine za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zinazofanyakazi kwa karibu na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambazo ni Kamati ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Mohamed Said Mohamed (Dimwa), Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mpendae na Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Hesabu za Mashirika ya Umma (PAC) inayoongozwa na Mheshimiwa Miraji Khamis Mussa (Kwaza), Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chumbuni.

Mhe. Spika, mabadiliko ya tabia nchi yamesababisha kuwa na misimu ya mvua isiyotabirika. Mvua za masika za mwaka huu zilianza vizuri katika wiki ya kwanza kwa kunyesha kwa wastani na hazikuleta athari kubwa kwa wananchi. Hata hivyo, katika wiki ya pili mvua kubwa zilishuhudiwa katika mwambao mzima wa pwani ya Afrika Mashariki ambazo zilileta maafa kwa baadhi ya wananchi wetu. Nawapa pole wale wote walioathirika kwa namna moja au nyengine.

Mhe. Spika, taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini Tanzania imetabiri kuwapo kwa mvua kubwa katika msimu huu wa masika kwenye maeneo yote ya Unguja na Pemba na mwambao mzima wa Afrika Mashariki. Kutokana na utabiri huo, nawaomba wananchi

wachukue tahadhari ya hali ya juu kujiepusha na madhara yanayoweza kusababishwa na mvua hizo. Hata hivyo, ni muhimu pia kuzitumia mvua hizo vizuri kadri inavyowezekana katika kuimarisha shughuli za kilimo.

Mhe. Spika, namalizia utangulizi wangu kwa kutoa shukurani zangu maalum kwa Wananchi wote wa Zanzibar kwa umoja na mshikamano wao na kudumisha amani na utulivu. Aidha, kwa heshima kubwa nawapongeza wananchi kwa kuendelea kuunga mkono Serikali yao inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi katika jitihada zake za kuwaletea maendeleo. Natoa wito kwa wananchi wote tuendelee kutunza amani yetu tukizingatia kwamba pasipo amani na utulivu hukosekana; na panapokosekana utulivu maendeleo hayawezi kupatikana.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba uniruhusu niwasilishe kwa ufupi Utekelezaji wa Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha Julai – Machi 2017/2018.

Utekelezaji Wa Programu Za Ofisi Ya Rais Na Mwenyekiti Wa Baraza La Mapinduzi Kwa Kipindi Cha Julai – Machi 2017/2018

Mhe. Spika,Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilitekeleza Programu kuu tano na ndogo 11 chini ya Mafungu mawili ambayo ni A01 na A02. Programu Kuu hizo ni kama zifuatazo:-

i. Programu ya Kusimamia Huduma na Shughuli za Mhe. Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu;
ii. Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi;
iii. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
iv. Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu; na
v. Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, Utekelezaji wa Programu hizi, ulizingatia Mpango Mkuu ya Kitaifa ikiwemo Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020, MKUZA, pamoja na Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Upatikanaji Wa Fedha

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ilitengewa jumla ya TZS. milioni 8,342.6 kwa mafungu yake mawili. Fungu A01 lilitengewa jumla ya TZS. milioni 6,634.7. Kati ya hizo TZS. milioni 730.0 kwa ajili ya mradi wa maendeleo na TZS. milioni 5,904.7 kwa ajili ya kazi za kawaida. Fungu A02 lilitengewa jumla ya TZS. milioni 1,707.9. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 Fungu A01 liliingiziwa jumla ya TZS. milioni 4,605.0 sawa na asilimia 78 kwa ajili ya matumizi ya

kawaida na TZS. milioni 730.0 sawa na asilimia 100.0 kwa ajili ya mradi wa maendeleo. Aidha, fungu A02 liliingiziwa TZS. milioni 1,263.0 sawa na asilimia 74.0.

Mhe. Spika, kupitia Programu zake, Ofisi ilitekeleza bajeti yake ya 2017/2018 na kuweka vipaumbele katika maeneo yafuatayo:-

i. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Rais, Baraza la Mapinduzi na Kamati zake;
ii. Kusimamia utekelezaji wa kazi za Baraza la Mapinduzi, Kamati zake na Kamati ya Makatibu Wakuu kwa kuzingatia Katiba na Sheria za Nchi;
iii. Kuwahudumia Wananchi kwa kuzitekeleza ahadi za Mhe. Rais pamoja na kuwapatia taarifa za shughuli za Serikali na maendeleo ambayo ni haki yao ya Kikatiba;
iv. Kusimamia utendaji na ufanisi wa kazi katika ORMBLM;
v. Kuendeleza ujenzi na kuimarisha usalama wa nyumba za Ikulu; na
vi. Kusimamia maendeleo ya wafanyakazi wa ORMBLM katika kutekeleza wajibu wao, uendelezaji wa maslahi yao zikiwemo stahiki na haki zao, ili waweze kutoa huduma kwa wananchi ipasavyo.

Mafanikio Ya Programu Za Ofisi Ya Rais Na Mwenyekiti Wa Baraza La Mapinduzi Kwa Kipindi Cha Julai – Machi, 2017/2018

1. Mhe.Spika**,** naomba kulithibitishia Baraza lako Tukufu kwamba Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilitekeleza bajeti yake kwa mafanikio makubwa kupitia Programu zake zote.

Programu ya Kusimamia Huduma na Shughuli za Mhe. Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu hii iliidhinishiwa TZS. milioni 3,664.1 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 iliingiziwa TZS. milioni 2,379.8 sawa na asilimia 81 kwa kazi za kawaida na TZS. milioni 730.0 sawa na asilimia 100 kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, mafanikio makubwa yamepatikana kupitia Programu hii ambapo shughuli za Mhe. Rais zimefanyika vizuri na wananchi wameeleweshwa juu ya shughuli kadhaa za Serikali zikiwemo maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Jarida la Ikulu pamoja na vipindi mbali mbali vya Redio na Televisheni vilitayarishwa na kurushwa hewani. Kadhalika, mitandao ya kijamii na magazeti yalitumika katika kuwapatia taarifa wananchi na watu mbali mbali.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alifanya ziara ya kikazi katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). Ziara hiyo, ilianza tarehe 22 hadi 25 Januari, 2018, kufuatia mualiko wa Mheshimiwa Sheikh Mohammed Bin Zayed Al Nahyan, Mrithi wa Mtawala wa Abu Dhabi na Naibu Amiri Jeshi Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi vya Umoja wa

Falme za Kiarabu. Katika ziara hio, Mhe. Rais alifanya mazungumzo rasmi na mwenyeji wake huyo.

Mhe Spika, Viongozi wengine ambao Mhe. Rais alikutana nao katika ziara hio ni Sheikh Mohammed Bin Rashid Al Makhtoum; Makamu wa Rais na Waziri Mkuu wa UAE na Mtawala wa Dubai, Sheikh Dk. Sultan Mohammed Al Qasimi; Mtawala wa Sharjah pamoja na Sheikh Saud Bin Saqr Al Qasimi; Mtawala wa Ras Al Khaimah. Kadhalika, Mhe. Rais alikutana na Wakuu wa Taasisi mbali mbali wa Falme hizo kutokana na ratiba aliyopangiwa. Kiambatisho Namba 1 kinahusika.

Mhe. Spika, mazungumzo ya Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Viongozi hao yalilenga katika kuendeleza uhusiano na ushirikiano uliopo baina ya Falme za Kiarabu, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Zanzibar. Kadhalika, mazungumzo hayo yalitoa fursa kwa viongozi hao kubadilishana mawazo juu ya mambo ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii ambapo viongozi wa falme za kiarabu UAE wameelezea nia yao ya kuendelea kuiunga mkono Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar katika jitihada zake za kuinua uchumi na kuendeleza huduma za jamii.

Mhe. Spika, wakati akiwa katika ziara hiyo, Mhe. Rais na ujumbe aliofuatana nao walipata fursa ya kutembelea Mji wa Nishati Mbadala uliopo Abu Dhabi (Masdar City) ambao umepiga hatua kubwa katika utafiti na matumizi ya nishati mbadala ya jua. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeandaa utaratibu wa kuwapeleka Wataalamu wake katika mji huo kwa lengo la kujifunza na kupata uzoefu juu ya nishati mbadala, ili utaalamu watakaoupata uweze kutumika Zanzibar. Kadhalika, Mhe. Rais alikutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Abu Dhabi (Abu Dhabi Fund) ambapo Mfuko huo umeonesha nia ya kuendelea kushirikiana na Zanzibar katika mipango yake ya miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, miradi mingine iliyotembelewa ni shamba la kisasa la ufugaji wa ng'ombe wa maziwa liitwalo Al Rawabi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaandaa Maofisa watatu watakaopatiwa mafunzo katika shamba hilo hivi karibuni. Kadhalika, Mhe. Rais, alitembelea Makao Makuu ya RAK GAS; Ras Al Khaimah, na kuelezwa juu ya shughuli mbali mbali zinazofanywa na kampuni hiyo katika utafutaji wa Mafuta na Gesi na hatimae Ras Al Khaimah na Zanzibar zimekubaliana kuendelea kutekeleza Maelewano ya Awali (MOU), yaliyotiwa saini tarehe 12 Novomba, 2011. Vile vile, jitihada za pamoja baina ya Ras Al Khaimah na Zanzibar zitaendelezwa katika kufanya utafiti wa Mafuta na Gesi asilia.

Mhe. Spika, kwa jumla, ziara ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika Umoja wa Falme za Kiarabu, ilifanikiwa sana kuimarisha uhusiano katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika kuimarisha ufuatiliaji wa mambo muhimu yaliyojitokeza kwenye ziara hiyo, Mhe. Rais ameunda Kamati ya Ufuatiliaji ambayo tayari imeanza kazi na kuwasilisha taarifa Serikalini.

Mhe. Spika kwa maelezo zaidi yanayohusiana na ziara hii kuna jarida maalumu ambalo tumeligawa ambalo linaelezea kwa ukamilifu mafanikio yote ya ziara hiyo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Mhe. Rais, alifanya ziara ya ndani katika Mikoa mitano ya Unguja na Pemba Kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mhe. Rais alitembelea Kiwanda cha Sukari Mahonda ambacho kimefungwa mashine mpya hivi karibuni. Kadhalika, alikagua mradi wa uchimbaji wa visima na usambazaji maji safi na salama uliofadhiliwa na Jamhuri ya Watu wa China. Mradi huo umekamilika na kukabidhiwa rasmi Serikalini tarehe 19 Aprili, 2018 ambapo wananchi 101,850 wa Shehia 21 watafaidika.

Mhe. Spika, katika ziara hizo, Mhe. Rais alitembelea kijiji cha Mbuyumaji na Mlilile na kuagiza kujengwa Skuli ya madarasa manne, Kituo cha Afya na barabara. Aidha, aliagiza kupeleka huduma za umeme katika vijiji hivyo. Maagizo hayo yametekelezwa ambapo ujenzi wa madarasa manne ya Skuli katika kijiji cha Mbuyumaji umekamilika na ujenzi wa kituo cha afya unaendelea. Vile vile, mradi wa maji na umeme umetekelezwa kwa hatua kubwa. Katika kijiji cha Mlilile huduma za maji sasa zinapatikana na barabara imetengenezwa.

Mhe. Spika, ziara za Mhe. Rais ziliendelea katika Mkoa wa Kusini Unguja, kwa kutembelea Mradi wa Maji Mitakawani. Mradi huo umeshakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi tangu tarehe 28 Oktoba, 2017. Vijiji vinavyofaidika na huduma za maji za mradi huo ni Mitakawani, Tunduni, Uzini na Bambi ya Bondeni. Vile vile, katika ziara hio, Mhe. Rais, aliagiza umeme ufikishwe katika pango la Mnywambiji, agizo ambalo limeshatekelezwa. Hivi sasa, wananchi wa Makunduchi na Kibuteni wanafaidika na huduma ya maji yanayotoka katika pango hilo.

Mhe. Spika, katika juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuinua Michezo, Mhe. Rais alikagua kiwanja cha Michezo Kitogani ambacho ujenzi wake umepiga hatua kubwa na kuwataka wahusika wafanye juhudi ya kuukamilisha. Vile vile, Mhe. Rais alikagua nyumba za madaktari Kajengwa Makunduchi na Muyuni. Mhe. Rais aliahidi kuiezeka pamoja na kuitia milango na madirisha nyumba ya madaktari ya Kajengwa. Ahadi ya Mhe. Rais ya kuiezeka nyumba hiyo ameshaitekeleza.

Mhe. Spika, kwa upande wa Pemba, Mhe. Rais alifanya ziara ambapo alifungua madarasa na maabara katika Skuli ya Chokocho na kuagiza vifaa vya maabara katika Skuli hio vipelekwe. Vifaa hivyo pamoja na meza na viti tayari vimeshapelekwa. Kwa upande wa kilimo, Mhe. Rais alikagua mashamba ya mikarafuu na kutembelea kambi za karafuu na kushiriki katika uchumaji. Mhe. Rais aliagiza juhudi zichukuliwe kuyagundua mashamba yote ya Serikali yaliyofichwa. Idadi ya mashamba yaliyogunduliwa yamefikia 9982.

Mhe. Spika, katika kusheherekea Maadhimisho ya miaka 54 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Mhe. Rais alifungua jengo la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na kuhimiza umuhimu wa ukusanyaji, utumiaji na uhifadhi wa takwimu sahihi kwa ajili ya maendeleo. Aidha, mnamo tarehe 6 Januari, 2018, Mhe. Rais alishiriki katika tukio la

kihistoria la kuzindua mradi wa umeme katika Kisiwa cha Fundo, Wete, Pemba. Hatua hio, ilikuwa ni miongoni mwa utekelezaji wa ahadi alizozitoa Mhe. Rais wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, katika kuhakisha kwamba wananchi wanapata habari na taarifa za Serikali na nyenginezo kwa uhakika, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alizifungua Studio mpya za kisasa za Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) tarehe 9 Januari, 2018. Ufunguzi wa Studio hizo, umeiwezesha Televisheni ya Zanzibar, kurejesha hadhi yake ya asili kwa kuwa na mitambo bora na watangazaji mahiri.

Mhe. Spika, siku hio hio, Mhe. Rais alifungua Soko la Kinyasini, Mkoa wa Kaskazini Unguja na kutoa wito kwa wakulima, wavuvi, wafugaji na wananchi wote kwa jumla kulitumia vyema Soko hilo. Shughuli nyengine alizozifanya Mhe. Rais katika maadhimisho ya Sherehe za miaka 54 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ni ufunguzi wa barabara ya Jendele-Unguja Ukuu Kaebona, Wilaya ya Kati Unguja ambayo imerahisisha usafiri kwa wananchi wa maeneo hayo na kuwawezesha kusafirisha mazao na bidhaa zao mbali mbali.

Mhe. Spika, kama ilivyo kawaida, tarehe 12 Januari, 2018 Mhe. Rais alijumuika na Wananchi wa Zanzibar na viongozi mbali mbali katika Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 54 ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Kiwanja cha Amaan. Kupitia hotuba yake aliyoitoa alielezea mafanikio yaliyopatikana katika sekta zote muhimu za kiuchumi, kijamii na kisiasa katika mwaka 2017. Alielezea juhudi, mwelekeo wa uchumi, uendelezaji wa miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na bandari na mchango wake katika kuendeleza sekta nyengine, ikiwemo biashara na utalii.

Mhe. Spika, katika hotuba hio, Mhe. Rais alifahamisha mafanikio yaliyopatikana katika kuendeleza sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Aliwataka wananchi kuwa imara katika kulinda hali ya amani na utulivu iliyopo ambayo ndio msingi wa mafanikio yetu. Aidha, alielezea mipango na juhudi za Serikali katika kuimarisha na kuulinda Muungano wa Tanganyika na Zanzibar wa 1964 uliopelekea kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, alibainisha juhudi na mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuendeleza ushirikiano na mataifa mbali mbali pamoja na mashirika ya Kimataifa.

Mhe. Spika, katika kuukaribisha mwezi mtukufu wa Ramadhani 2017, Mhe. Rais alitoa risala maalum ya kuwataka wananchi kuwa na nyoyo za upendo na huruma baina yao na wageni. Alihimiza utamaduni wa kuvumiliana baina ya waumini wa dini mbali mbali katika mwezi wa Ramadhani. Kadhalika, aliwahimiza wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa za chakula kutoka nje ya nchi kuwapa unafuu wa bei wananchi hasa ikizingatiwa kwamba Serikali imetoa punguzo la ushuru wa bidhaa hizo. Aidha, aliwahimiza wafanyabiashara wote kuwa waadilifu katika kuendesha shughuli zao na kujiepusha na tamaa za kupandisha bei ya bidhaa bila ya kuzingatia sheria.

Mhe Spika, katika hotuba aliyoitoa kwenye Baraza la Idd-el-Fitri mwaka 2017, Mhe. Rais alitoa pongezi maalum kwa Waislamu kwa kukamilisha Ibada ya Funga ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kuwataka wananchi wote kwa ujumla kuishi kwa mapenzi na kuvumiliana. Alitoa pongezi maalum kwa Taasisi zote za Serikali na Binafsi kwa kutoa huduma nzuri kwa wananchi katika kipindi chote cha mwezi mtukufu wa Ramadhani. Vile vile, katika hotuba hiyo, Mhe. Rais alisisitiza haja ya kuimarisha uwajibikaji na uadilifu katika kutekeleza majukumu yetu.

Mhe Spika, katika kuukaribisha mwaka mpya wa 2018, Mhe. Rais aliendelea na utamuduni wake wa kuhutubia wananchi kupitia vyombo vya habari. Katika risala yake, alielezea matukio makubwa na muhimu yaliyopita katika mwaka 2017 ambayo yalikuwa na umuhimu maalum kwa maendeleo na historia ya nchi yetu. Kupitia Risala hio, Mhe. Rais alitoa salamu maalum za upendo kwa wanafamilia wa wanajeshi 14 wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliofariki nchini Congo (DRC).

Mhe. Spika, shughuli nyengine ambazo Mhe. Rais alizifanya katika mwaka wa fedha 2017/2018 ni kuufungua Mkutano wa 17 wa Baraza la Mawaziri la Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika na Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu tarehe 8 Septemba, 2017, Unguja. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kuweka mikakati na kuongeza maarifa ya kupambana na mbinu zinazotumiwa katika kutakatisha fedha haramu.

Mhe. Spika, katika hatua nyengine, Mhe. Rais alizindua Maonesho ya Kilimo Kizimbani yaliyofanyika tarehe 10 Oktoba, 2017 na kuhimiza umuhimu wa utumiaji wa mbinu za kisasa katika kuendeleza Kilimo, Ufugaji na Uvuvi. Vile vile, Mhe. Rais alihudhuria katika Kongamano la Kiswahili lililoandaliwa na Baraza la Kiswahili la Zanzibar tarehe 21 Disemba, 2017 ambapo alisisitiza juu ya kuendeleza lugha ya Kiswahili katika ngazi ya Kimataifa pamoja na matumizi ya Kiswahili fasaha.

Mhe. Spika, akiendelea na shughuli zake, Mhe. Rais alifungua mkutano mkuu wa Chama cha Walimu Zanzibar, tarehe 10 Februari, 2018. Mhe. Rais aliwasihi walimu kupanua wigo wa shughuli zao kwa kulipatia ufumbuzi tatizo la wanafunzi la kuanguka katika mitihani yao na kuutaka uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwa karibu zaidi na walimu. Aidha, aliwahimiza walimu kuwa imara katika kutekeleza maagizo ya serikali ya kutoa elimu bure kuanzia ngazi ya msingi hadi sekondari.

Mhe. Spika, miongoni mwa shughuli nyengine alizozifanya Mhe. Rais ni kushiriki katika Maadhimisho ya Siku ya Sheria Zanzibar, tarehe 12 Februari, 2018. Katika wadhifa wake wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*), Mhe. Rais alitunuku Stashahada, Shahada, Shahada za Uzamili na Shahada za Uzamivu kwa wahitimu wa Chuo hicho tarehe 13 Febuari, 2018. Aidha, Mhe. Rais alizindua ukumbi mpya wa Chuo hicho uliopewa jina la Dk. Ali Mohamed Shein, uliopo Tunguu Wilaya ya Kati Unguja.

Mhe. Spika, kama ilivyo kawaida, tarehe 01 Mei, 2018, Mhe. Rais, alishiriki katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, Wete, Pemba. Katika maadhimisho hayo,

Mhe. Rais alisisitiza juu ya suala la uwajibikaji, kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali za umma pamoja na kuwataka wafanyakazi waongeze juhudi katika kazi. Vile vile, aliwataka Waajiri na Chama Cha Wafanyakazi kushirikiana na serikali katika kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika sehemu za kazi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha, 2017/2018, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alikutana na viongozi wa nchi mbali mbali, wakuu wa Taasisi za Kimataifa na Mabalozi. Tarehe 8 Agosti, 2017, Mhe. Rais alikutana na Rais wa Mauritius wa wakati huo, Mhe. Ameenah Gurib Fakim. Mazungumzo ya viongozi hao yalikwenda vizuri ambapo masuala ya kushirikiana yalitiliwa mkazo. Vile vile, Mhe. Rais alikutana na Bibi Patricia Janet Scotland, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, Ikulu Unguja ambapo kiongozi huyo alimthibitishia Mhe. Rais kwamba Jumuiya ya Madola inaunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Mhe. Spika, wageni wengine aliokutana nao ni Mkurugenzi Mtendaji wa *UNAIDS* ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Bwana Michel Sidibe. Kiongozi huyo aliahidi kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika juhudi zake za kupambana na maradhi ya UKIMWI. Mhe. Rais alionana na Mheshimiwa Abdel Fatah El Sisi Rais wa Misri, tarehe 14 Agosti, 2017, mjini Dar es Salaam ikiwa ni moja katika hatua muhimu ya kuimarisha uhusiano kati ya Misri, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar kwa jumla.

Mhe. Spika, katika kipindi hicho, Mhe. Rais, vile vile alikutana na Dk. Jose Graziana da Silva, Mkurugenzi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa. Kadhalika, alikutana na Mhe. Dk. Mohamed Bin Hamed Al Rumi, Waziri wa Mafuta na Gesi wa Oman na ujumbe wa *UNICEF* ulioongozwa na Bwana Renevan Deugen. Katika mazungumzo yake na viongozi hao, Mhe. Rais amesisitiza umuhimu wa kuendeleza na kutekeleza diplomasia ya kiuchumi pamoja na kuimarisha viwanda na uwekezaji nchini. Orodha kamili ya wageni aliokutana nao Mhe. Rais ipo katika Kiambatisho Namba 2.

Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba wananchi wameendelea kupata taarifa za utekelezaji wa shughuli za Mhe. Rais kwa wakati na usahihi. Urahisi wa kupatikana habari kwa haraka umetokana na kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (*ICT*). Hali hii imeshuhudiwa katika ziara za Mhe. Rais katika Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (*UAE*) ambapo habari zimeweza kuwafikia wananchi kwa haraka na katika hali ya ubora.

Mhe. Spika, matoleo manne ya Jarida la Ikulu na toleo moja maalum yamechapishwa ambayo yameelezea kwa kina utekelezaji wa shughuli za maendeleo mjini na vijijini. Jumla ya Kalenda 6,300 zimechapishwa zikielezea matukio ya shughuli za Mhe. Rais. Katika kipindi hiki jumla ya vipindi 15 vya redio na vipindi 6 maalum vya televisheni vimetayarishwa na kurushwa kupitia *ZBC* vikielezea utekelezaji wa ahadi za Mhe. Rais na maoni ya wananchi kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kiambatisho Namba 3 kinatoa ufafanuzi.

Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. milioni 508.1 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 iliingiziwa TZS. milioni 386.6 sawa na asilimia 76 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, utekelezaji wa programu hii umeiwezesha Zanzibar kuimarisha ushiriki wenye tija katika Jumuiya za Mtangamano wa Kikanda za *SADC*, *EAC*, *IORA* na Jumuiya ya Utatu (*EAC-SADC-COMESA*). Aidha, mahusiano mazuri yameimarika zaidi baina ya serikali na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi yaani Diaspora. Serikali imeendeleza dhamira yake ya kuwashajiisha Wanadiaspora kushiriki katika kuiletea Zanzibar maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia Kongamano la Nne la Wanadiaspora.

Mhe. Spika, Mkutano wa Kilele wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulifanyika jijini Kampala, Uganda tarehe 23 Februari, 2018. Mkutano huo ulijadili mambo mbali mbali ya maendeleo ikiwemo maendeleo ya miundombinu na kuanzisha Taasisi ya Fedha na Taasisi nyengine kwa ajili ya utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Fedha ifikapo 2024. Ajenda nyengine zilizozungumzwa ni pamoja na kuharakisha utaratibu wa nchi ya Sudan ya Kusini kushiriki kikamilifu katika shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kushajiisha maendeleo ya viwanda vya kutengeneza gari, ili kuifanya Jumuiya kuwa na ushindani katika sekta ya viwanda hivyo.

Mhe. Spika, mikutano mingine ya wataalamu ilifanyika katika miji ya Dodoma, Dar es Salaam, Nairobi na Kampala ambayo kwa ujumla wake iliratibu utekelezaji wa kusimamia uondoshwaji wa vikwazo vya biashara visivyokuwa vya kiushuru na mapendekezo ya mapitio ya viwango vya pamoja vya ushuru wa forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Tamasha la Sanaa na Utamaduni lilifanyika Kampala, Uganda mwezi Septemba, 2017. Maonesho ya Biashara ya Jua kali/Nguvu kazi yalifanyika mwezi Disemba, 2017 Bujumbura, Burundi yakiwa na lengo la kutengeneza mazingira mazuri ya kibiashara na kutafuta fursa za masoko kwa bidhaa za wajasiriamali na zinazozalishwa katika ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa mwezi Agosti, 2017 mjini Pretoria, Afrika Kusini kulifanyika Mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*). Miongoni mwa Ajenda zilizojadiliwa ni pamoja na kuridhiwa kwa Jamhuri ya Umoja wa Visiwa vya Comoro kuwa mwanachama mpya wa *SADC* na kuifanya Jumuiya hiyo kuwa na nchi Wanachama 16. Aidha, Mkutano wa Kilele uliagiza kukamilisha kazi ya tathmini ya maombi ya uwanachama ya Burundi na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa *SADC*.

Mhe. Spika, kufuatia maazimio ya Mkutano wa Kilele, Baraza la Mawaziri wa nchi za *SADC* ilikutana mwezi Machi, 2018 mjini Pretoria. Katika mkutano huo, miongoni mwa mambo yaliojadiliwa ni pamoja na utekelezaji wa maazimio ya Mkutano wa Kilele ikiwemo kuimarisha maendeleo ya viwanda na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje

ya Nchi za *SADC*. Aidha, mkutano huo umezungumzia ajenda ya kuweka mfumo shirikishi utakaowezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya nchi wanachama.

Mhe. Spika, mambo mengine yaliyojadiliwa katika mkutano huo ni kuongeza kasi ya kukamilisha maandalizi ya uanzishwaji wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha *SADC* ambacho kinalenga kuweka msisitizo katika maeneo ya Mafunzo ya Taaluma za Ufundi na Kazi za Amali, "*Technical – Vocational Educational Training*" na kinatarajiwa kutoa nafasi za '*Scholarship'* zipatazo 300 kwa nchi zote za *SADC*. Chuo hicho kitakuwa na Makao Makuu yake Nchi ya Ufalme wa eSwatini (*Swaziland*).

Mhe. Spika, Mkutano wa Saba wa Makatibu Wakuu wa Jumuiya ya Nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi ulifanyika Mjini Bali, Indonesia tarehe 2 Agosti, 2017. Mkutano huo ulilenga kufanya ufuatiliaji wa maazimio ya Mkutano wa kwanza wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika Mjini Jakarta Indonesia mwezi Machi, 2017 ambapo Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alimuwakilisha Rais wa Jamuhuri wa Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Aidha, mkutano huo ulipokea mapendekezo ya wagombea waliojitokeza kugombea nafasi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo ambao ni kutoka Afrika Kusini, Kenya na Comoro.

Mhe. Spika, kupitia mkutano huo Jumuiya ya *IORA* ilikubali ombi la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kuipa fedha kutoka katika mfuko wake maalum kwa ajili ya kufanya warsha ya Maendeleo ya Mikakati ya Kikanda ya uendelezaji maliasili ya uvuvi katika eneo la Bahari ya Hindi. Warsha hiyo ilifanyika Zanzibar mwezi Oktoba, 2017 na ilihudhuriwa na nchi wanachama 10 pamoja na Kamisheni ya Samaki wa Jodari ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Tuna Commission*). Madhumuni ya warsha hiyo ni kuweka Mkakati wa pamoja kwa nchi wanachama ya kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali ya uvuvi wa Bahari ya Hindi ili kuimarisha akiba ya chakula, ajira, uchumi na kukomesha uvuvi haramu. Mgeni rasmi katika warsha hiyo alikuwa Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa niaba ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Mhe. Spika, katika eneo la Ushirikiano wa Kimataifa, Zanzibar imeshiriki katika Mkutano wa Tatu wa Kamisheni ya Kudumu ya Mashirikiano baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kiarabu ya Misri uliofanyika tarehe 08 hadi tarehe 10 Januari, 2018 (*Tanzania – Egypt Joint Permanent Commission*) Cairo, Misri. Ujumbe wa Zanzibar katika Mkutano huo uliongozwa na Mheshimiwa Issa Haji Ussi Gavu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Makubaliano mbali mbali yalifikiwa ambayo yatakuwa na tija kwa Zanzibar katika Sekta za Elimu, Afya, Usafiri wa Baharini, Michezo na Kilimo cha Umwagiliaji.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, mahusiano baina ya Zanzibar na Jamhuri ya Umoja wa Visiwa vya Comoro yameendelea kuimarika zaidi. Ujumbe maalum wa Mawaziri wa Zanzibar ulifanya ziara ya kikazi nchini humo mwezi Julai, 2017 na Aprili, 2018. Ziara hizo zilikuwa na lengo la kufuatilia Mkataba wa makubaliano ambao ulisainiwa na Marais wa nchi mbili hizi mwaka 2014. Kamati ya pamoja ya utekelezaji wa

Makubaliano imeundwa yenye wajumbe wanne, wawili kutoka kila upande. Kamati hiyo inatarajia kuanza kazi ya kufuatilia utekelezaji wa makubaliano kabla ya mwezi Juni, 2018. Mashirikiano katika nchi mbili hizi yanahusisha usafiri wa baharini, biashara, kilimo, utalii, elimu na utamaduni.

Mhe. Spika, ujumbe wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ulifanya ziara ya kikazi nchini Morocco kuanzia tarehe 05 Agosti hadi 12 Agosti, 2017 kwa ajili ya kukuza mashirikiano kati ya nchi hizi mbili. Ujumbe huo uliongozwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Issa Haji Ussi Gavu. Katika ziara hiyo, masuala mbali mbali ya maendeleo yalijadiliwa yakiwemo mashirikiano ya kibiashara na Benki ya Attijariwafa yenye Makao Makuu yake Mjini Casablanca.

Mhe. Spika, Benki hiyo imeonesha nia ya kuwekeza katika eneo la Afrika ya Mashariki na kuitumia Zanzibar kama mlango wake wa kupitia. Benki ya Attijariwafa itatoa fursa kubwa katika kukuza uchumi ikiwemo utoaji wa mikopo yenye riba ndogo. Wakati huo huo, Taasisi inayoshughulikia Biashara na Uwekezaji ya Morocco ilikusudia kufanya ziara Zanzibar mwishoni mwa mwaka 2017 pamoja na Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Morocco wakiwemo wa Sekta ya Utalii, ili kuangalia fursa za kibiashara na uwekezaji zilizopo Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa upande wa ushirikishwaji wa Diaspora kwa maendeleo ya Zanzibar, ujumbe wa Madaktari kutoka Maryland, Marekani kupitia Jumuiya ya Wanadiaspora wa Tanzania wanaoishi Maryland (*Head Inc*) ulifika Zanzibar kwa ajili ya kutoa huduma za Afya kuanzia tarehe 30 Juni hadi 10 Julai, 2017. Ujumbe huo ulijumuisha Madaktari, Wafamasia na Wauguzi. Madaktari hao walitoa huduma kwa kushirikiana na Madaktari na Wauguzi wenyeji katika vituo vinne ambavyo ni Hospitali ya Mnazi Mmoja, Vituo vya afya vya Chwaka, Matemwe na Bumbwini. Huduma walizozitoa ni pamoja na tiba ya maradhi ya ngozi, shindikizo la damu, kisukari na magonjwa ya macho na kuwapatia wagonjwa miwani. Vile vile, walitoa ushauri kuhusiana na saratani kwa wanawake. Aidha, ujumbe huo ulikabidhi dawa na vifaa tiba vya aina mbali mbali vyenye thamani ya US$ 459,075.04 kwa Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, katika kuonesha matokeo ya kushajiisha Wanadiaspora katika kuchangia Maendeleo, Wazanzibari wanaoishi nchini Denmark kupitia Jumuiya yao ya AHAS GROUP wameunga mkono juhudi za serikali za kuimarisha sekta ya elimu na afya kwa kutoa msaada wa vifaa tiba na vifaa vya elimu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na Skuli ya Jang'ombe msingi "B" vyenye thamani ya US$ 26,000.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zimefanya Kongamano la Nne la kitaifa la Watanzania wanaoishi nje ya nchi (*4th Tanzania Diaspora Conference*) tarehe 23 hadi 24 Agosti, 2017, hapa Zanzibar. Lengo kuu la kongamano hilo ni kuwashajiisha Wanadiaspora kuwekeza nchini kwao kwa maslahi yao na kwa ustawi wa uchumi wa Tanzania. Kongamano hilo lilihudhuriwa na Wanadiaspora 154 kutoka Mataifa mbali mbali duniani. Dhamira ya Kongamano hilo ilikuwa ni "Uzalendo kwa Maendeleo" na kauli mbiu isemayo "MTU KWAO, NDIO NGAO". Aidha, Wanadiaspora katika Kongamano

hilo walitakiwa kuwa wazalendo kwa nchi yao ya asili na kuwekeza katika sekta mbali mbali za kiuchumi na kijamii na kuitangaza Zanzibar na Tanzania kwa ujumla katika nchi wanazoishi, ili kuwavutia zaidi wawekezaji na watalii.

Mhe. Spika, Jumuiya ya Wanadiaspora wa Marekani *DICOTA* waliandaa Jukwaa la Afya tarehe 11 Novemba, 2017 mjini Maryland, Marekani. Jukwaa hilo lilihudhuriwa na Wataalamu mbali mbali wa afya wanaoishi Marekani. Mmoja wa watoa mada katika jukwaa hilo alikuwa Balozi Arikana Chihombori - Quao Balozi wa Umoja wa Afrika katika Umoja wa Mataifa. Mada zilizozungumzwa katika Jukwaa hilo ni pamoja na vifo vya wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano kwa nchi za Afrika na uzoefu wa utoaji huduma za afya zinazotolewa na Diaspora nchini Tanzania. Ujumbe wa Zanzibar katika jukwaa hilo uliongozwa na Mhe. Harusi Said Suleiman, Naibu Waziri wa Afya.

Mhe. Spika, ujumbe huo ulipata fursa ya kufanya mazungumzo na Wanadiaspora katika Sekta ya Afya pamoja na kutembelea miji ya *Virginia* na *Seattle* nchini Marekani. Aidha, ujumbe huo ulipata fursa ya kukutana na Viongozi wa Jumuiya ya Wazanzibari wanaoishi Marekani (*ZADIA*) na kuona vifaa Tiba mbali mbali ambavyo vinasafirishwa katika nchi zinazoendelea hususan nchi za Afrika.

Mhe. Spika, Jumuiya ya Watanzania wanaoishi Dallas, Marekani waliandaa Kongamano la siku ya Mtanzania mjini Dallas kuanzia tarehe 27 hadi 29 Aprili, 2018. Kongamano hilo lilienda sambamba na maadhimisho ya kusherehekea miaka 54 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Lengo la Kongamano hilo lilikuwa ni kuonesha utamaduni na historia ya Tanzania na maliasili ilizojaaliwa nazo ambazo zitawezesha wawekezaji na wafanyabiashara wa Marekani kuja kuwekeza na kutalii. Kongamano hilo lilipata bahati ya kuhudhuriwa na kufungwa na Mhe. Zubeir Ali Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi.

Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. milioni 2,462.2 kwa matumizi ya kazi za kawaida, na hadi kufikia mwezi Machi, 2018 iliingiziwa TZS. milioni 1,838.6 sawa na asilimia 74 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, mafanikio yaliyopatikana kupitia Programu hii ni pamoja na kuwepo kwa Mpango wa miaka mitano wa Rasilimali Watu na Mpango wa miaka mitatu wa Urithishwaji watumishi; Kuimarika kwa usalama wa serikali kupitia ukaguzi wa Wafanyakazi na Majengo; na kuanza kwa Utafiti juu ya fursa zinazopatikana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai – Machi, 2018 Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imewajengea uwezo wafanyakazi 18 katika mafunzo ya muda mrefu kwenye fani za sayansi ya jamii, usimamizi na ukarimu, ununuzi na ugavi, usimamizi wa rasilimaliwatu, takwimu na siasa ya jamii katika ngazi za Cheti,

Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamivu. Aidha, wafanyakazi 25 wameongezewa ujuzi katika mafunzo ya muda mfupi ya usimamizi na ukarimu yaliyoendeshwa na wakufunzi kutoka Chuo cha "*National Research Institute of Food and Fermentation Industries*" cha Jamuhuri ya Watu wa China.

Mhe. Spika, kupitia programu hii, wafanyakazi 80 wamepewa mafunzo ya kujikinga na maradhi yasiyoambukiza pamoja na kupima afya zao. Mafunzo hayo yaliendeshwa na wataalamu kutoka Wizara ya Afya. Sambamba na hayo, wafanyakazi 86 wamelipwa stahiki zao za likizo na 16 wamelipwa malipo baada ya saa za kazi (Kiambatisho Namba 4 na 5 vinatoa ufafanuzi juu ya Mafunzo na Likizo).

Mhe. Spika, utafiti mdogo wa kutathmini mahitaji ya mafunzo ya wafanyakazi umefanyika. Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huo wafanyakazi watapatiwa mafunzo kwa mujibu wa mahitaji yao na bajeti iliyopangwa. Aidha, taarifa za wafanyakazi katika "*Database*" ya maendeleo ya rasilimaliwatu zimepitiwa na baadhi yake kufanyiwa marekebisho kwa kuzingatia vielelezo vilivyowasilishwa na wafanyakazi hao.

Mhe. Spika, Kamati ya Uongozi na Kamati Tendaji ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zimekutana kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na Serikali. Wajumbe wa vikao hivyo walipata nafasi ya kujadili na kutathmini utekelezaji wa majukumu na mienendo ya wafanyakazi. Aidha, vikao vinne vya Bodi ya Zabuni vimefanyika ambavyo vimejadili ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa mujibu wa Sheria. Vile vile, Kamati ya Ukaguzi wa Ndani imefanya vikao vyake vitatu kwa ajili ya kupitia utaratibu wa matumizi na kumshauri Katibu Mkuu njia bora za kuimarisha usimamizi wa matumizi.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanza kazi ya kufanya mapitio ya Sheria ya Mambo ya Rais namba 5 ya mwaka 1993 na Sheria ya Usalama wa Taifa na Siri za Serikali namba 5 ya mwaka 1983. Baada ya mapitio hayo, mapendekezo ya marekebisho yatapelekwa Serikalini kabla ya kuletwa hapa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kupitishwa.

Mhe. Spika, zoezi la utafiti juu ya fursa zinazopatikana katika mtangamano wa Afrika Mashariki na namna Zanzibar itakavyonufaika nazo unaendeshwa kwa pamoja kati ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Kazi ya kukusanya na kuchambua taarifa za utafiti huo zimekamilika. Hatua itakayofuata ni kuwasilisha rasimu ya awali ya ripoti ya utafiti huo kwa wahusika, kazi hiyo inategemewa kufanyika mwezi Mei, 2018. Aidha, kazi ya kukusanya taarifa za utafiti wa mahitaji ya kujifunza na kufundisha lugha ya Kiswahili katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaendelea. Kukamilika kwa tafiti hizi mbili kutasaidia kuweka bayana fursa zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na mikakati ya Zanzibar kuweza kunufaika nazo.

Mhe. Spika, kupitia progamu hii, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kushirikiana na Tume ya Mipango na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali zinaendelea

kukamilisha utafiti juu ya mchango wa Wanadiaspora kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Zanzibar. Kazi ya kukusanya na kuchambua takwimu imekamilika na ripoti ya awali itatolewa mwezi Juni, 2018. Utafiti huu ni moja kati ya agenda zilizoainishwa ndani ya Tafiti za Kitaifa za Zanzibar.

Mhe. Spika, utafiti mdogo juu ya upatikanaji wa takwimu katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi umekamilika. Matokeo ya utafiti huu yamewezesha Maofisa Mipango wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Unguja na Pemba kupata mafunzo juu ya kukusanya na kuchambua takwimu. Mfumo wa ukusanyaji takwimu umeandaliwa ambao utawawezesha Maofisa Mipango kuzitumia takwimu hizo katika kazi zao za kila siku.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba imesimamia utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa ufanisi ikiwemo kuhudumia na kuziweka salama nyumba za Ikulu zilizopo Pemba. Vile vile, kupitia programu hii, taarifa nne za tathmini za kijamii zimetayarishwa zinazoelezea matatizo mbali mbali ya wananchi vijijini. Aidha, vikao saba vya Maofisa Wadhamini Pemba vimefanyika na kuzungumzia utunzaji na usimamizi wa rasilimali fedha, mkakati wa watumishi wa umma kutojiunga na vyuo visivyo rasmi na uingiaji na utokaji kazini kwa watumishi wa umma. Kwa upande mwengine Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeanza kuweka msingi wa ujenzi wa Ofisi yake mpya ya Chake Chake, Pemba.

Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kuwa wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2,285 wamefanyiwa upekuzi wa awali na endelevu na Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO) (Kiambatisho Namba 6). Aidha, umefanyika ukaguzi wa kiusalama katika majengo manane ya Serikali yaliyopo Unguja, Pemba na Tanzania Bara. Majengo hayo ni Wakala wa Uchapaji wa Serikali, Masjala ya Idara ya Uvuvi, Masjala ya Wizara ya Afya, Ikulu Ndogo Bwefum, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) Unguja na Pemba, Kamisheni ya Ardhi na Shirika la Bima la Zanzibar Kanda ya Mbeya. Katika ukaguzi huo Taasisi zilishauriwa juu ya kuimarisha usalama katika maeneo ya kufanyia kazi.

Mhe. Spika, mafunzo juu ya utunzaji na udhibiti wa siri za Serikali yamefanyika kwa wafanyakazi wa ORMBLM, Dar es Salaam na Dodoma, Masheha wa Mikoa mitano ya Zanzibar, Makatibu Muhtasi wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Maofisa na Watendaji wa Bodi ya Mapato Zanzibar, Unguja na Pemba. Jumla ya washiriki 525 walinufaika na mafunzo hayo (Kiambatisho namba 7) kinatoa ufafanuzi.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri kumradhi kidogo, Waheshimiwa Wajumbe naona kuna bahasha zinazunguka humu ndani naomba ziende kimya kimya, zisitumike humu ndani. Tuendelee Mhe. Waziri sijui zina nini maana yake Spika sina habari.

Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu hii iliidhinishiwa TZS. milioni 394.0 kwa matumizi ya kawaida, na hadi kufikia mwezi Machi, 2018 iliingiziwa TZS. milioni 231.5 sawa na asilimia 59 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, kupitia Programu hii, mafanikio makubwa yamepatikana ikiwemo kufanikisha vikao vya kawaida na dharura vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake pamoja na Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu ambapo pamoja na mambo mengine, nyaraka mbalimbali zikiwemo za Sheria na Sera zilijadiliwa na kutolewa maamuzi.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki vikao 20 vya BLM vimefanyika ambapo jumla ya nyaraka 84 zikiwemo tisa za Sheria na tatu za Sera zilijadiliwa na kutolewa maamuzi. Aidha, Kamati ya Makatibu Wakuu imefanya vikao 28 ambavyo vimejadili nyaraka 37 zikiwemo sita za Sheria na tatu za Sera na kuzitolea maoni ya kitaalamu na hatimae kuziwasilisha Baraza la Mapinduzi. Kiambatisho Namba 8 kinatoa ufafanuzi.

Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameendelea na utaratibu wake wa kawaida wa kukutana na Viongozi wa Wizara na Mashirika kwa lengo la kupima utendaji wa Serikali kwa wananchi. Katika kipindi hiki, vikao 15 vilifanyika vikiwahusisha Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji Waandamizi wa Serikali. Aidha, vikao hivyo viliangalia utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Mpango kazi, upatikanaji wa fedha na uwajibikaji.

Mhe. Spika, katika kuimarisha Utawala Bora, Viongozi na Watumishi wa Umma wamepatiwa mafunzo ya kujenga uwezo wa kuelewa dhana na misingi ya Utawala Bora wenye kuzingatia Haki na Sheria. Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliongoza kongamano hilo la kuwajengea uwezo viongozi wa kisiasa na kiutendaji wa Serikali kuhusu Utawala Bora na Uchumi.

Mhe. Spika, Kongamano hilo lililobeba kauli mbiu isemayo **“**Utawala Bora ni Msingi wa Uchumi Imara”, lilifanyika tarehe 15 Machi, 2018. Pamoja na mambo mengine, Kongamano hilo lilijadili mada zinazohusu Mgongano wa Maslahi katika Utumishi wa Umma, Mafanikio ya Utelekezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA III) kwa lengo la kufahamu kwa kina mwenendo wa uchumi wetu katika kufikia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya Mwaka 2020 (*Zanzibar Development Vision 2020).*

Mhe. Spika, kupitia programu hii, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi Mipango, Sera na Utafiti na Watendaji wengine wa ngazi za juu wamepewa mafunzo kuhusu mbinu na umahiri katika kufanya majadiliano ya kufikia mapatano *(Negotiation skills).* Mafunzo hayo, yametolewa na Taasisi ya UONGOZI ya Dar es Salaam. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukuza uelewa wa watendaji wa ngazi za juu wa Serikali katika masula yanayohusu kufanya majadiliano ya kufikia mapatano katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa yanayolenga kulinda maslahi ya Zanzibar ikiwemo uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika Programu hii, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekiimarisha Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kilichoanzishwa chini ya Ofisi ya Baraza la Mapinduzi. Muundo na majukumu yake yamekamilika pamoja na kuajiri watumishi wenye weledi kwa ajili ya kufanya kazi za Ufuatiliaji na Tathmini. Ni matarajio yetu kuwa, utekelezaji wa Sera, Sheria na Miongozo na Maamuzi yanayotolewa na Serikali utaendelea kuimarika na kuwa wenye ufanisi na tija zaidi.

Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu hii iliidhinishiwa TZS. Milioni 1,313.9 kwa matumizi ya kawaida, na hadi kufikia mwezi Machi, 2018 iliingiziwa TZS. milioni 1,031.5 sawa na asilimia 79 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, mafanikio yaliyofikiwa kutokana na utekelezaji wa Programu hii ni pamoja na kuimarika kwa mazingira na mfumo wa uendashaji wa kazi za kuwajengea uwezo wafanyakazi, kuimarisha mawasiliano na kuimarisha Maktaba ya kumbukumbu na Nyaraka za Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, uwezo wa wafanyakazi umeendelea kuimarika na wenye kuleta ufanisi zaidi kutokana na kuendelea programu za kujenga uwezo wao kitaaluma kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kulingana na mahitaji na mabadiliko ya wakati. Wafanyakazi wanne wameendelea kupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za shahada fani ya Sayansi ya Habari na shahada ya uzamili za Umma na Sayansi Kompyuta. Wafanyakazi wengine sita wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani za Itifaki, Usimamizi wa Fedha, Udereva wa Viongozi Mashuhuri sambamba na kuwapatia wafanyakazi taaluma ya namna ya kujikinga na maradhi yanayoambukiza ikiwemo UKIMWI na yasiyoambukiza.

Mhe. Spika, kupitia programu hii, Mtambo mpya wa mtandao wa mawasiliano ya Serikali *(E-Government)* umeunganishwa ili kurahisisha mawasiliano pamoja na kuweka mashine za kutunzia na kutengenezea nyaraka katika Maktaba ya Baraza la Mapinduzi.

MWELEKEO WA BAJETI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeandaa bajeti yake ya mwaka wa fedha 2018/2019 kwa mujibu wa muongozo wa utayarishaji wa bajeti ya Serikali na kuendelea kuwa na Programu Kuu 5 na Programu Ndogo 11.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeongezeka kwa TZS. milioni 1,830.1 sawa na asilimia 60 ya ongezeko la Matumizi Mengineyo. Kutoka TZS. milioni 3,000.6 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 hadi TZS. milioni 4,830.7 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa matumizi ya kawaida. Kwa mradi wa maendeleo, ongezeko ni TZS. milioni 270.0 sawa na asilimia 36. Kutoka TZS. milioni 730.0 mwaka wa fedha 2017/2018 hadi TZS. milioni 1,000 mwaka wa

fedha 2018/2019. Ongezeko hili ni kutokana kuengezeka kwa mahitaji katika Ofisi Ya Rais Na Mwenyekiti Wa Baraza La Mapinduzi.

Mhe. Spika, katika Fungu A01 fedha za nyongeza zimeongezeka katika ununuzi wa mashine ya ukaguzi Ikulu, bajeti ya Washauri wa Mhe. Rais, kuzitangaza shughuli za Mhe. Rais karibu zaidi na wananchi hasa maeneo ya vijijini, kuimarisha shughuli za upekuzi wa wafanyakazi na ukaguzi wa majengo na miundo mbinu ya Serikali. Aidha, kuimarisha mazingira katika nyumba za Ikulu ya Dodoma na Chake Chake, Pemba. Katika Fungu A02 fedha za nyongeza zimeelekezwa katika kufanikisha shughuli za Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 imejipangia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuratibu shughuli na huduma za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
ii. Kusimamia majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake;
iii. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za Wizara, Idara na Taasisi za Serikali pamoja na maamuzi ya Serikali;
iv. Kuelimisha jamii na Viongozi juu ya Sera ya Diaspora ya Zanzibar;
v. Kuwajengea uwezo Viongozi na Watendaji kupitia semina za mafunzo, ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi;
vi. Kuwawezesha wananchi kupata taarifa juu ya utekelezaji wa shughuli za Serikali yao;
vii. Kuwawezesha watendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushiriki katika mtangamano wa Jumuiya za Kikanda yenye kuleta tija kwa Zanzibar;
viii. Kuwashajiisha Wanadiaspora kuchangia katika maendeleo ya Zanzibar;
ix. Kuimarisha upatikanaji wa takwimu katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
x. Kuimarisha mazingira na usalama katika nyumba za Ikulu, Unguja, Pemba, Dar es Salaam na Dodoma;
xi. Kuimarisha usalama kwa watumishi wa Serikali na maeneo wanayofanyia kazi; na
xii. Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuipatia Ofisi vitendeakazi kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

PROGRAMU KUBWA NA NDOGO NA MAKISIO YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mhe. Spika, Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zinatekelezwa na Ofisi na Idara zifuatazo:-

i. Ofisi ya Faragha ya Rais;
ii. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi;

iii. Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu;
iv. Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi;
v. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
vi. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
vii. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi –Pemba; na
viii. Ofisi ya Usalama wa Serikali yaani GSO.

Mhe. Spika, Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Fungu A01 ni kama zifuatazo:-

Programu ya Kusimamia Huduma na Shughuli za Mhe. Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu

Mhe. Spika, lengo kuu la Programu hii ni kusimamia huduma na Shughuli za Mhe. Rais na kuimarisha mawasiliano baina ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na wananchi wake. Aidha, kuendeleza Taswira nzuri ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni Umma na Wananchi wote kwa jumla kuwa na uelewa kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Mhe. Rais. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Kusimamia Huduma na Shughuli za Mhe. Rais; na
ii. Programu Ndogo ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi.

Mhe. Spika, aidha, Programu hii itatekelezwa sambamba na Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu.

Mhe. Spika, katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kutekeleza maagizo na maelekezo yanayotokana na shughuli za Mhe. Rais;
ii. Kupanga na kutekeleza mahitaji ya Mhe. Rais kwa ajili ya kutekeleza kazi zake;
iii. Kutoa huduma za uendeshaji na utawala katika Ofisi ya Faragha ya Mhe. Rais;
iv. Kuimarisha huduma kwa kuzipatia vifaa, zana na bidhaa nyumba za Ikulu zilizopo Unguja, Pemba, Dar – es - Salaam na Dodoma;
v. Kuifanyia matengenezo nyumba ya Ikulu ya Mnazi Mmoja na Ikulu ndogo zilizopo Dar – es - Salaam, Unguja, Dodoma na Pemba;
vi. Kutoa huduma za uendeshaji na utawala katika Ofisi za Washauri wa Mhe. Rais; na
vii. Kukuza mawasiliano baina ya Ikulu, Wananchi na Wadau wa habari.

Mhe. Spika, ili Programu ya Kusimamia Huduma na Shughuli za Mhe. Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 5,445.5. Kati ya hizo TZS. milioni 4,445.5 kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS. milioni 1,000 kwa kazi za maendeleo.

Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi

Mhe. Spika, lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha mashirikiano na Jumuiya za Kikanda, Kimataifa na Kuwashirikisha ipasavyo Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi katika maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii ya Zanzibar. Aidha, matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni Zanzibar kufaidika na fursa za Kiuchumi na Kijamii zinazotokana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kikanda na Kimataifa; na
ii. Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi yaani kuratibu shughuli za Diaspora.

Mhe. Spika, katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kushiriki katika Mikutano ya Kikanda ndani na nje ya nchi;
ii. Kuendeleza Ushirikiano wa Kimataifa;
iii. Kujenga uelewa kwa jamii juu ya Sera ya Diaspora Zanzibar na utekelezaji wake;
iv. Kuandaa Kongamano la Watanzania wanaoishi nje ya nchi yaani Kongamano la Diaspora.
v. Kujenga uelewa juu ya fursa zinazopatikana kutokana na Jumuiya za mtengamano wa Kikanda (*EAC, SADC, IORA, TRIPATITE* na *AU*); na
vi. Kushiriki katika mikutano ya ndani na kimataifa inayohusiana na Diaspora.

Mhe. Spika, ili Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 610.7 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na MBLM

Mhe. Spika, malengo makuu ya Programu hii ni kuimarisha uwezo wa kiutendaji na kuratibu shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Kuimarisha Shughuli za Mipango, Kuandaa na Kuchambua Sera na Kufanya Utafiti; Kuimarisha Shughuli za Upekuzi kwa Watumishi kabla na baada ya Kuajiriwa na Kuimarisha Usalama wa Majengo na Miundombinu ya Serikali. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika kwa mazingira ya utendaji kazi. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo nne zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Pemba; na
iv. Programu Ndogo ya Kusimamia Usalama wa Watumishi wa Umma.

Mhe. Spika, katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kulipa mishahara kwa wafanyakazi na stahiki zao;
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi;
iii. Kuandaa vikao vya Kamati zilizomo ndani ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa sheria;
iv. Kutoa huduma za uendeshaji na Utawala katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
v. Kufanya ukaguzi wa hesabu za awali na endelevu na Vikao vya Kamati ya ukaguzi;
vi. Kuandaa Sera ya Mawasiliano ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na mpango mkakati wake;
vii. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
viii. Kufanya utafiti juu ya ushiriki na tija kwa Zanzibar katika mikutano ya Kikanda na Kimataifa kutoka 2015/16 - 2017/18;
ix. Kukusanya takwimu na kutathmini utekelezaji wa ripoti ya mahitaji ya takwimu ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
x. Kutoa huduma za uendeshaji na Utawala katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba;
xi. Kufanya upekuzi wa awali wa kiusalama na endelevu kwa wafanyakazi;
xii. Kufanya ukaguzi wa kiusalama katika majengo na miundombinu ya Serikali; na
xiii. Kutoa mafunzo kwa watumishi juu ya utunzaji wa siri na maadili ya kazi.

Mhe. Spika, ili Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 2,136.8 kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.

Mhe. Spika, Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Fungu A02 ni hizi zifuatazo:-

Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba Na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi Na Kamati ya Makatibu Wakuu

Mhe. Spika, lengo la Programu hii ni kuhakikisha uwajibikaji wa Serikali katika Kutoa huduma kwa Wananchi. Aidha, kuhakikisha malengo ya Wizara na Taasisi za Serikali yanatekelezwa ipasavyo na kufikiwa. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika

Sera, Sheria na Miongozo yenye kusaidia ukuaji wa uchumi, maendeleo na kudumisha amani na umoja Nchini. Program hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia shughuli za Baraza la Mapinduzi na Kamati zake; na
ii. Programu Ndogo ya Tathmini ya Utendaji kazi na Uwajibikaji wa Taasisi za Umma.

Mhe. Spika, katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kutayarisha vikao vya kawaida vya BLM na Kamati ya Makatibu Wakuu na kufuatilia utelekezaji wa maamuzi yake;
ii. Kutayarisha vikao Maalum vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yake;
iii. Kusimamia Programu za mafunzo ya kujenga uwezo kwa Watendaji wa Serikali na Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi;
iv. Kuandaa vikao vya kuhimiza uwajibikaji wa Watumishi wa Umma kati ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi (KBLM/KMK) na Watendaji Wakuu wa Wizara na Taasisi za SMZ;
v. Kuimarisha taswira na hali ya Utumishi wa Umma Nchini;
vi Kuimarisha Uhusiano na Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya na Majukwaa ya Kikanda na Kimataifa
vii. Kuratibu kazi na ziara za Waheshimiwa Mawaziri wasio na Wizara maalum
viii Kutayarisha mikutano kati ya Mhe. Rais na Wizara za SMZ, ili kutathmini utekelezaji wa Mipango kazi na kufuatilia utekelezaji wa maagizo na maelekezo yanayotolewa;
ix. Kujenga uwezo wa kiutendaji kwa watumishi wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini
x. Kufuatilia utekelezaji wa masuala maalum yanayohusu Sera, Sheria na Maamuzi ya Serikali.

Mhe. Spika, ili Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu iweze kutekelezwa kikamilifu, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 509.8 kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.

Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi

Mhe. Spika, lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha mazingira ya kazi, mahusiano ya umma na kuongeza ujuzi wa wafanyakazi. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuwa na mfumo bora na wa kisasa wa kuendesha shughuli za Ofisi ya Baraza la Mapinduzi na Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo moja ifuatayo:-

i. Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuimarisha miundombinu ya majengo pamoja na mazingira yake;
ii. Kuimarisha huduma za mawasiliano na utekelezaji wa kazi za kila siku;
iii. Kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi;
iv. Kutoa taaluma ya afya kuhusu maradhi yasiyoambukiza na kujikinga na UKIMWI;
v. Kuimarisha huduma za Maktaba na Kitengo cha Uandaaji, Usambazaji na Uhifadhi wa Kumbukumbu za BLM; na
vi. Kuwalipa wafanyakazi mishahara na stahiki zao.

Mhe. Spika, ili Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iweze kutekelezwa kikamilifu, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 1,451.8 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO

Mhe. Spika, labda niseme maelezo kidogo tu kwamba katika kitabu chetu kuna makosa kidodo ya uandishi wa tarakimu za namba kwamba haziko sahihi. Kwa hivyo naomba zile ambazo zitazisema mimi ndio sahihi.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2018/2019, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inakadiria kutumia jumla ya TZS. milioni 10,433.7 kwa ajili ya Matumizi ya utekelezaji wa Programu za Fungu A01 na A02.

Fungu A01 linakadiriwa kutumia TZS. milioni 8,472.1 kwa kazi za kawaida na mradi wa maendeleo. Kati ya fedha hizo, TZS. milioni 7,472.1 kwa ajili ya kazi za kawaida na TZS. milioni 1,000.0 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maendeleo. Fungu A02 linakadiriwa kutumia TZS. milioni 1,961.6 kwa kazi za kawaida (Kiambatisho Namba 9).

MAOMBI YA FEDHA 2018/2019

Mhe. Spika, ili kuiwezesha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zenye jumla ya TZS. milioni 10,433.7 Kati ya fedha hizo, TZS. milioni 9,437.7 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TZS. milioni 1,000.0 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo.

MWISHO

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa

kuendelea kuniamini mimi Mhe. Issa Haji Ussi kwa kunipa dhamana ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vile vile, nampongeza Mhe. Rais kwa juhudi anazozifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar na kuhakikisha kuwa wanaendelea kuishi kwa amani na utulivu. Nakuombeni Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tuendelee kumuunga mkono Rais wetu katika jitihada zake hizo.

Mhe. Spika, kabla sijamaliza hotuba yangu hii naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo letu la Chwaka kwa kuendelea kuniamini na kwa mashirikiano wanayonipa. Naomba niwathibitishie kwamba tutaendelea kufanyakazi na kutimiza ahadi zangu kadri Mola atakavyonijaalia. Nawaomba waendelee kunipa ushirikiano, ili tuijenge kwa pamoja Chwaka njema tuitakayo.

Mhe. Spika, nawashukuru tena kwa dhati Watendaji wote wa ORMBLM kwa kuanzia na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Mhe. Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu Mkuu ORMBLM, Bwana Salum Maulid Salum Kibanzi, Naibu Katibu Mkuu ORMBLM Bi Rahma Ali Khamis, Katibu wa Rais na Naibu Katibu wa Rais kwa utendaji wao mzuri wa kazi ambao unarahisisha kazi za Uwaziri na kusimamia Wizara. Aidha, nawashukuru kwa namna ya kipekee Waheshimiwa Washauri wa Rais katika kufanikisha kazi za Ofisi hii.

Mhe. Spika, nakushukuru tena wewe binafsi na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano yenu makubwa mnayoendelea kuipatia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wote. Ni dhahiri kwamba mafanikio ya utekelezaji wa majukumu na malengo ya Ofisi hii yamewezekana kutokana na ushirikiano wenu. Aidha, nakushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini wakati wote nikiwasilisha hotuba hii. Ni matumaini yangu kuwa mtatoa ushauri na michango mizuri itakayosaidia utekelezaji wa majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na kuipitisha Bajeti hii pamoja na kutupatia ushauri na maelekezo ambayo yataimarisha utekelezaji wake.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

KIAMBATISHO 1: RATIBA YA ZIARA YA RAIS UAE

DATE	EVENT	REMARKS
Saturday 20/1/2018	Arrival at Dubai International Airport b EK 726 From Dar es Salaam.	
	Depart Dubai International Airport (Majli for Abu Dhabi	Jumeirah at Etihad Towers Hote
	Arrival at Abu Dhabi Jumeirah at Etiha Towers Hotel.	
	ABU DHABI	

DATE	EVENT	REMARKS
Sunday 21/01/2018	**Private Program**	
Monday 22/01/2018	Visit Masdarcity at south east of Ab Dhabi.	Visitythe model city which reli on renewable energy sources
	Visit Sheikh Zayed Grand Mosque.	The largest mosque in the Unite Arab Emirates
	Arrival and Luncheonat the Hotel	Jumeirah at Etihad Towers Hote
	Depart for Courtesy call on His Highne Sheikh Mohammed Bin Zayed Al Nahyan	Majlis at Kasr Al Bahar
	Courtesy call on His Highness Shaik Mohammed Bin Zayed Al Nahyan, Crow Prince of Abu Dhabi and Deputy Supren Commander of the UAE Armed Forces	To enhance bilateral relations ar economic cooperation
	Arrival at the Hotel	Jumeirah at Etihad Towers Hote
	Courtesy call on H.E. Mohamed Saif A Suwaid, Director General, Abu Dhabi Fur for Development	At the Presidential Suit Jumeirah at Etihad Towers Hote
		To discuss Road Proje construction of 20 Km road, fro Fumba - Airport - Zanzib Town.
Tuesday 23/01/2018	Depart Abu Dhabi For Dubai	
Tuesday 23/01/2018	**DUBAI**	
	Visit Jebel Ali Port and Free Zone Dubai.	Deep port and thelargest ma made harbour.
		The world's ninth busiest po and the biggest as well as th busiest port in the Middle-East
	Meeting with UAE Business Community.	At DubaiChamber of Commer Headquarters.

DATE	EVENT	REMARKS
		To attract investors in tourism and investment.
		Presentation by Executive Director of ZIPA
	Courtesy call on His Highness Sheikh Mohammed Bin Rashid Al Maktoum, Vice President, Prime Minister and Ruler of Dubai.	Palace Majlis
	Arrival at the Hotel,	Dubai Palace Downtown Hotel
	VisitNakheelNew CityDevelopment and Palm Jumeirah Project.	
	Luncheon at NakheelNew CityDevelopment and Palm Jumeirah	
	Arrival at the Hotel, Dubai.	Palace Downtown Hotel
Wednesday 24/01/2018	Depart from Dubai Palace Downtown Hotelfor Sharjah.	Visit
	Courtesy call on His Highness Sheikh Sultan bin Mohammed Al Qasimi, Supreme Council Member and Ruler of Sharjah.	To continue cooperation in the sector of education with Zanzibar State University.
		Cooperation and development in the health sector pharmaceutical industry and hospital equipment
	Arrival at SharjahEast Fish Processing LLC	Situated at the border of the Emirates of Sharjah and Ajman
	Visit East Fish Processing Company.	
	Depart from Sharjah East Fishing Processing LLC to for Dubai	Palace Downtown Hotel
	Arrival at Palace Downtown Hotel in Dubai	
	Depart Palace Downtown Hotelfor Al Rawabi Dairy Farm in Sharjah	
	VisitAl Rawabi Dairy Farm and Luncheonat the Farm	
	Depart Al Rawabi Dairy Farm in Sharjah for Ras Al Khaimah.	
	Arrival atRas Al Khaimah.	Waldorf Astoria Hotel

DATE	EVENT	REMARKS
Thursday 25/01/2018	**RAS AL KHAIMAH**	
	Visit Land reclamation Project at Al Marjan Island	
	Courtesy call on His Highness Shaikh Saud Bin Saqr Al Qasimi, Supreme Council Member and Ruler of Ras Al Khaimah.	Cooperation on Oil and Gas exploration.
		Follow up on implementation of MoU between Zanzibar and Ras Al Khaimah.
	Official Luncheon hosted by His Highness Sheikh Saud bin Saqr Al Qasimi, Supreme Council Member and Ruler of Ras Al Khaimah.	Palace Majlis
Friday 26/01/2018	Visit Rak Gas Headquarters	
	Depart Ras Al Khaimah for Dubai Grand Hyatt Hotel.	Grand Hyatt
	Arrives Dubai Grand Hyatt Hotel and luncheon at the Hotel followed by private programme	Grand Hyatt
Saturday 27/01/2018	**DUBAI**	
	Depart Grand Hyatt for Dubai International Airport.	
	Flight EK 725 takes off for Dar es Salaam.	

KIAMBATISHO 2: ORODHA YA WAGENI WALIOFIKA IKULU NA KUONANA NA MHE. RAIS KUANZIA AGOSTI 2017 HADI APRILI, 2018

TAREHE	JINA LA MGENI	CHEO
AGOSTI, 2017		
03.08. 2017	Dk. Leopold Zekeng	Mkurugenzi Mwakilishi wa UNAIDS Nchini Tanzania
04.08.2017	Axel Knospe	Mwakilishi wa Kampuni ya SHELL Nchini Tanzania
10.08.2017	Bwana Xu Xinpei	Meneja wa China "Harbour Engineering Company Ltd".
11.08.2017	Bibi Patricia Boroness Scotland	Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola

TAREHE	JINA LA MGENI	CHEO
	Mheshimiwa Dk. Asha – Rose Migiro	Balozi wa Tanzania nchini Uingereza
14.08.2017	Mheshimiwa Abdel Fattah Al-Sisi	Rais wa Misri (alikutana nae DSM)
28.08.2017	Mheshimiwa Ameenah Gurib Fakim	Rais wa Jamhuri ya Mauritius
28.08.2017	Prof. Kenneth I. Simala	Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki
SEPTEMBA, 2017		
04.09.2017	Mheshimiwa Dk. Lu Youqing	Balozi wa Jamhuri ya Watu wa China nchini Tanzania
06.09.2017	Bwana Kommer Damen	Mwenyekiti wa Kampuni ya "Damen Shipyards" ya Uholanzi
07.09.2017	Dk. Jose Graziano da Silva	Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO)
20.09.2017	Bwana Stephen B. Kargo	Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Maendeleo ya Viwanda (UNIDO)
OKTOBA, 2017		
12.10.2017	Prof. Stener Kvinnsland	Afisa Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukeland Nchini Norway
13.10.2017	Bwana Michel Sidibe	Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la UNAIDS na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.
13.10.2017	Mheshimiwa Dk. Mohammed bin Hemed Al Ruhmi	Waziri wa Mafuta na Gesi wa Oman
	Dk. Salem bin Nasser Al Ismaily	Kiongozi wa Taasisi ya Uwekezaji wa Oman
	Bibi Matha Al Mahrooqiya	Mshauri wa Waziri wa Utalii wa Oman
	Dk. Ahmed Hamoud Al Habsy	Balozi Mdogo wa Oman, aliyepo Zanzibar
16.10.2017	Mheshimiwa Mohammed Mansour Al Malik	Balozi wa Saudi Arabia nchini Tanzania
17.10.2017	Bwana Stephen B. Kargbo	Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Viwanda (UNIDO)
	Mheshimiwa Richard Mabonero	Balozi wa Uganda nchini Tanzania

TAREHE	JINA LA MGENI	CHEO
31.10.207	Bwana Renevan Dengen	Watendaji wa UNICEF
	Bibi Francessca Morandi	
	Bwana Shone Keenan	
	Bwana Masoud Salim	
NOVEMBA, 2017		
09.11.2017	Bibi Jacqueline Mahon	Mwakilishi wa Shirika la UNFPA nchini Tanzania
09.11.2017	Bibi Tully Esther Mwambapa	Mkurugenzi Masoko wa Benki ya CDRB
	Bwana Godwin Sumunyu	Mkurugenzi Mahusiano wa Benki ya CRDB
	Bwana Eusebio Mabofu	Meneja wa Benki ya CRDB, Tawi la Zanzibar
14.11. 2017	Mheshimiwa Dk. G. Viswananthan	Mkuu wa Chuo Kikuu cha VIT nchini India
24.11.2017	Mheshimiwa Rotland Pardede	Balozi wa Indonesia nchini Tanzania
	Mheshimiwa Ali Abdalla Al-Mahruqi	Balozi wa Omani nchini Tanzania
27.11.2017	Mheshimiwa Wang Ke	Balozi wa China nchini Tanzania
	Mheshimiwa Abdulrahman Kaniki	Balozi wa Tanzania nchini Zambia
	Mheshimiwa Meja Jenerali Issa Suleiman Nassor	Balozi wa Tanzania nchini Misri
27.11.2017	Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma	Jaji Mkuu wa Tanzania
JANUARI, 2018		
16.01.2018	Bwana Kamal Attaya	Afisa Mtendaji Mkuu wa Kamupuni ya RAK Gesi
	Bibi Anayaty Tahir	Mshauri wa Mambo ya Sheria
FEBRUARI, 2018		
05.02.2018	Mheshimiwa Rotland Pardede	Balozi wa Indonesia nchini Tanzania
26.02.2018	Mheshimiwa Muhidin Ally Mbweto	Balozi wa Tanzania nchini Nigeria
	Mheshimiwa Wilroad Peter Slaa	Balozi wa Tanzania nchini Sweeden
27.02.2018	Mheshimiwa Sahabi Isa Gada	Balozi wa Nigeria nchini Tanzania
28.02.2018	Mheshimiwa Jaji Mstaafu Semistcles Kaijage	Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) akifuatana na

TAREHE	JINA LA MGENI	CHEO
		ujumbe wake.
MACHI, 2018		
06.03.2018	Mheshimiwa Mohammed Fakih Al-Baadawy	Balozi wa visiwa vya Comoro nchini Tanzania.
08.03.2018	Bwana Zhang Peng	Makamu wa Rais Muwandamizi wa Kampuni ya ZTE
	Bwana Yi Yahua	Makamu wa Rais wa Kampuni ya ZTE
09.03.2018	Bwana Li Yong	Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Viwanda (UNIDO)
27.03.2018	Mheshimiwa Ali Davutaglu	Balozi wa Uturuki nchini Tanzania
27.03.2018	Bwana Gao Mengdon	Meneja Uendeshaji wa Kampuni ya HUAWEI
	Bwana Omar Zeng	Mkurugenzi wa Kampuni ya HUAWEI Zanzibar
	Bwana Gavan Zhao	Meneja Mahusiano wa Kampuni ya HUAWEI
APRILI, 2018		
03.04.2018	Prof. Mark Mwandosya	Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere pamoja na Wajumbe wa Bodi
05.04.2018	Bwana Han Guangshu	Mkurugenzi wa "Nanjing Drum Tower Hospital" ya nchini China.
06.04.2018	Mheshimiwa IGP Mstaafu Ernest Jumbe Mangu	Balozi wa Tanzania Nchini Rwanda
	Mheshimiwa Meja Jenerali Mstaafu Simon Marco Mumwi	Balozi wa Tanzania Nchini Urusi
09.04.2018	Bwana Zhou Junxue	Mwenyekiti wa Kampuni ya "Kunshan Asia Aroma Coperation Limited"
	Bwana Fu Chun Jiang	Mkurugenzi wa kampuni ya "Kun Kunshan Asia Aroma Cooperation limited" nchini China.
	Bwana Mr. Yang Ming	Mkurugenzi Biashara ya Kimataifa wa China
17.04.2018	Bwana Jecha Salim Jecha	Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) akifuatana na Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

TAREHE	JINA LA MGENI	CHEO
19.04.2018	Bwana Mohamed Elabbady	Makamu wa Rais wa Shirika la Ndege la Misri (Egyptair) aliyepo nchini Misri.
28.04.2018	Bwana Jean Boustany	Mwakilishi wa Kundi la Makampuni ya “Privinvest and Advanced Marine Transport (ATM)”, kutoka Dubai.

KIAMBATISHO 3: VIPINDI VILIVYORUSHWA HEWANI NA IDARA YA MAWASILIANO NA HABARI IKULU-ZANZIBAR 2017-2018

Vipindi vya radio

NAM.	JINA LA KIPINDI	KITUO CHA KURUSHIA VIPINDI - REDIO	TAREHE YA KURUSHWA HEWANI
1.	Utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu – Mahojiano na Mkurugenzi wa Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu		2/8/2017
2.	Sehemu ya kwanza - Uzinduzi wa Tawi jipya la CRDB Chake Chake, Pemba		13/09/2017
3.	Maoni ya Wananchi kuhusu Ujenzi wa Barabara Ya Jendele-Cheju-Kaebona	ZBC-REDIO	27/09/2017
4.	Maendeleo ya Skuli ya Sekondari ya Moh'd Juma Pindua	"	25/10/2017
5.	Maoni ya Wananchi kuhusu Ujenzi wa Soko Jipya la Samaki na Mboga - Tibirinzi	"	8/11/2017
6.	Utekelezaji wa Ahadi za Dk. Shein - ufikishwaji wa Nishati ya Umeme Kisiwa cha Fundo	"	22/11/2017
7.	Kipindi maalum - mahojiano na Uongozi wa Zawa kuhusu Utekelezaji wa Ilani ya Uchanguzi Sekta ya Maji	"	13/12/2017
8.	Maoni ya Wananchi wa Mlilile na Banda Maji - Juu ya Ziara ya Dk na Hatua za Utekelezaji wa Maagizo yake	BADO KWENDA HEWANI	27/12/2017
9.	Maoni ya Wazee wa Vitongoji na Wawi - Miaka 54 ya Mapinduzi ya Zanzibar	"	10/1/2018
10.	Jumuiya ya Wazee na Wanadiaspora	"	24/1/2018
11.	Maendeleo Kijiji cha Ngomeni	"	7/2/2018
12.	Utekelezaji wa Ahadi za Dk. Shein - Shehia ya Matemwe Kusini-Mbuyu Maji	"	14/02/2018
13.	Uzinduzi wa Umeme Kisiwa cha Fundo	"	14/03/2018
14.	Maendeleo ya Kituo cha Afya cha Michenzani	"	28/03/2018
15.	Mwaka mmoja na nusu Hospitali ya Abadalla Mzee	"	18/4/2018

Vipindi vya Televisheni

NAM.	JINA LA KIPINDI	KITUO CHA KURUSHIA VIPINDI - TV	TAREHE YA KURUSHWA HEWANI
1.	Kipindi maalumu - Mahojiano na Mkurugenzi wa ZURA	ZBC-TV	5/10/2017
2.	Mahojiano na Uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar - ZAWA	"	12/10/2017
3.	Utekelezaji wa ahadi za Dk. Shein - ufikishwaji wa Nishati ya umeme Kisiwa cha Fundo	"	19/10/2017
4.	Utekelezaji wa ahadi za Dk. Shein - ufikishwaji wa Nishati ya umeme na vyombo vya usafiri Kisiwa Panza - Chokocho	"	2/11/2017
5.	Maendeleo ya Skuli ya Sekondari ya Moh'd Juma Pindua	"	23/11/2017
6.	Ziara ya Dk. Shein Falme za Kiarabu	"	15/02/2018

KIAMBATISHO 4: WAFANYAKAZI WALIOPATIWA MAFUNZO KWA MWAKA 2017/2018

Mafunzo ya muda mrefu

NAM.	NGAZI YA ELIMU	FANI	IDADI YA WAFANYAKAZI		JUMLA
			M'MKE	M'ME	
1.	Shahada ya Uzamivu	Lugha ya Kiswahili		1	1
		Sayansi ya Siasa		1	1
		Sheria za Kimataifa	1		1
2.	Shahada ya Uzamili	Uchumi		1	1
		Usimamizi wa Maktaba	1		1
3.	Shahada ya Kwanza	Mawasiliano	1		1
		Takwimu	1		1
		Ustawi wa Jamii	1		1
		Maendeleo	1		1
		Teknolojia na Biashara		1	1
		Uongozi wa Biashara		1	1
		Sheria	1		1
		Uongozi wa Rasilimali Watu	1		1
4.	Stashahada	Usimamizi wa Utalii na Ukarimu	1	1	2
		Manunuzi na Ugavi		1	1
		Uongozi wa Rasilimali Watu	1		1
5.	Astashahada	Upishi	1		1
	Jumla ndogo		**11**	**7**	**18**

MAFUNZO YA MUDA MFUPI

NAM.	NGAZI YA ELIMU	FANI	IDADI YA WAFANYAKAZI		JUMLA
			M'MKE	M'ME	
1.	Mafunzo mafupi	Maendeleo ya Utalii	1		1
2.	Mafunzo mafupi	Vijana na Jumuiya ya Afrika Mashariki	50	50	100
3.	Mafunzo mafupi	Usimamizi Wa Utalii na Ukarimu	1	3	3
4.	Mafunzo mafupi	Maradhi yasioambukiza	40	40	80
5.	Mafunzo Mafupi	Maradhi ya Ukimwi	40	40	80
6.	Mafunzo mafupi	Usimamizi wa Utalii na Uchumi	15	10	25
7.	Mafunzo mafupi	Mafunzo ya Kuzima Moto na Uokozi	35	41	76
	Jumla ndogo		182	183	365
	Jumla Kuu		**158**	**149**	**383**

KIAMBATISHO 5: IDADI YA WATUMISHI WALIOKWENDA LIKIZO

NAM.	JINA LA IDARA/TAASISI	UNGUJA		PEMBA		JUMLA KUU
		M'ME	M'MKE	M'ME	M'MKE	
1.	Ofisi ya Faragha ya Rais	23	21			44
2.	Baraza la Mapinduzi	4	9			13
3.	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	0	0			0
4.	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	5	5			10
5.	Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje	0	2			2
6.	Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu	2	0			2
7.	Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba		0	8	7	15
	JUMLA KUU	**34**	**37**	**8**	**7**	**86**

KIAMBATISHO 6: ORODHA YA TAASISI ZILIZOFANYIWA UPEKUZI

NAM.	WIZARA/TAASISI	IDADI
1.	Wizara ya Afya	518
2.	Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii	32
3.	Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale	46
4.	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ	60
5.	Wakala wa Serikali wa Uchapaji	09
6.	Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA)	13
7.	Shirika la Umeme (ZECO)	45
8.	Wizara ya Fedha na Mipango	122
9.	Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati	36
10.	Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)	22
11.	Mahakama Kuu Zanzibar	28
12.	Mamlaka ya Mafunzo ya Amali	14
13.	Wakala wa Maabara na Mkemia Mkuu	35
14.	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	1,010
15.	Shirika la Bima la Zanzibar	26
16.	Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji	65
17.	Wizara ya Biashara na Viwanda	14
18.	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege	06
19.	Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia	20
20.	Shirika la Viwango (ZBS)	11
21.	Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wazee, Wanawake na Watoto	10
22.	Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi	04
23.	Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	04
24.	Wakala wa Utafiti wa Mifugo	03
25.	Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	02
26.	Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)	20
27.	Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC)	09
28.	Baraza la Wawakilishi	02
29.	Shirika la Meli na Uwakala	03
30.	Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali	95
31.	Tume ya Mipango Zanzibar	01
	JUMLA	**2,285**

KIAMBATISHO 7: IDADI YA WATUMISHI WALIOPEWA MAFUNZO YA UDHIBITI NA UTUNZAJI SIRI NA TAASISI WANAZOTOKA

NAM.	TAASISI	IDADI
1.	OFISI YA RAIS NA MBLM DAR ES SALAAM NA DODOMA	17
2.	MAKATIBU MUHTASI WA WIZARA ZA SMZ	24
3.	MASHEHA MKOA WA MJINI MAGHARIBI	112

4.	MASHEHA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA	68
5.	MASHEHA MKOA WA KUSINI UNGUJA	61
6.	MASHEHA MKOA WA KASKAZINI PEMBA	55
7.	MASHEHA MKOA WA KUSINI PEMBA	53
8.	BODI YA MAPATO ZANZIBAR	135
	JUMLA	**525**

KIAMBATISHO 8: ORODHA YA NYARAKA ZA SERA NA SHERIA ZILIZOJADILIWA NA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2017/2018

NAM.	SERA/SHERIA
1.	Mswada wa Kufuta Sheria ya Uchaguzi Nambari 11 ya Mwaka 1984 na Kutungwa Upya Sheria ya Usimamizi wa Uchaguzi ya Mwaka 2017.
2.	Mapendekezo ya Kutunga Sheria ya Kuanzisha Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo vidogo na vya Kati Zanzibar.
3.	Mapendekezo ya Kutungwa kwa Sheria Mpya ya Uanzishwaji wa Sheria ya Bima ya Afya, Zanzibar.
4.	Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali, 2017.
5.	Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Usajili wa Matukio ya Kijamii na Kadi za Utambulisho wa Mzanzibari Mkaazi.
6.	Kuanzisha Sheria ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Zanzibar.
7.	Mapendekezo ya Kutungwa Sheria ya Kusimamia Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji pamoja na Kufuta Sheria Namba 2 ya Mwaka 1995 ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji.
8.	Mswada wa Sheria ya Kufutwa na Kutunga Upya Sheria ya Adhabu Namba 6 ya Mwaka 2004 ya Sheria za Zanzibar.
9.	Mswada wa Sheria ya Kufutwa na Kutunga Upya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Namba 7 ya Mwaka 2004.
10.	Rasimu ya Sera ya Utalii.
11.	Rasimu ya Sera ya Michezo.
12.	Rasimu ya Sera ya Taifa ya Ardhi.

KIAMBATISHO 9: MAPITIO YA UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

JINA LA IDARA	PROGRAMU NDOGO	BAJETI KWA MWAKA WA 2017/2018	FEDHA ZA MIEZI TISA 2017/2018	ASILIMIA YA FEDHA KWA MWAKA
Ofisi ya Faragha ya Rais	Kusimamia Huduma na Shughuli za Mhe. Rais	3,360,876,000	2,009,424,015	60
	Uratibu wa Shughuli za Mhe. Rais (Mradi wa Maendeleo)	730,000,000	500,000,000	68
Idara ya Mawasiliano na Habari - Ikulu	Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi	303,211,000	244,401,205	81
Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	Uratibu wa shughuli za Baraza la Mapinduzi na Majukumu ya KBLM/KMK.	139,531,000	99,075,800	71
	Tathmini ya Utendaji Kazi na uwajibikaji wa Taasisi za Umma	254,499,000	132,424,000	52
	Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	1,313,870,000	1,031,500,200	79

JINA LA IDARA	PROGRAMU NDOGO	BAJETI KWA MWAKA WA 2017/2018	FEDHA ZA MIEZI TISA 2017/2018	ASILIMIA YA FEDHA KWA MWAKA
Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje	Kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kikanda na Kimataifa	306,389,000	227,963,250	74
	Kuratibu Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi	202,065,000	174,005,000	86
Idara ya Uendeshaji na Utumishi	Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	1,240,062,000	888,124,740	72
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za ORMBLM	286,964,000	221,248,570	77
Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Pemba	Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za ORMBLM - Pemba	860,133,000	645,718,763	75
Ofisi ya Usalama wa Serikali (G.S.O)	Kusimamia Usalama wa Watumishi wa Umma	75,000,000	56,262,000	75
	Jumla	**9,072,600,000**	**6,230,147,543**	**69**

KIAMBATISHO 10: MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO	MSHAHARA	UENDESHAJI OFISI	MATUMIZI YA MAENDELEO	MAPENDEKEZO 2018/2019
Kusimamia huduma na shughuli za Mhe. Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu	**2,219,208,240**	**2,779,515,752**	**100,000,000**	**4,998,723,992**
Kusimamia Huduma na Shughuli za Mhe. Rais	2,082,765,300	2,475,099,752	100,000,000	4,557,865,052
Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi	136,442,940	304,416,000	-	440,858,940
Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu	**936,000,000**	**509,800,000**	-	**1,445,800,000**
Uratibu wa shughuli za Baraza la Mapinduzi na Majukumu ya KBLM/KMK.	936,000,000	404,765,000	-	404,765,000
Tathmini ya Utendaji Kazi na uwajibikaji wa Taasisi za Umma		105,035,000	-	105,035,000
Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi		**515,800,000**	-	**515,800,000**

PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO	MSHAHARA	UENDESHAJI OFISI	MATUMIZI YA MAENDELEO	MAPENDEKEZO 2018/2019
Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi	**89,170,320**	**448,795,000**	-	**537,965,320**
Kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kikanda na Kimataifa	89,170,320	270,780,000	-	359,950,320
Kuratibu Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi		178,015,000	-	178,015,000
Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	**1,358,521,440**	**1,576,889,248**	-	**2,935,410,688**
Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	728,107,860	778,899,248	-	1,507,007,108
Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za ORMBLM	146,419,860	261,408,000	-	407,827,860
Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za ORMBLM -	483,993,720	370,000,000	-	853,993,720

PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO	MSHAHARA	UENDESHAJI OFISI	MATUMIZI YA MAENDELEO	MAPENDEKEZO 2018/2019
Pemba				
Kusimamia Usalama wa Watumishi wa Umma	-	166,582,000	-	166,582,000
JUMLA KUBWA	**4,602,900,000**	**5,830,800,000**	**100,000,000**	**10,433,700,000**

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono, muda tuliobakia nao ni robo saa Mhe. Waziri ametumia saa 1 na dakika 8 ambazo ni nzuri sana kwa kutuokolea wakati, naomba huu muda mchache ambao tumebakiwa nao kabla ya kufika saa 6:00 kamili nimwite kabisa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ambae anaesimamia hii Wizara ili aje aanze halafu atakuja kumalizia jioni.

Mhe. Spika: Hawahi? ahsante, Waheshimiwa kwa ushauri wenu sasa basi nitasitisha shughuli za Baraza za Wawakilishi mpaka saa kumi na moja za jioni ambapo Mwenyekiti atakuja kuwasilisha ripoti ya Kamati.

(Saa 6.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)
(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa niaba yake Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Panya Ali Abdalla (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naomba nisome hotuba hii ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Spika, sina budi kwa kuanza kumshukuru Allah (S.W) mwingi wa utukufu na rehma kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la Tisa kwa dhamira ya kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar ambao ndio sababu ya sisi kusimama katika Baraza hili. Aidha, nakushukuru na kukupongeza wewe Mhe. Spika, kwa jitihada zako na namna unavyoliongoza Baraza hili tukufu kwa ustadi na upeo mkubwa. Ni imani yangu kwamba utaendelea kutuongoza kwa uadilifu na ustadi wa hali ya juu kwa lengo la kuimarisha demokrasia katika chombo hiki muhimu cha kuwatumikia wananchi.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuiongoza nchi yetu kwa hekima, busara, uadilifu na ustadi mkubwa kwa muda wote alio madarakani. Hekima na busara zake anazozitumia katika kuongoza nchi yetu ndio ambazo zimetufanya hadi leo kuweza kuishi kwa amani na utulivu. Namuombea kwa Allah (S.W) azidi kumpa nguvu na afya njema ili aweze kutuongoza kwa busara zaidi yeye na wasaidizi wake wote.

Sina budi pia kumshukuru na kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa umahiri wake mkubwa wa kuyasimamia vyema majukumu ya Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, nimshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu), pamoja na watendaji wake wote, wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Wizara hii. Pia kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kazi zao nzuri wanazozifanya wakati wote wa kazi za Kamati, jambo ambalo limepelekea wepesi kwangu kuweza kuiongoza Kamati hii inayosimamia Ofisi muhimu kabisa. Wajumbe wa Kamati wameonesha umahiri, uweledi na umakini wa hali ya juu na wameweza kuijadili ipasavyo bajeti hii na kuhoji mambo mengi ya msingi kwa lengo la kuhakikisha fedha wanazoidhinisha katika Baraza hili, zinatumika vizuri na kwa maslahi mapana kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, napenda kutumia fursa hii pia kuwapongeza na kuwashukuru Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu kwa kuendelea kuwawakilisha na kuwatumikia wananchi waliowachagua. Ni wazi kwamba wananchi wamejenga imani kubwa kwetu, nasi hatuna budi kurejesha imani kwao kwa kuwatumikia kwa dhati na kwa moyo wetu wote kwa dhamira ya kutetea maslahi yao katika Baraza hili tukufu.

Naomba niwakumbushe wajumbe wenzangu kuwa kipindi chetu cha miaka mitano kinakimbia kwa kasi kubwa, hivyo kila mmoja wetu ajitahidi kutekeleza aliyoahidi na kwa pamoja tutakuwa tumemsaidia Mhe. Rais kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kukamilisha ahadi zake kwa wananchi waliotuchagua.

Mhe. Spika, kabla ya kuendelea na hotuba hii, kwa ruhusa yako na kwa heshima ya kipekee naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:

1. Mhe. Omar Seif Abeid — Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla — M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ame Haji Ali — Mjumbe
4. Mhe. Amina Iddi Mabrouk — Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu — Mjumbe
6. Mhe. Mussa Ali Mussa — Mjumbe
7. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame — Mjumbe

Aidha, kamati hii inafanyakazi kwa kusaidiwa na Makatibu wawili ambao wamekuwa wakitusaidia kwa kiasi kikubwa na kwa uweledi wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yetu. Msaada wa makatibu hao umekuwa chachu ya mafanikio makubwa ya kamati hii. Makatibu hao ni:

1. Ndg. Karima Abdul-Wahab — Katibu

2. Ndg.Talib Enzi Talib. Katibu

Mhe. Spika, moja kati ya jukumu la msingi la kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya wizara katika mapato na matumizi ya kila mwaka. Hivyo, katika kutekeleza jukumu hilo lililoelezwa katika Kanuni ya 96(1), kamati yangu ilikaa na kuijadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi siku ya tarehe 2/5/2018, na leo hii kwa ruhusa yako na kwa niaba ya kamati napenda kuwasilisha maoni ya kamati kuhusiana na bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019**.**

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nitekeleze jukumu nililopewa na kamati la kuwasilisha maoni ya kamati, mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ina mafungu mawili tu ambayo ni Fungu **A01**- Ofisi ya Rais Ikulu, na Fungu **A02**-Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, na imepanga kutekeleza programu kuu tano (5) zenye programu ndogo kumi na moja (11) ambazo kwa ujumla zitajumuisha shughuli zote zinazokusudiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 kama inavyoonekana katika kitabu kikuu cha bajeti.

PROGRAMU KUU YA KUSIMAMIA HUDUMA NA SHUGHULI ZA MHE. RAIS NA KUIMARISHA MAWASILIANO IKULU

Mhe. Spika, katika programu hii kuu kuna programu ndogo nazo ni:

1. Programu ndogo ya Kusimamia Huduma na Shughuli za Mhe. Rais

2. Programu ndogo ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi

Programu ndogo ya Kusimamia Huduma na Shughuli za Mhe. Rais inayosimamiwa na Ofisi ya Faragha ina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa ahadi na maagizo ya Mhe. Rais na usimamizi wa nyumba za mapumziko anazozitumia Mhe. Rais.

Kwa ujumla, kamati yangu inapongeza jitihada zinazochukuliwa na Ofisi ya Faragha ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku likiwemo lile la kufuatilia ahadi zinazotolewa na Kiongozi wetu Mkuu wa Nchi katika maeneo tofauti, ambapo kwa mwaka 2017/2018 ahadi za Mhe. Rais zilifuatiliwa na kutekelezwa kwa ufanisi chini ya usimamizi wa Ofisi ya Faragha kama inavyoonekana katika kitabu kikuu cha Bajeti.

Aidha, **k**amati yangu imefurahishwa na inapongeza Ofisi ya Rais kwa kuziimarisha na kuziweka katika hadhi inayostahiki nyumba za Ikulu Ndogo za Micheweni na Chake Chake Pemba. Ujenzi wa Ikulu Ndogo ya Micheweni na Chake Chake ambao umefikia katika hatua ya kuridhisha. Pia kamati imefarajika na Ongezeko la Bajeti kwa mwaka 2018/2019 kwa ujumla wake, hasa katika Miradi ya Maenedeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Faragha yenye lengo la kuimarisha majengo yanayotumiwa na Mhe. Rais, kwa kweli ni jambo la kupongezwa.

Mhe. Spika, kamati yangu inafarajika kwa kuona kuwa maagizo yake yamezingatiwa juu ya tatizo la mmong'onyoko wa ardhi katika Ikulu ya Mkoani ambapo wizara imechukua hatua muafaka kwa kukabidhi fedha kwa ajili ya kazi hiyo kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ili tatizo hilo liweze kumalizika. Ni imani yangu kuwa taasisi iliyokabidhiwa fedha hizo itatimiza wajibu wake haraka iwezekanavyo na fedha

hizo zitatumika vizuri ili kuinusuru Ikulu hiyo isiendelee kuathirika na mmong'onyoko huo.

Mhe. Spika, programu ndogo ya pili ni ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi ambayo inakusudia kuendeleza taswira nzuri baina ya Mhe. Rais na wananchi wake. Kamati yangu imeridhika na makadirio yaliyopangwa katika programu hii.

Pia, kamati imefarajika na hatua zilizochukuliwa na Ofisi ya Rais katika kuimarisha zaidi suala la kumtangaza Rais wetu na kumfanya awe karibu zaidi na wananchi anaowatumikia kwa kuanzisha akauti za mitandao ya kijamii, vipindi vya redio na TV vinavyoonesha shughuli mbali mbali anazofanya Mhe. Rais katika kuwatumikia wananchi. Tumekuwa tukishuhudia matukio mengi ambayo Mhe. Rais anahudhuria huwa yanarushwa moja kwa moja *(Live)* kupitia mitandao ya kijamii hasa akaunti maarufu ya *facebook* ya *Ikulu ya Zanzibar Update.* Jumla ya vipindi 21 vinavyohusu mambo mbali mbali ya Mhe. Rais vimeandaliwa na kurushwa hewani na vyengine vimefanyiwa marudio kupitia redio na televisheni. Kuwepo kwa jarida maalum la Ikulu linaloeleza kazi mbali mbali anazofanya Mhe. Rais ni jambo la kupongezwa.

Aidha, kamati inaomba na kushauri idara ichukue jitihada za makusudi kuwafikia idadi kubwa zaidi ya wananchi, sio tu ndani ya Zanzibar, bali hata nje ya nchi ambapo mitandao ya kijamii inatumika kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika, suala la ziara za Mhe. Rais nalo limeweza kuratibiwa vizuri. Ziara yake katika nchi za kiarabu *(UAE)* imeleta tija kubwa kwa Wazanzibari hasa kwa kutembelea nchi ya Ras al Khaimah ambayo tunatarajia itashirikiana na Zanzibar katika utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi. Ukweli, kufanya hivyo ni utekelezaji wa Ilani ya CCM kwani hilo tuliahidi kwa wananchi kupitia ilani yetu.Tunampongeza Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kulisimamia ipasavyo.

Mhe. Spika, kamati yangu pia, inapongeza kwa kuchukua jitihada za kuweka vipindi mbali mbali vya matukio ya kihistoria yanayohusu viongozi wetu wakuu na nchi kwa ujumla na kuwafanya wananchi wa rika mbali mbali waweze kujua historia ya nchi yao vizuri. Kufanya hivyo kumesaidia kuepusha taarifa za upotoshaji dhidi ya viongozi wetu, sambamba na kuliwezesha rika la vijana kuifahamu vyema historia ya nchi yetu, wapi tunapotoka, tulipo sasa na tunapoelekea.

Hivyo, kamati imeridhika na utekelezaji wa bajeti iliyopita katika programu hii na inatarajia katika bajeti 2018/2019 fedha walizoziomba kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii zitafanikisha utekelezaji wa malengo waliyoyapanga.

PROGRAMU KUU YA KURATIBU USHIRIKIANO WA KIKANDA, MASHIRIKA YA KIMATAIFA NA WAZANZIBARI WANAOISHI NJE NCHI

Mhe. Spika, programu hii ina lengo la kuiwezesha Zanzibar kushiriki kikamilifu katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa na kuwashirikisha ipasavyo Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kwa lengo la kukuza maendeleo ya Zanzibar katika nyanja tofauti.

Mhe. Spika, katika kuona azma ya kuwepo kwa Idara ya Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje inazaa matunda, kamati yangu inasisitiza kuzingatiwa ushauri wake kwamba jitihada zaidi ziongezwe katika kuwavutia wawekezaji wenye asili ya Kizanzibari kuja kuwekeza katika sekta mbali mbali ikiwa ni pamoja na Sekta ya Utalii.

Aidha, idara inatakiwa kujitahidi zaidi kuhamasisha Wazanzibari waliopo nje kusaidia ndugu zao waliopo Zanzibar kama vile walivyofanya Wazanzibari waliopo Denmark ambao wametoa mchango mkubwa wa vifaa katika Sekta ya Afya na Elimu kwa ndugu zao wa Zanzibar kupitia jumuiya yao ya ***AHAS GROUP.***

Mhe. Spika, kamati imefurahishwa na jitihada za idara hii kwa kuweza kutekeleza yale iliyojipangia. Mbali na kuwa idara imeshiriki katika mikutano kadhaa ya kimataifa na kushiriki mikutano ya Jumuiya za Kikanda. Kamati yangu inataka kuona zaidi matokeo ya kushiriki katika mikutano hiyo na namna Wazanzibari wanavyofaidika nayo. Aidha, kuhusu Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia ni mategemeo ya kamati kuona kwamba mikataba hiyo itawanufaisha wananchi wa Zanzibar.

PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA OFISI YA RAIS IKULU

Mhe. Spika, katika programu hii kuna programu ndogo nne nazo:

1. Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

2. Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

3. Uratibu na Usimamizi wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Pemba

4. Usimamizi wa Usalama wa Watumishi wa Umma

Mhe. Spika, kumekuwepo mafanikio kadhaa yaliyopatikana kupitia programu kuu hii ambayo ni pamoja na kuwepo kwa Mpango wa Miaka Mitano wa Rasilimali Watu na Mpango wa Miaka Mitatu wa Urithishwaji Watumishi, Kuimarika kwa Usalama wa Serikali kupitia Ukaguzi wa Wafanyakazi na Majengo na kuanza kwa Utafiti juu ya Fursa zinazopatikana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, licha ya mafanikio hayo yaliyopatikana kwa mwaka wa fedha uliopita 2017/2018, kamati inatarajia kuona kwamba katika mwaka wa fedha 2018/2019, wananchi wa Zanzibar wanafaidika vya kutosha na kupata fursa zitokanazo na uwepo wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kwa mfano, wananchi wengi hata wahitimu mbali mbali kutoka vyuo vikuu hawaifahamu vyema jumuiya hiyo na fursa zinazoweza kupatikana kwa Wazanzibari kutoka katika jumuiya hiyo.

Vile vile, kuhusu kuwepo kwa Mpango wa Miaka Mitano wa Rasilimali Watu na Mpango wa Miaka Mitatu wa Urithishwaji Watumishi, kamati inashauri kuwaandaa wafanyakazi ili wakati wa kustaafu unapofika wawepo warithi wao ili kushika nafasi hizo.

Mhe. Spika, kwa kuwa Programu ya Utawala na Uendeshaji inajihusisha pia na kufanya tafiti mbali mbali kwa dhamira ya kupeleka mbele maendeleo ya Ofisi ya Rais**,** kamati yangu inataka kuona matokeo ya tafiti zilizofanywa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (ORMBLM) kwa mwaka wa fedha 2017/2018, zinawasaidia Wazanzibari kufaidika na fursa zinazopatikana katika soko la Afrika Mashariki, hasa hasa vijana wanaohitimu vyuo vikuu.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Kuratibu na Kusimamia Shughuli za Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Pemba ambayo ina lengo la kuimarisha uwezo wa kiutendaji na uratibu wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (ORMBLM). Kabla sijatoa maoni ya kamati kwa eneo hili, kwa niaba ya kamati yangu naomba kwanza nichukue fursa hii kumpongeza

Ofisa Mdhamini katika Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ndg. Amour Hamad Saleh kwa namna anavyoendeleza jitihada za mrithi wake. Kwa kweli anafanya kazi nzuri, ikiwa ni pamoja na kusimamia vyema masuala ya ujenzi wa nyumba za Ikulu unaoendelea huko Micheweni na Chake Chake. Ni imani ya kamati yangu kwamba nyumba za mapumziko za Mhe. Rais zinazoendelea kujengwa zitasimamiwa vyema chini ya uwepo wake.

Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo wafanyakazi, Ofisi ya Rais inastahiki pongezi kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi 18 katika mafunzo ya muda mrefu kwa viwango mbali mbali na wafanyakazi 25 wameongezewa ujuzi katika mafunzo ya muda mfupi. Kupitia programu hii, wafanyakazi 80 wamepewa mafunzo ya kujikinga na maradhi yasiyoambukiza pamoja na kupima afya zao.

Mhe. Spika, lengo la ldara ya Usimamizi wa Usalama wa Utumishi wa Umma *(GSO)* ni kuimarisha shughuli za upekuzi kwa watumishi wa umma, kabla na baada ya kuajiriwa pamoja na kuhakikisha usalama sehemu za kazi. Kwa ujumla, kamati imeona kwamba utendaji wa kazi wa **i**dara hii una mafanikio pamoja changamoto mbali mbali zinazojitokeza katika utendaji wa kazi zao za kila siku.

Mhe. Spika, idara ya *GSO* ni miongoni mwa idara zenye mazingira magumu ya utendaji kazi. Hata hivyo, tunaipongeza idara hii kwa kuweza kufanya kazi nzuri na kuweza kufanikisha malengo yake kwa kiasi kikubwa. Katika mwaka wa fedha 2017/218, idara imeweza kufanya upekuzi wa watumishi wa umma kwa mafanikio makubwa. Jumla ya watumishi 2,285 wamefanyiwa upekuzi na jumla ya majengo 8 yamekaguliwa.

Aidha, kamati inaipongeza idara kwa kuweza kufikia malengo iliyojiwekea na kuondoa khofu ya kamati ya kutokufikiwa kwa malengo hayo hasa kutokana na kasoro za kisheria zilizo katika sheria inayotumiwa na idara hiyo, sheria ambayo sasa imeanza kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni miongoni mwa idara muhimu ambazo jukumu lake la msingi ni kufanya tathmini ya Sera na Sheria mbali mbali zinazotekelezwa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kamati yangu inaipongeza sana idara hii kwa kuanza kufanya mapitio ya sheria mbili (2) zilizo chini ya Ofisi ya Rais, sheria hizo ni Sheria ya Usalama wa Taifa na Siri za Serikali Nam. 5/1983 inayotumiwa na *GSO* katika kutekeleza majukumu yake na Sheria ya Mambo ya Rais Nam. 5/1993 inayohusu masuala mbali mbali ya Mhe. Rais.
Kamati inaipogeza idara kwa kuzifanyia mapitio sheria hizo na kubaini kasoro zake na hatimaye kupendekeza marekebisho yatakayosaidia sana kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi ya *GSO* na Ofisi ya Rais kwa ujumla. Kamati inasisitiza kupatiwa kiwango cha fedha idara kwa ajili ya utekelezaji wa programu kuu hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Spika, kamati yangu kwa umakini pia imepitia Fungu A02-Ofisi ya Baraza la Mapinduzi ambalo lina Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu, na Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA MAJUKUMU YA KIKATIBA NA KISHERIA YA BARAZA LA MAPINDUZI NA KAMATI YA MAKATIBU WAKUU

Mhe. Spika, **c**hini ya programu kuu hii, kamati yangu imepatiwa ufafanuzi juu utendaji kazi wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha mwaka 2017/2018. Kamati imeridhishwa na inaipongeza Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kutekeleza kwa ufanisi na ubora wa hali ya juu malengo waliyojipangia ikiwemo kufanya vikao vya BLM na Kamati ya Makatibu Wakuu. Jumla ya vikao 20 vya BLM na 28 vya Makatibu Wakuu vimefanyika kwa ufanisi mkubwa. Ni ukweli ulio wazi kwamba vikao hivyo ndio injini ya utendaji kazi wa serikali na kuwepo kwake ndio kunapelekea taasisi nyingine zote za serikali kuweza kutekeleza majukumu yao ambayo mara nyingi hutegemea maelekezo na miongozo ya vikao hivyo.

Aidha, tunaipongeza Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kuandaa vikao vya kutathmini utendaji wa kila taasisi, maarufu kama "Bango Kitita" baina ya Mhe. Rais na kila Wizara ya SMZ ambapo vikao 15 vimefanyika. Vikao hivyo vimekuwa na tija kubwa kwani vinasaidia sana kuona zile fedha tunazoziidhinisha katika Baraza hili zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kuweza kuleta tija ya maslahi mapana ya wananchi tunaowatumikia.

Mhe. Spika, kamati imefurahishwa na kitengo cha ufuatiliaji na tathmini cha Baraza la Mapinduzi kwa kuongeza wafanyakazi wawili wenye ujuzi kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa kitengo hicho. Aidha, kamati imeridhika kwa namna ambavyo kitengo kimeweza kufanya kazi nzuri ya kufuatilia wizara zote katika utekelezaji wake wa Sera, Sheria, Miongozo na Maagizo ya Serikali. Hivyo, kamati yangu inasisitiza kazi hiyo iendelee kwa umakini zaidi ili kila taasisi iweze kufuatiliwa na kutathminiwa namna inavyotekeleza Sera, Sheria, Miongozo pamoja na Majukumu yake ya kila siku kwa lengo la kupeleka mbele maendeleo na juhudi za serikali.

Hivyo, kamati imeridhika kwa kiasi kikubwa fedha walizoziomba Ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kuamini kwamba zitaweza kutekeleza malengo ya Fungu A02 la Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, kwa ujumla, kamati yangu imeridhishwa na utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais ya mwaka 2017/2018 na imeridhia bajeti iliyopendekezwa ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni jumla ya Tsh. 10,433,700,000 kwa Fungu la A01 na A02, zilizoambatana na ufafanuzi wa mipango mbali mbali ya mwaka mzima. Aidha, kamati yangu imeridhika kwa ongezeko la fedha ambalo zimeekezwa katika ununuzi wa Mashine ya Ukaguzi Ikulu, Bajeti ya Washauri wa Mhe. Rais pamoja na shughuli za kumtangaza Mhe. Rais hasa vijijini na Kuimarisha Shughuli za Upekuzi wa Wafanyakazi, ukaguzi wa Majengo na Miundombinu. Aidha, kuimarisha mazingira katika nyumba ya Ikulu Dodoma na Chake Chake (Pemba). Pia, ongezeko la fedha katika kufanikisha Shughuli za Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini, hivyo, kamati inatarajia fedha hizo kutumika kama zilivyokusudiwa katika Bajeti 2018/2019.

HITIMISHO

Mhe. Spika, baada ya maoni hayo ya kamati yangu ambayo yamejikita katika programu kuu na ndogo, nasisitiza kwamba lengo la maoni hayo ni kuimarisha utendaji katika kila taasisi iliyo chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ili kuhakikisha wizara hii inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Aidha, ni imani ya kamati yangu kuwa baada ya hotuba nzuri iliyosomwa na Mhe. Waziri, pamoja na maoni haya ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, nawaomba Wajumbe wengine wa Baraza lako tukufu, waichangie vyema bajeti hii kwa lengo la kupata utekelezaji bora wenye maslahi kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, napenda kukushukuru tena wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati, pamoja na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa. Sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii, ili wamuwezeshe Mhe. Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliyojipangia katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, mimi mwenyewe kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naiunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Panya Ali Abdalla kwa uwasilishaji mzuri sana na uliookoa muda. Sasa Waheshimiwa Wajumbe tutaanza kuchangia na naomba niwataje wachangiaji watatu wa mwanzo. Kwa sasa hivi ataanza Mhe. Ali Suleiman Ali, atafuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na Mhe. Machano Othman Said ajiandae. Mhe. Ali Suleiman Ali. *(Makofi)*

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako Tukufu kuchangia Hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa bajeti ya mwaka 2018/2019. Lakini kwa dhati kabisa nimpongeze sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anazozifanya na pia kukuza uchumi wa nchi yetu, yeye pamoja na Wajumbe wote wa Baraza la Mawaziri kwa mashirikiano na watendaji mbali mbali wa sekta ya fedha katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa niseme kwa moyo wangu, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake leo mazuri ya uungwana kabisa, akasema tu kwamba anawapongeza wana Simba wote wa Tanzania, na amekiri Mheshimiwa kwamba Simba wa mwaka huu mwendo wa kasi sio Simba wa zamani. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri awe na moyo huo huo, lakini umefika wakati abadilike atoke huko aje huku. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi zake nzuri, niseme kwamba Mhe. Rais ni mwelekeo au ni mwelekezi katika shughuli zetu mbali mbali katika nchi yetu. Lakini na sisi ambao tuko nyuma yake tujizatiti kuhakikisha kwamba tunafanya kazi nzuri ili kuiweka nchi na Chama chetu cha Mapinduzi ambacho kinaongozwa na Serikali hii kifanye vizuri katika uchaguzi wa 2020. Lakini jengine Mheshimiwa niseme tu kwamba kadri kitabu hichi kilivyoandikwa mambo yetu mazuri. Mimi naipongeza hotuba hii na naiunga mkono kwa

asilimia 100 na nakiri kwamba wananchi wangu wote wa Jimbo la Kijitoupele walionichagua na wale waliopotea njia ambao mwaka 2020 watanichagua mimi, niseme kwamba tunaiunga mkono hotuba hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Rais katuongoza katika muelekeo mzuri na maendeleo yanaonekana. Niwapongeze mawaziri wote kwa juhudi zao za kusimamia kila kilichoelekezwa, kuhakikisha kwamba faida inapatikana katika kuwaondolea shida wananchi wetu katika maeneo mbali mbali. Mhe. Spika, mimi niseme tu kwamba kwa miaka miwili hii na miezi miwili nahesabu hivyo maana yake kwa kuwa uchaguzi ulianza 20 sisi Machi, 2016 tumefanikiwa mengi, mimi nimefanikiwa mengi kwa upande wangu chini yake Mheshimiwa kwa maelekezo yake mazuri.

Katika kipindi hichi kifupi naanza kusema nimebahatika katika jimbo langu na majirani zangu miundombinu ya maji, maskuli, barabara na miundombinu mingine kadhaa ambayo inaendelea. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wawe karibu na sisi au sisi tuwe karibu na wao tushirikiane, tushauriane ili tukuze hayo tulioendelea. Mhe. Spika, pamoja na hayo niseme tu kwamba, mimi katika kitabu hichi nitachangia machache yafuatayo ukurasa wa 38 *paragraph* ya 97, kuna mazuri hapa yote lakini nitasema machache na wenzangu niwape nafasi waendelee na mengine.

Mhe. Spika, moja Kuratibu Shughuli za Huduma za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Spika, Idara ya Uratibu au taasisi hii ni muhimu kwa sababu inampangia Mhe. Rais kila palipokuwa na mwendo wa hapa na hapa aende aone na afanye kazi zake vizuri kwa maelekezo ya ushauri na maelekezo mengine. Mimi niwapongeze sana kwa hili na nasema tu kwamba ni muelekeo mzuri na ni mwendo mzuri wa kuhakikisha kwamba uratibu ni shughuli muhimu juu ya kujua kile tunachokifanya katika maeneo yetu.

Mhe. Spika, jengine namba 4 ni kuelimisha jamii na viongozi juu ya Sera ya Diaspora ya Zanzibar. Mhe. Spika, tukitaka tusitake kuna vijana wetu wengi wa Zanzibar au wa Tanzania, lakini nachukua Wazanzibari waliokuwepo nje ya nchi, umefika wakati wajitambue kwao na naamini wanajitambua kwao. Kwa sababu baada ya kukaa miaka mingi ambayo walipotea njia walikuwa hawajajifahamu, walipofahamu kila mmoja ana hamu ya kwao kuleta maendeleo kwa kile anachokipata. Naishauri serikali hili ni wazo zuri na ni wazo ambalo linafaa, lakini tuwasaidie kwa hali na mali wenzetu hawa wajaribu kujitambua kila walipo. Kwa sababu wananchi wetu hawa wengi au vijana wetu hawa wapo mataifa mbali mbali, ukenda Uingereza unawakuta, ukenda Marekani unawakuta, ukenda Arabuni na sehemu nyengine, lakini hawakuondoka kama kwa tatizo gani, kutafuta maisha na tunaambiwa tafuta maisha popote kwa maslahi yako wewe na ndugu zako.

Kwa hivyo, kitengo hichi nakipongeza na nawapongeza wenzetu hawa lakini tu kwamba tuzidi kutoa taaluma kuongeza juhudi na kupatikana tija kwa nchi yetu na wao wenyewe. Kwa hivyo, hiyo naipongeza.

Lakini jengine Mhe. Spika, ya sita kuwawezesha wananchi kupata taarifa juu ya utekelezaji wa shughuli ya serikali yao, yaani serikali yetu sote tuliokuwemo humu. Mheshimiwa hilo ni wazo zuri na ni utaratibu mzuri kila kinachofanyika kielekezwe na kitolewe taarifa hii, sio Rais tu hata ikiwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi humu, Madiwani, Wabunge kila tunalolifanya tulitangaze, lionekane na lijulikane kwa sababu kuna watu wanafikiria yote yaliyokuwepo kule yameletwa bila sisi kushughulika na mambo mengine.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba mimi naiunga mkono taarifa hii ni jambo muhimu na bila ya taarifa huna kitu kitakachoeleweka katika jamii yako na wananchi wako. Lakini niwapongeze sana waandishi wa habari. Mhe. Spika, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii nawapongeza tuwatumie waandishi wa habari kwa mema yetu na mazuri tunayoyafanya katika maeneo yetu, bila ya wao huwezi kupata kitu katika maeneo yako. Nawapongeza waandishi wote wa vyombo vyote tuwachukue katika shughuli zetu, watoe taarifa zetu ili tuhakikishe zinaonekana, wale wanaotamba tamba kuhangaika waone aibu na wasifike katika maeneo yetu. Mimi nawapongeza sana waandishi hongereni sana, ongezeni bidii tutakuteteeni katika shughuli zenu zote ili muweze kujulikana na mzidi kujulikana.

Mhe. Spika, ya nane kuwashajihisha hii nishaichangia kwa ufupi kuleta maendeleo katika nchi yetu hii naona haina matatizo. Lakini nyengine kuimarisha upatikanaji wa takwimu katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Spika, takwimu ni muhimu na bila ya takwimu huwezi kupanga chochote. Kwa hivyo, huu ni mpango mzuri na unafaa kwa sababu takwimu ni jambo moja wapo la kuweza kujua tu, mimi nina watu 1,000 utawafanyia nini? Nitazingatia huyu ana shida kiasi gani, takwimu hiyo; hawa wako hivi, hawa hivi. Kwa hivyo, niseme takwimu ni jambo muhimu ambalo lina faida katika utekelezaji na uimarishaji pia wa pato la nchi kujua tu huyu ana kasoro hii amuongezee ili apate faida. Kwa hivyo hii napongeza.

Mhe. Spika, kuimarisha usalama wa watumishi wa serikali na maeneo wanayofanyia kazi, na kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kuipatia ofisi vitendea kazi kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Spika, mfanyakazi anafanya kazi zake, wengine lakini sio wote, wanafanyakazi *kilillah taala* wale wanaojitolea kweli kweli. Kwa hivyo, ofisi hii ina shughuli muhimu kuhakikisha kwamba wafanyakazi wale wanajituma wanafanya kazi zao vizuri, lazima wawe katika uangalizi mzuri wa kuhakikisha kwamba usalama wao kazini, pia afya zao zipo kiasi gani, ili waweze kuongeza tija katika kuimarisha uchumi katika maeneo yetu na sekta mbali mbali katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa jumla nimesema kwamba mimi nimeunga mkono mapema hotuba hii na nimeikubali kwa asilimia 100 na wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele. Lakini nampongeza tena Mhe. Rais tumuungeni mkono kwa juhudi zetu zote, yeye ndio muelekeo wetu kwa kuwa kafanya zuri na sisi tutafute zuri zaidi hatumshindi yeye. Kwa sababu yeye ndio baba yetu lakini tuhakikishe kwamba tunamfuata kutokana na matendo mazuri katika maeneo yetu ili kuwaondolea shida wananchi wetu katika majimbo yetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100 sina tatizo. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, atafuatiwa na Mhe. Machano Othman Said na Mhe. Suleiman Makame Ali ajiandae.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Spika. *Bismillah Rahman Rahim.* Mimi nitaomba kuchangia Hotuba ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi 2018/2019 kama ifuatavyo.

Kwanza nitakuwa na maombi ya moja kwa moja kwa Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye mwenyewe ataangalia kwa mujibu wa uwezo wake aliokuwa nao katika Katiba ya nchi. Jambo la mwanzo kwa Mhe. Waziri ombi langu kubwa kwamba Zanzibar *majority* ni waislam asilimia 99 *point something*, *point* yangu ipo hapa kwa Mhe. Rais na kwako wewe Mhe. Waziri ambaye utafikisha salamu hizi, tungeomba siku ya Ijumaa kama ya leo basi iwe *holiday* kwa Zanzibar. Au kama suala hili litakuwa gumu kwa mujibu wa nchi basi Ijumaa iwe ni *half day* kuanzia asubuhi mpaka saa 6:00 na Jumamosi iwe ni *half day* na Jumapili iwe ni *holiday* kama ilivyo.

Mhe. Spika, nazungumza hivi kwa sababu wenzetu wa dini ya pili wakristo siku ya Jumapili huwa ni siku yao ya kwenda kanisani wanapata siku nzima ya *holiday*. Sisi waislam ambao *majority 99% point something* Zanzibar tunafanya kazi Ijumaa siku nzima. Ukiangalia ni kitu ambacho katika tamaduni zetu na sisi wenyewe hatuko vizuri, hasa mimi mwenyewe si-*support* kabisa kufanya kazi Ijumaa. Leo kurudi hapa Baraza la Wawakilishi siku ya Ijumaa kwangu mimi naona tafrani kwa sababu sisi waislam siku ya Ijumaa ni siku ya sikukuu kwetu. Tunaomba sana Mhe. Waziri ufikishe salamu hizi kwa Mhe. Rais kwa mujibu wa uwezo wake aliokuwa nao siku ya Ijumaa aifikirie ili na sisi waislam tupate angalau kuweza kusherehekea sikukuu yetu.

Mhe. Spika, jengine niende kwa ndugu zetu wa Diaspora ambao Mhe. Waziri mara mbili tatu tumeshakuona kwenye TV unazungumzia sana suala la Diaspora. Hawa ndugu zetu nilishawahi kuzungumza kipindi cha nyuma. Mimi nitatoa mfano hata kwako wewe Mhe. Waziri au kwangu mimi, kwa miaka waliyoondoka ndugu zetu wa Zanzibar kwenda nje kutafuta maisha, hata wewe Mhe. Waziri ungekuwa wakati ule una pesa za kwenda Ulaya ungekuwa umeshaondoka kwenda Ulaya na mimi halikadhalika. Lakini inawezekana wakati huo wewe unavua huna fedha ya kwenda Ulaya ndio maana hujaweza kuondoka kwenda Ulaya. Lakini wapo ndugu zetu ambao walioweza kupewa fedha kwa njia ya kukopeshwa, kuuza vitu vyao, kusaidiwa, wakakusanyiwa wakaondoka kwenda kutafuta maisha, sasa hivi imefika wakati Wazanzibari wanataka kurudi kwao lakini wamekuwa kama wageni.

Mhe. Spika, ningeomba kupitia kwa Mhe. Rais na kupitia kwa Mhe. Waziri kama nilivyotoa mfano huo, tumshukuru Mwenyezi Mungu uendelee kuwa Waziri mpaka ufe madarakani pamoja na mimi haya ndio mambo mazuri kwa sababu ukitoka nje hali

ngumu kama sio mfanyabiashara utakuja kuishia pagumu. Mwenyezi Mungu akujaalie kila la kheri uwepo kwenye nafasi hiyo. Mimi kila nikiona viongozi vijana kama nyinyi mnateuliwa nafurahi, itafika wakati nchi kama hizi tutaongoza vijana na wazee watabaki kutushauri.

Mhe. Spika, lengo langu zaidi lipo kwamba Wazanzibari wale basi angalau Mhe. Rais awaruhusu kuweza kupata kitambulisho yaani *Zanzibar ID*. Sizungumzii kupewa uraia kwanza wa kusema kupewa paspoti. Nazungumzia wapewe *ID* ya Zanzibar ili waweze kumiliki nyumba kwa majina yao na watakapofika angalau nchini hapa wajisikie kwamba wao Wazanzibari hata kama wana paspoti ya nje. Kuna vitambulisho vya Utanzania mbali hicho sikizungumzii, nazungumzia *Zanzibar ID* kwa sababu Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ana uwezo nacho kikadi kile kwa kuweza kumpa mtu yeyote ndani ya nchi hii.

Mhe. Spika nimuombe Mhe. Rais ndugu zetu hawa Diaspora ambao wamepata maisha magumu huko kwenda kufanyakazi katika mazingira magumu na hatimaye wamekuwa wana *invest* sana nchini kwao katika kujenga nyumba nzuri, kufanya biashara na kuwasaidia ndugu zao waliokuwa wanyonge ndani ya Zanzibar. Leo wanakuja mtu na familia yake ya watu saba wameshatoa tiketi zaidi ya milioni 20 maana yake tuzungumze ukweli, tiketi ya rahisi ni dola elfu moja na mia mbili kwa mtu mmoja tiketi za Europe, *economic class*. Anakuja yeye na watoto wake anafika *Airport* analipishwa dola 50 *visa*, haji-*feel* kabisa kama yeye ni Mzanzibari. Hili suala tumuombe Mhe. Rais kwa Wazanzibari wale mbali ya *ID of Zanzibar* wakipewa pia na ile *visa exemption* iwepo kwa ajili yao, ili waweze na wao kujisikia kwamba hii Zanzibar kwamba kuna serikali inatujali. Inawajali lakini *of course* kila wakipata vitu kama hivi *Zanzibar ID, visa exemption* na mambo mengine ya kumiliki nyumba na ardhi basi watakuwa wanajisikia zaidi.

Mhe. Spika, mimi kwenye wizara hii sina mengi na kwa kweli Mhe. Waziri ana bahati kuwepo wizara hii kwa sababu hapati kupigwa na tunaiheshimu. Lakini haya ni maombi yangu makubwa mimi kwa upande wa wananchi wa Zanzibar ambao wapo nje ya nchi, na sisi ambao kwa siku ya Ijumaa Mhe. Rais aifikirie sana, tunataka ndugu zetu wakristo wafaidike lakini na sisi waislam pia tufaidike kupata kusherehekea siku yetu ya Ijumaa.

Mhe. Spika, suala langu jengine kuna kipindi tulikwenda kutembea Mazizini Ngazimia katika nyumba ya Mhe. Rais ambayo ni Ikulu anayoishi. Tulikwenda kutembea kwenye madhehebu ya Wahindu sehemu ya Ngazimia wanaopata kuzikana, kuchomana na kufanya shughuli zao pale juu, kwa kweli kwa hali ya usalama kwa upande ule hairidhishi kabisa. Hili nalizungumza wazi kwamba tumekwenda tumekuta kuna watu wapo karibu na ukuta wa Mhe. Rais kwa upande wa Ngazimia sehemu ya Wahindu ambapo kiusalama siwezi kuongelea, Mhe. Rais nyumba yake inalindwa vipi wenyewe wanajua siri zao.

Mhe. Spika, kwa pale naomba vyombo vya ulinzi viende vikaangalie na isiruhusu kabisa katika eneo lile la juu watu kufanya mazoezi wala kukaa katika eneo lile. Wanataka mazoezi waende baharini wakishakumaliza baharini watafute njia watoke. Haiwezekani

nyumba ya Mhe. Rais iko hapa watu wanafanya mazoezi ndani ya mita 10 na nyumba ya Mhe. Rais unaiona. Tumekwenda mimi na Kamati yangu na Mheshimiwa *DC* tumekuta kuna watu wahuni kabisa ambao nikizungumza wahuni kwamba wanavuta unga, wanavuta bangi, tumewaona kwa macho yetu. Nasikia wakati mwengine kunafanywa mpaka disco dogo pale kunapigwa mziki watu wanakusanyana karibu ya ukuta wa Mhe. Rais. Tungeomba sana wizara yako ikaenda kusimamia watu pale maeneo yale na hasa wenyewe wale Wahindu hawataki kabisa kwa sababu pale kuna makaburi.

Mhe. Spika, niende kwenye masuala ya moja kwa moja yanayomhusu Mhe. Rais na jitihada zake anazozifanya katika nchi yetu. Nizungumze wazi kabisa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015/2020 Mhe. Rais naweza kusema takriban ameshaimaliza. Nazungumza hivyo mimi nikijipigia hesabu ndani ya jimbo langu vitu alivyoviahidi vyote naweza kusema ameshavikamilisha kwa asilimia 95.8 na ikimalizika barabara ambayo ameshailipia ya kutoka Bububu hadi Mkokotoni basi itakuwa kwa ufupi ahadi zake kwa asilimia 100 atakuwa ameshakamilisha. Hili tayari ameshalipia, Wachina wemeshaanza kazi na kazi kwangu mimi imeshakamilika. Ndani ya jimbo langu katengeneza soko kubwa la kisasa, katengeneza mradi wa maji mkubwa, katengeneza Kituo cha Afya Kikobweni, barabara pamoja na vitu vyengine.

Mhe. Spika, mimi nimpongeze sana Mhe. Rais pamoja na viongozi wake wote ambao wanamshauri, viongozi wa Wizara yake Mhe. Waziri pamoja na Makatibu wake wote na watu wote ambao wanamshauri kuweza kufanya kazi kwa pamoja, pamoja na kutekeleza ahadi ya Chama cha Mapinduzi. Hakuna jambo jengine lolote la kusema labda mtu anaweza akamsema Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ni Rais ambaye anajitahidi kadri ya uwezo wake kuweza kuitengeneza nchi kwa njia yoyote ikiwa kwa njia ya fedha *cash* au kwa njia ya kukopa lakini anataka kuona nchi inatengenezwa.

Mhe. Spika, niwaombe wale ambao wanafanya mambo ambayo watairejesha serikali nyuma au watakuja kumuingia Mhe. Rais aonekane kwamba hafanyi kazi zake vizuri hasa kwenye masuala ya barabara. Ukiangalia barabara zote Zanzibar ni mbovu, hujui hii imetengenezwa mwezi gani, hii mwaka gani, zote zina mashimo kama utauotesha mti utaota. Tungeomba watu wote wanaopewa dhamana katika masuala ya serikali hasa katika mawizara, basi wawe waadilifu waweze kumpa heshima Mhe. Rais kama alivyo yeye. Mimi binafsi katika fahamu zangu sijawahi kusikia Rais anapewa sifa nyingi kama yeye na wengineo, lakini kila mmoja kuna kuzidiana.

Mhe. Spika, Rais wetu tuliyekuwa nae sasa hivi hatujawahi kusikia kachukua kiwanja cha mtu, hatujawahi kusikia kachukua nyumba ya mtu, hatujawahi kusikia kakamatwa na pesa feki, wala kaingia kwenye magendo au kwenye *corruption.* Hivi ndio kiongozi tunayemtaka, kama kunawezekana kuongezwa muda kama atataka mwenyewe aongezewe tu hakuna jengine. Mhe. Spika, nazungumza sio kama nampa sifa kwa kuwa Rais wangu au chama changu, lakini hii ni hali halisi. Mimi binafsi nimeshafanya *research* ya nguvu kwake yeye sijawahi kukamata hata kipande cha tende kwamba kakichukua. Hii inaonesha dhahiri kwamba Marais kama hawa ndio tunaowataka na hivi ndivyo anavyotekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jana hapa tumepitisha Bajeti ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tumempa heshima yake tumeona kwamba kitabu chake kipo vizuri, lakini na kwa Mhe. Rais vile vile kipo kizuri zaidi. Haiwezekani tumpitishie naweza kusema mtoto wake au msaidizi wake, maana yake yeye atakuwa baba, yule atakuwa ndugu, tukamuachilia tukampitishia kwa heshima zote, halafu leo Mhe. Rais kitabu chake hichi aje ainuke mtu humu apige buti nitashangaa sana. Nitawaomba Waheshimiwa wote kama heshima tuliyompa msaidizi wake ambaye ni Makamu wetu wa Pili wa Rais, basi na Rais iwe mara mbili watu wakae kimya hata hiyo ndio wapige mara nne. (*Makofi)*

Mhe. Spika, mimi niwahakikishie Wawakilishi wenzangu kwamba mimi binafsi Mwakilishi wa Jimbo la Chaani ninayemtetea ni Mhe. Rais tu, Wizara zilizobakia zote watakoma. Hapa ni Wizara mbili tu, Wizara tunazozipa heshima ni mbili tu, Mhe. Rais na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hakuna nyengine. Hizi tumeona kwa sababu zina uhakika hatutaki kuwaambia kitu kwa sababu viongozi wetu wako vizuri. *(Makofi)*

Baada ya hayo…

Mhe. Spika: Dakika tatu zimebaki Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf: Mimi ushauri wangu ndio huo. Mhe. Spika, ushauri wangu Mhe. Rais hapa hakuna mjadala wala ingekuwa hakuna haja ya kusubiri Jumatatu, lakini ndio kwa mujibu wa Sheria na Kanuni tutampitishia hakuna mtu atakayesimama na atakayesimama atapambana na mimi nje. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, nazungumza hivi kwa sababu leo nimefurahi sana siku ya Ijumaa na ananifurahisha Mhe. Rais na vitendo vyake kuwa ni muadilifu na sisi binafsi wananchi wote anatupenda, hasa na ushirikiano mzuri baina ya sisi Wawakilishi tunapokuwa na shida zetu, tunapokuwa na maombi yetu, tunapotaka kuja kuzungumza nae hajawahi kudharau, wala hajawahi kusema haji, hii peke yake ni heshima kwetu. Ningeomba Waheshimiwa wengine kwamba wasiwe na wasi wasi kama vitabu vyao vitakuwa vizuri tutawaachilia, lakini kama vitakuwa vibaya watakuwa na kazi ya kuinuka na kusimama mpaka watujibu tutakaporidhika.

Mhe. Spika, baada ya hayo niipongeze Wizara yote pamoja na Mheshimiwa kijana kama nilivyosema nafurahi kuona Waheshimiwa vijana kuteuliwa. Mimi natamani siku za mbele wazee wote wabaki kuwa washauri vijana tuongoze nchi. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameshaanza kukubali kwa sasa, sasa hivi anateua vijana tu, kwa maana hiyo anawa-*train* ili tuje tuongoze nchi.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono asilimia efu moja badala ya mia moja kitabu hichi. Ahsante sana.

MWONGOZO

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf wakati anazungumza alizungumza lugha ya vitisho kati yetu ili tusiweze kupitisha bajeti hii. Kwa hivyo, naomba mwongozo wako tufanye nini ili tuweze kupitisha bajeti hii.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa. Waheshimiwa nadhani hakuna haja ya kuwa na wasi wasi kwa sababu tunaongozwa na Kanuni, hivi vitisho vipo vingi, hata Bungeni nafikiri mnasikia vitisho vinatoka kwa baadhi ya Wabunge kutishia Zanzibar, lakini haviwezi kusaidia. Kwa hivyo, hilo lisikushughulisheni, tunakwenda kwa mujibu wa Kanuni zetu. *(Makofi)*

Naomba sasa nimwite Mhe. Machano Othman Said, atafuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali, na Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo) ajiandae.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka salama na uzima kuweza kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Spika, jambo la pili nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kitabu chake kizuri na kwa kukiwasilisha vizuri.

Mhe. Spika, jana wakati tulipokuwa tukijadili hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, baadhi yetu tulizungumzia umuhimu kwa watu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kitabu chao nao wamekiandika kwa *details* ziara za Mhe. Rais ili kila mmoja ajue ziara zikoje. Lakini kwa bahati nzuri leo kitabu hichi humu ziara za Mhe. Rais zimepangwa vizuri, zimepangwa ziara ya nchi aliyotembelea, nani kaonana nao na kwa madhumuni gani. Pia kitabu hichi kimepanga wageni ambao Mhe. Rais kawapokea Ikulu kwa tarehe na wakati. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake kwa jinsi ambavyo wamekipanga kitabu hichi vizuri.

Mhe. Spika, kwa hakika leo tunazungumzia bajeti ya Mhe. Rais wetu au ofisi yake. Mwenyekiti kazungumza vizuri, Mhe. Nadir Abdul-latif na yeye kazungumza vizuri ingawa kwa lugha kali. Lakini mimi naiunga mkono ile lugha aliyoitumia leo. Ni vyema kwamba tuzungumze na tuangalie mapungufu kama yapo, lakini baadae tuunge mkono bajeti hii kwa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kwanza la mwanzo nimpongeze Mhe. Rais, ameweza kuisimamia na kuiongoza nchi yetu kwa amani, kwa utulivu mkubwa. Nafikiri tulipoanza kuingia mwaka 2016 mwanzoni baada ya uchaguzi wa marejeo mitaani maneno yalikuwa mengi sana, lakini hatimaye sasa hakuna mwenye maneno, kila mtu amejionea kwamba serikali hii inakwenda vizuri na kwa bahati nzuri mapato yamekua kwa kiwango kikubwa sana kuliko ilivyokuwa mwanzo. Hali ya kifedha nafikiri ya serikali yetu ni nzuri na utekelezaji wa ilani unakwenda vizuri kwa Chama chetu cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais amejitahidi sana kutembelea Wilaya na Mkoa kwa Unguja na Pemba na amekutana na wananchi. Yapo baadhi ya mambo ambayo mtu ukitaka

kuuliza katika bajeti hii, lakini kwa sababu ya ziara za Rais unaona kwamba majibu umeshayapata huko, kwa hivyo hapa unakazia tu na kuunga mkono bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nizungumze mambo kama mawili au matatu. La kwanza la ushirikiano wa kimataifa na kikanda. Mhe. Spika, hii ni sekta muhimu sana katika ofisi hii na kwa bahati nzuri Tanzania kikanda hapa tuna makanda mawili ambayo tuna ushiriki wa kudumu. Tupo katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki yenye nchi sita sasa na tuko Ukanda wa *SADC,* kote huko Tanzania tumo. Kwa sababu Tanzania tumo maana yake na Zanzibar tumo.

Kwa hivyo, niombe tu kwamba ziko wizara za kudumu za kushiriki katika mikutano ya kikanda hapa Zanzibar na waratibu wao ni Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, niombe sana tushirikiane na wenzetu Bara ili kuhakikisha kwamba Zanzibar na sisi tunashiriki, na tusishiriki katika ngazi za mawaziri tu, tuanze kushiriki katika ngazi za chini za watendaji katika vikao vya Tanzania vya kuandaa ajenda na kupenyeza mambo yetu yenye maslahi na Zanzibar.

Vile vile sisi kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yako maeneo ambayo tuna maslahi binafsi kama Zanzibar. Zipo nchi ambazo tuna maslahi nazo. Mhe. Spika, kwa wafanyabiashara wengi wa Zanzibar ambao wanakwenda China, ni nadra sana kama hakwenda katika Mji wa Guangzhou katika Jimbo la Guangzhou lina wakaazi karibu milioni 110. Watanzania na Wazanzibari ambao wapo kule wengine wameamua kuishi, wengine wanafanya biashara na kurudi, lakini wanapata tabu kubwa kwa sababu *visa* za China kwa Watanzania inabidi kila mwisho wa mwezi watoke wakagonge *visa* warudi tena.

Kwa hivyo, niiombe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ifanye ushawishi kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili tufungue Ubalozi Mdogo katika Mji wa Guangzhou ili ulete tija kwa wafanyabiashara na Watanzania na Wazanzibari ambao wanakwenda China kwa shughuli zao za kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, pia tunalo tatizo la muda mrefu kidogo la kutokuwa na Ubalozi katika nchi ya Cuba, na wao Wacuba wapo tayari sana kwa sababu hapa Tanzania wanao Ubalozi, na Serikali ya Jamhuri ya Muungano umeahidi kufungua ubalozi Cuba.

Sasa niombe tu basi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nayo kwa sababu sisi na Cuba tuna uhusiano pia wa karibu na maalum iwekeze nguvu kuishawishi serikali ifungue haraka, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ifungue haraka Ubalozi nchini Cuba ambao utatusadiana sana Zanzibar kama katika masuala ya afya, utalii na mambo mengine. Matarajio yangu kwamba Mhe. Waziri kama ambavyo amefanya juhudi za kuwasiliana na watu wa Morocco, basi pia watafanya juhudi kwa ajili ya China na Cuba ili Zanzibar tuweze kunufaika na masuala haya.

Lakini pia nilitaka kujua katika haya ya mambo ya Diaspora ni jambo zuri na bahati nzuri tumeona juhudi zetu za Serikali yetu katika kuwashawishi hawa, lakini sijaliona eneo moja kama linafanya vizuri, eneo la kurejesha fedha nyumbani ambapo nchi za wenzetu

kama Kenya, Somalia wanapata fedha nyingi sana kwa kupitia mirejesho ya kibenki na miamala ile inakuja inasaidia nchi katika kukuza uchumi.

Tatizo ninaloliona kwa Zanzibar wengi ambao wanaleta fedha, fedha sijui zinakuja kwa Said Mmaka zinakwenda sijui kwa nani, anapewa mtu mfukoni anayekwenda London, anayekwenda Canada, sasa hatusaidii sana uchumi wa nchi katika kujiimarisha ingawa zinawasaidia wananchi lakini hazisaidii uchumi wa nchi. Nafikiri kuwe na utaratibu mzuri ambao utasaidia kuonekana kwamba kweli, kwa sababu tukifanya hesabu Wazanzibari ambao wako nje ya nchi ni wengi sana, katika balozi zetu wakiitwa wanakwenda wengi mpaka wanajaa. Nasikia mara ya mwisho Watanzania waliitwa katika Ubalozi wa Tanzania Oman, mkutano haukufanyika kwa sababu Ubalozi ulijaa na watu wengine wakawa hawana pa kukaa katika hoteli. Sasa hili nalo tuone kwamba lina umuhimu.

La mwisho kwa sababu sikutaka kuichangia sana wizara hii niombe tu kwamba pamoja na juhudi nzuri za Kitengo cha Mawasiliano Ikulu kinafanya kazi nzuri, lakini ni vyema kiimarishwe zaidi kwa sababu kitengo kile ndio roho ya Mhe. Rais katika mambo ya habari na mambo ya uenezi na kueleza mambo ambayo Rais wetu ameyatekeleza.

Mhe. Spika, baada ya hayo mimi sikuwa na mengi naunga mkono kwa niaba ya wananchi wa Mfenesini bajeti hii kwa asilimia 100 na nawaomba waheshimiwa wenzangu waunge mkono kwa sababu bajeti nzuri na inaonekana wazi wazi. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Machano Othman Said, sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali atafuatiwa na Mhe. Ali Khamis Bakar na Mhe. Simai Mohammed Said ajiandae.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye Hotuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, kabla ya kuchangia kwanza niwapongeze sana watendaji wote wa Wizara hii pamoja na watendaji waliokaa katika kujadili na kuhakikisha kwamba wanaipanga bajeti hii ya mwaka 2018/2019, niwape hongera sana kwa kazi ngumu walioifanya hiyo na kuhakikisha kwamba kwa lengo la kutuletea maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya hapo nende moja kwa moja kwenye mada. Mimi sana nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uadilifu wake, uhodari na uchapa kazi ambao wananchi wa Zanzibar wamemchagua kwa kumuamini kwa kuwaletea maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, niwaombe sana watendaji wote ambao wameteuliwa na Mhe. Rais, kuanzia Ofisi ya Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi hadi Mawaziri wasimuangushe Mhe. Rais na wawe waadilifu katika kutenda kazi ili kuhakikisha kwamba tunapata maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwani kuna baadhi ya watendaji wengine si waadilifu, wengine ni wadanganyifu. Hata kwenye msimu ule wa karafuu uliopita kuna baadhi ya maeneo Mhe. Rais alidanganywa matokeo yake yakatokea yale. Sasa Mhe. Rais kawaamini na yeye ndio wasaidizi wake, kwa hiyo niwaombe sana kuhakikisha kwenye hili wanamuunga mkono na kutekeleza yale ambayo wamepewa dhamana zile ili kuhakikisha kwamba tunapata maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, niombe sana wajumbe wenzangu kuiunga mkono bajeti hii ya Mhe. Rais ili kuhakikisha kwamba anapata pesa katika ofisi yake na kutuletea maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nina imani kwamba majimbo mengi hapa ya Zanzibar likiwemo jimbo langu la Ziwani kwenye fedha hizi zitafikiwa ambazo kuhakikisha Mhe. Rais anakwenda baadhi ya maeneo mengine anatoa ahadi na pesa hizi ndizo atakazotekeleza kwa huko majimbo kwetu ili kuwaletea wananchi maendeleo.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye suala la wale wenzetu Diaspora, alisema Mhe. Nadir Abul-latif Yussuf na Mhe. Ali Suleiman Ali kwamba mtu kwao ni ngao. Wenzetu walioko huko Ughaibuni nao wana kazi kubwa na pia wameelewa umuhimu wa Zanzibar, umuhimu wa mtu ni kwao, wanajitahidi kukushanya hicho walichonacho wanaleta huku ili kuhakikisha kwamba sisi ndugu zao tuliokuwepo huku tunapata maendeleo.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende moja kwa moja katika kuwaomba wajumbe wanzangu kuipitisha bajeti hii kwa asilimia 100 ili kuhakikisha kwamba tunampa uwezo Mhe. Rais, na bila ya kuzuia kifungu chochote kuhakikisha kwamba Mhe. Rais anaetekeleza yale aliyokusudia kuyatekeleza na ofisi yake kwa ujumla.

Mhe. Spika, mimi sina mengi ya kusema kwenye hotuba hii isipokuwa ni kuunga mkono na niwaombe wenzangu sana kwamba tuunge mkono na tuipitishe bajeti hii bila ya kikwazo chochote. Kama tulivyompitishia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais , basi na Mhe. Rais tumpitishie ili kuhakikisha kwamba tunapata maendeleo katika nchi yetu. Mhe. Spika, mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Suleiman Makame Ali, sasa naomba nimwite Mhe. Ali Khamis Bakar atafuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil ajiandae.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia hutuba hii ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kwa siku ya leo tukiwa wazima na afya njema, lakini vile vile atujaalie Mwenyezi Mungu tumalize shughuli zetu salama katika siku ya leo Ijumaa ili turudi majimbo kwetu, lakini vile vile turudi katika sehemu zetu tunazoishi tukiwa wazima.

Mhe. Spika, nianze katika suala la kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kutuletea maendeleo endelevu ambayo mimi ni shuhuda katika jimbo langu la Tumbe nikianza katika Sekta ya Elimu.

Mhe. Spika, mimi nimefaidika sana katika kipindi chake cha uongozi kupata skuli tano jambo ambalo hapo nyuma lilikuwa halipo. Nimefaidika kupata skuli tano mpya kabisa nzuri na kwa kusema ukweli sasa hivi wanafunzi wanasoma vizuri, wazee wao wameridhika. Wakiwa ndani ya uongozi wa Mhe. Rais hapo nyuma ilikuwa wanafunzi hawa wanakwenda shule wakiwa wanakaa katika mazingira ambao ni magumu lakini sasa hivi wanakaa katika madarasa ambayo ni mazuri wanapata vikalio. Lakini zaidi Mhe. Spika, katika kipindi hiki cha uongozi wa Mhe. Rais tumeona kwamba kuna pesa za *TASAF* zinazotolewa vile vile zinaleta ufanisi zaidi kuweza kufaidika kwa wananchi na watoto hawa kwa kupata sare lakini vile vile mabuku na baadhi ya mambo mengineyo.

Mhe. Spika, kuhusu suala la afya niendelee kumpongeza Mhe. Rais katika Jimbo langu la Tumbe vile vile nimebahatika kupata vituo vitatu vipya katika kipindi hiki cha uongozi wake. Kwa hiyo, ni suala la kujivunia na la kupigiwa mfano, kwa kweli wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe wamefaidika na wamepungua kutembea masafa marefu kufuata huduma ndogo ndogo katika hospitali ya Micheweni ambayo ndio *Cottage* kwa Wilaya ya Micheweni. Lakini wanabahatika kupata huduma hizi kwa kupitia ndani ya shehia zao, Shehia ya Tumbe hospitali hii ipo, Shehia ya Chimba hospitali hii ipo, lakini vile vile na Shumba Viamboni hospitali hii ipo.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije kwenye suala la maji nipongeze vile vile serikali kwa kusimamia vyema suala hili. Mimi katika Jimbo langu la Tumbe suala la maji nimetekelezeka kwa asilimia 80.9. Kwa sababu hapa Mhe. Spika, katika jimbo langu nimebahatika kuchimbiwa visima vitatu na kwa kweli sasa hivi katika jimbo langu hakuna hata sehemu moja ambayo hakuna mtu ambaye hakupata huduma ya maji. Nampongeza sana Mhe. Rais lakini vile vile nampongeza sana Mhe. Ofisa Mdhamini Pemba (JB) kwa kazi nzuri aliyoifanya. Kila baada ya hatua anapoona kuna sehemu labda wananchi wangu hawajapata maji basi ananipigia simu ananambia Mhe. Ali kuna sehemu fulani, kijiji fulani wananchi wako hawajapata maji tushirikiane tupeleke maji ili kwa kutatua matatizo ya wananchi. Mhe. Spika, nashukuru sana hilo suala tunalifanya na linaendelea vizuri. (*Makofi)*

Mhe. Spika, niende katika suala la umeme vile vile katika jimbo langu limetekelezeka vizuri isipokuwa katika kijiji kimoja. Nina imani kwa juhudi za serikali na uongozi wa Mhe. Rais wetu mpendwa na hili nalo litakaa sawa.

Mhe. Spika, kwa kweli mengi mazuri wenzangu walikwisha kuyataja na kuona kwamba kuna haja ya kujivunia katika uongozi wa Rais wetu mpendwa ambaye siku hadi siku halali usiku na mchana kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata huduma ambazo zinastahiki katika nchi yao wanayoishi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niipongeze vile vile serikali kwa kuona kwamba kuna wananchi walioathirika na mvua lakini vile vile ambao waliathirika kwa njia nyengine ya

upepo na baadhi ya mambo mengine. Niipongeze serikali tu kwa juhudi kubwa ambazo zitafanyika najua tukiiunga mkono hutuba hii pesa zitakazopatikana vile vile zitashirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutekeleza haya majukumu ambayo yapo.

Mhe. Spika, mimi katika jimbo langu la Tumbe nimebahatika tena niwaambie tu Wawakilishi wenzangu mimi napokea wageni kwa sababu nashukuru kwamba kuna nyumba ishirini na tano zitajengwa kwa walioathirika na mvua na mambo mengine. Najua watatoka sehemu mbali mbali katika Pemba kwa sababu jana hapa hotuba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais imesema kwamba kutajengwa nyumba hizi kwa upande wa Unguja, lakini kwa Pemba zitajengwa ndani ya jimbo langu la Tumbe. Kwa hiyo, najivunia sana matunda haya kuona kwamba serikali inawajali wananchi wake, lakini vile vile na sisi kama viongozi itabidi tushirikiane kuhakikisha kwamba maendeleo haya yanapatikana.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema kwamba naishauri serikali kuna jambo ambalo jana lilijitokeza Mhe. Waziri wa Afya alilizungumza kwa aina yake na mimi naomba hapa niseme kitu. Mhe. Spika, tumeona kwamba nchi za wenzetu unapokwenda basi mbali ya ile *visa* au tiketi uliyokwenda nayo jambo la mwanzo unalochunguzwa basi ni sehemu ya cheti ambacho ni cha kuangalia afya yako.

Mhe. Spika, sijui kama jambo hili hapa serikalini lipo ama ni vipi, na kama lipo basi kuna baadhi ya sehemu nyengine wanabakisha mianya ambayo inawafanya wananchi wanaoingia katika nchi yetu kunatokea baadhi ya mabalaa. Mhe. Spika, nasikia kuna homa inaitwa homa ya mapenzi mtu akikuangalia tu kishakuambukiza. (*Makofi)*

Sasa hii homa imekuja Mhe. Rashid Makame Shamsi anasema iliingia jimboni kwake hii homa mtu akikuangalia kishakuambukiza. Sasa hii homa kusema ukweli watu nasikia ilitokea kwa upande wa Kenya kuna mwananchi ambaye aliingia katika nchi yetu ya Unguja hakujulikana wapi alitokea baada ya kufika tu tayari aliweza kuambukiza.

Naishauri sana serikali liangaliwe jambo hili kwa wale wananchi watakaoingia ndani ya nchi yetu kuingia bila ya kibali na mambo mengine waangalie jambo la mwanzo kuweka kifaa maalum kwa ajili ya kuwachunguza hawa kama mtu ana maradhi yake tusione bora pesa, bora utu kuliko kitu. (*Makofi)*

Mhe. Spika, mimi napenda sana kwamba watu hawa wachunguzwe hata kama mtu atakuja ku-*invest* mamilioni ya pesa tuache pesa zake lakini asije akatuletea mabalaa mengine. Kwa kusema ukweli Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu atuepushie mbali maradhi haya yangesambaa basi nina imani kama tungepoteza roho kwa asilimia kubwa, lakini Mhe. Waziri wa Afya jana alisema yumo katika kufanya uchunguzi Jumatatu tutapata taarifa. Mhe. Spika, kuna maradhi mengine hayasubiri Jumatatu pale pale yakikushika unakufa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naipongeza sana serikali yangu, naipongeza sana wizara na watendaji wake wote Mwenyezi Mungu awajaalie mzigo huu waliopewa

waende nao vizuri wamsaidie Mhe. Rais tukishirikiana na sisi Wawakilishi ili kufanikisha nchi yetu iende vizuri. Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. (*Makofi)*

Mhe. Spika ahsante sana Mhe. Ali, naomba sasa nimwite Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) atafuatiwa na Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil na Mhe Rashid Makame Shamsi ajiandae.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kutangulia kukushukuru wewe ikiwa Ijumaa hii leo kuweza kuwa na sisi hapa. Lakini pia nitakuwa mkosefu wa fadhila nisipowapongeza Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote na Waziri mwenye dhamana Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) kwa kazi nzuri ya kutuletea bajeti hii leo pamoja na maelezo mengi mazuri yaliyopendeza hasa ukizingatia ofisi yenyewe. Mimi kwa upande wangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunguu nitapenda nitoe mawazo yangu na niweze kuiachangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusu makadirio na mapato matumizi ya fedha kwa mwaka 2018/2019.

Mhe. Spika, ukiangalia ofisi hii na mambo mengi ambayo yamekuwa yanafanyika au yanasimamiwa na kiongozi wetu Mhe. Rais, basi unaweza kusema kwamba maelezo yaliyokuwemo katika kitabu chetu hiki tulicholetewa leo au hotuba iliyosomwa na yeye mwenyewe yapo sawa sawa au yanakwenda sambamba, yote ni kweli na unaweza ukayaangalia na ukayavuta ukayaona kabisa.

Lakini na mimi pia nitapenda nitoe pongezi zangu katika maeneo ambayo tayari tumeanza kuyaona na mafanikio makubwa. Moja ambalo nataka nimpongeze Mhe. Rais mwenye ofisi yake Mhe. Waziri mwenye dhamana ni katika suala zima la afya na elimu kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi kwa upande wa jimbo letu la Tunguu tuna mpango wa kujengwa Hospitali ya Rufaa, lakini pia na Chuo cha Tiba katika eneo la Binguni. Najua mchakato umeanza na naamini kwa busara za Mhe. Rais mwenyewe pamoja Waziri mwenye dhamana basi watahakikisha kama ilivyotajwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ifikapo mwaka 2020 tutakuwa tayari tumeshachukua hatua kubwa ili anayekuja kufuata aweze kuendeleza mawazo ambayo haya yote ameanza nayo yeye mwenyewe. Kwa sababu lazima tukiri, unaweza ukakuta jambo katika ilani lakini lazima kila kitu kina kianzio chake, na mwenye mawazo na ndoto hii ni yeye mwenyewe Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwapa au kujenga hospitali ya kisasa katika Mkoa wa Kusini Unguja katika eneo la Binguni Jimbo la Tunguu.

Lakini pia katika suala la elimu kitendo cha kuweza kuwaondolea wanyonge hasa watu wengi ambao ni maskini katika skuli za msingi kuchangia na naamini zoezi hili litaendelea pia katika skuli za sekondari. Tunaweza tukaona jambo dogo lakini kwa kweli kwa wananchi wetu kama utaangalia hata mimi jimboni kwangu kule Tunguu na mkoa wetu wa Kusini basi ni jambo ambalo itakuwa limewakomboa na limeweza kuwasadia na kuwapa unafuu wananchi wengi wa Zanzibar ili kuweza kuwasaidia katika suala zima.

Lakini pia kuwapa juhudi na motisha vijana hasa na wazee kuwapeleka watoto wao katika skuli za msingi na kuwapa nguvu pia kuendeleza elimu yao katika skuli ya sekondari.

Eneo jengine ambalo halihitaji kusemewa sana lakini linaonekana ukipita Mnazi Mmoja sasa hivi sio kama zamani, unapotoka mjini sasa hivi ukitoka katika uwanja wa *basketball* unapofika Mnazi Mmoja zamani ulikuwa unaangalia kulia kwenye Ofisi ya Mhe. Mahmoud Thabit Kombo Waziri wa Elimu, lakini siku hizi lazima utaangalia mkono wa kushoto kwa sababu kuna jengo jipya pale na linavutia. *(Makofi)*

Wewe unapoingia mjini sasa hivi mandhari katika mji wetu imebadilika katika sura na hadhi, na unapoangalia lile jengo watu wengine hukuuliza kwani ile hoteli, basi watu wengine huwaambia pale ni hospitali bwana, ni hospitali ya kisasa ya rufaa imejengwa na serikali iliyokuwepo madarakani na Chama cha Mapinduzi ikiongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hiyo, pongezi ziende sana kwake yeye pamoja na kule kwetu tukenda Pemba Hospitali ya Abdalla Mzee.

Lakini eneo jengine nataka niligusie pia ni suala la Afrika Mashariki. Mhe. Spika, marehemu baba yangu alikuwa na kibao ofisini kwake kinasema hivi: *When you do right no body remember, but when you do wrong no body forget.* Yaani kwamba unapofanya kitu sawa hakuna mtu atakayekumbuka, lakini pale utakapokosea kila mmoja atakunyooshea mkono. Sasa hapa nia yangu ni kwamba nataka kusema hivi au hoja yangu ni hii. Ni kwamba mengi ambayo tunakuwa tunayaona tunayachukulia au *we take for granted*. Kuna mambo mazuri sana yamekuwa yanafanywa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kushirikiana na Mawaziri wake, lakini mengi haya pia tunayachukulia kama kawaida. Jambo la kwanza ni umoja, amani ambao tulikuwa tuna *enjoy* sasa hivi Zanzibar kwa muda muda wa zaidi ya miaka minane tangu imekaa serikali yake.

Hapa leo tunapozungumza suala la utalii ingekuwa hakuna umoja, hakuna amani, hakuna utalii, hakuna Darajani biashara, hakuna lolote ambalo lingeweza kufanyika. Leo tungesema ama tungeangalia masuala ya kodi ambayo imeongezeka ingekuwa hatuna amani hiyo basi hizo kodi na fedha tungekuwa tunazitafuta hapa kupandisha mishahara na mambo mengine. Haya yote yamefanikiwa kutokana na busara zake. Niseme penye wengi pana mengi, sio wote ambao ni Wazanzibari ambao wanaishi ndani ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba katika nchi yetu wanatutakia mema.

Lakini viashiria ambavyo vilivyokuwa vinajitokeza, busara na hekima ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameweza kutuongoza sisi pamoja na serikali yake hasa kwa kushirikiana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi. Leo ndipo tulipo hapa katika zaidi ya miaka minane sasa hivi ya uongozi wao tunapata matunda na sote tuna umoja. Leo ukitoka nje amani imetawala tunazungumziwa vizuri wenzetu sasa hivi katika nchi tofauti za Bara la Afrika wanatuongelea kwa mema.

Inawezekana wengine hawasomi magazeti kimataifa au hawaangalii katika mitandao, tunaangalia mengi ambayo yapo ndani mwetu au nchi zetu za majirani, lakini mazuri ambayo tunayosemewa basi haya yapo na tunazidi kung'ara katika Bara la Afrika. Pongezi hizi ziende pia kwa serikali yake kwa pamoja na mashirikiano, pamoja na watendaji wote wa SMZ.

Mhe. Spika, nataka niseme katika mnasaba huo niliosema kwamba wengi tunakuwa tunasahau juzi juzi hapa tulikuwa tuna matatizo ya umeme juu ya madeni tunasemwa kila siku deni lile tunadaiwa na wenzetu wa SMT, lakini sasa hivi kimya huoni kwenye magazeti yanaandikwa kwa sababu fedha zinalipwa. Kwa hiyo hii ni *credit* ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba deni ambalo Zanzibar tulilokuwa tunadaiwa la Muungano kwenye masuala ya umeme na *TANESCO, ZECO* wanalipa na SMZ pia kwa kupitia wizara yenye dhamana wamekuwa wanachangia.

Kwa hiyo, mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu tunawapongeza sana kwa sababu mambo haya pia yana kasoro zake unapokaa na deni muda mrefu mtu anapokudai basi inafika pahala inabidi sasa muanze kunyosheana vidole. Kwa hiyo, mimi namshukuru sana Mhe. Rais na bidii hizi ziendelee katika maeneo yote ili sisi sasa tuwe tunakwenda tunajikaza katika maendeleo. Hata ukiangalia katika eneo la umeme kama utafuatilia katika visiwa vya Pemba ukiangalia mle ndani maeneo mengi sasa hivi ndugu zetu kule wameanza kupata umeme, na ukiangalia katika suala zima la umeme kwa upande wa vijijini vya Zanzibar sasa hivi sisi nafikiri tunakimbilia kwenye asilimia themanini tunakaribia. Unguja na Pemba maeneo yote au vijiji vyote vitakuwa tayari vina umeme inawezekana tukifika 2020 itakuwa ni sehemu chache tena.

Mhe. Spika, sisemi kama mtu kajenga nyumba yake sasa katika shamba lake hana umeme anaweza kuinyooshea mkono serikali, tunaangalia katika shehia na kuwafikia wananchi katika vijiji ambao waliko wengi. Haya ni matunda ambayo ya serikali hii iliyoko madarakani ya Chama cha Mapinduzi. Inawezekana watu hawayaoni haya ndio maana nikasema *when we do good nobody remember, when you do bad nobody forget*, ukijikwaa tu basi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, maneno haya tunataka na wenzetu waliokuwa nje ambao wao maisha siku hizi naona kidogo wametulia inaelekea marafiki zetu au watani wetu wameridhika na inawezekana Chama cha Mapinduzi na serikali hii ndio itakayotawala milele. Maana yake sasa hivi wamesha-*give up* kama unakwenda katika mechi sasa hivi tena umeshafunga magoli. Wenzangu waliotangulia kusema wamesema ingekuwa tayari kama suala la ilani na nilimsikia jana Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mwakilishi mahiri wa Jimbo la Mpendae alisema kwamba kama ni ilani katika sekta ya elimu basi limeshatekelezwa lote na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar. Kwa hiyo, inawezekana kama ingekuwa tunataka twende kwa uchaguzi tuite kila baada ya miaka miwili maana yake kila kitu kinakwenda kwa haraka sasa hivi, ndio maana nikasema Chama cha Mapinduzi inawezekana kikatawala milele hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, lakini pia nataka nigusie katika Sera ya Diaspora tumekuwa tunazungumza yale ambayo tunayoyataka nini wafanyiwe Wazanzibari ambao wanaishi nje ya Tanzania.

Ninapoongea Wazanzibari tunaongelea ndugu zetu kutoka Tanzania Bara pia. Lakini moja ambalo tulikuwa tunalisubiri ni sera kwa sababu sera ndio huko mbele itakuja kuzaa sheria yenyewe pia ili sasa tuweze kujua mpangilio maalum. Lakini na mimi nilitaka niombe kitu kimoja Mhe. Spika, nikupongeze sana Mhe. Spika wewe mwenyewe pia kwa ziara kubwa uliyoifanya katika nchi ya Marekani hivi karibuni kwenda kushiriki katika kikao kile cha Watanzania na kuwaunga mkono na naamini umepata mengi kule na sisi utapata kutuhadithia ili tuendelee na juhudi hizi za kuwasaidia Watanzania wenzetu.

Mhe. Spika, moja katika sera hizi ambazo tunataka tuziangalie ni kuwaunganisha hawa Watanzania wenye jumuiya tofauti walioko nje. Ni kweli kabisa mimi nilimfuata mara moja waziri mwenye dhamana nikamuuliza katika hizi *association* zilizokuwa za Watanzania waliokuwepo ni nje, ni zipi ambazo tayari wameshaungana wote kwa pamoja tukaanza kujua idadi ya Watanzania mahitaji yao. Kwa sababu kuna *random request* zinazokuja utasikia wanataka *visa* waondolewe, wengine wanataka haki ya kuweza kumiliki ardhi, wengine wanataka haki ya kuweza kuishi, lakini lazima wao pia tuwe na kitu kwa ujumla kwa pamoja ili sauti yao iwe *reasonable*. Juhudi ambazo zimechukuliwa na wizara au na serikali leo kuwaalika hapa kuja kushiriki na kutuunga mkono katika hotuba ya bajeti ni mwanzo mzuri sana kwa sababu zamani tulikuwa hatuwajui viongozi wao katika masuala ya Diaspora tunasikia wapo tunawaona lakini mara nyingi wanakuwa ndio wale wale ambao wanajitokeza.

Mhe. Spika: Bado dakika tatu Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwa hiyo hawa ni vizuri katika suala hili zima tukaendelea kubakia nao na tukaweza kuwaunga mkono. Lakini katika hili la Diaspora kwenye sera hizi mikutano ile ya kimataifa inayofanyika Zanzibar wigo wake uzidi kupanuka zaidi na katika mpango mzima ambao uliofanya katika wanapokuja hapa kuonana na mabenki wazidi kupanua na kushirikisha pia benki ambazo zipo Tanzania Bara na wenzetu kutoka Bara pia washiriki kwa wingi zaidi ili twende sambamba na wenzetu kutoka Tanzania Bara.

Mhe. Spika, nimalizie kwa jambo ndogo tu ambalo nahisi lina umuhimu wake. Nikiangalia Ofisi ya Mhe. Rais ambayo ni ile Ikulu ya Zanzibar ambayo ipo mjini pale, lile jengo ni la kihistoria lilijengwa mwaka 1903, lakini ni jengo ambalo pia sambamba lipo mbele ya Ubolozi wa Urusi lililokuwa zamani ni majengo ya historia. Kwa bahati nzuri au mbaya ile nje imefungwa, bado watu wengi wageni huwa wanapenda kupita maeneo yale kutaka kupiga picha kutokana na historia, hasa sasa hivi tunaanza kupokea wageni kutoka Urusi wanakuja pia Zanzibar na lile jengo lao liko pale. Sasa iwe wazi kama haparuhusiwi kupiga picha ni eneo gani wanaweza kupiga picha, na kama wale ma-*tour guide*s watakuwa wanawapeleka pale kuwaonesha yale majengo na historia basi pajulikane ni eneo gani wanaweza kusimama ili pasitokee na sintofahamu yoyote na pakawa hapapendezi hasa kwa wetu wanaosimamia masuala ya ulinzi na usalama wa jengo husika.

Mhe. Spika, baada ya hapo nichukue nafasi hii kukushukuru wewe na Wajumbe wa Baraza lako kwa kunisikiliza. Niseme tu nampongeza Mwenyekiti aliyesoma hotuba kwa niaba ya Kamati, nimpongeze Mhe. Waziri na niseme kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunguu naunga mkono hoja mia juu ya mia, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Simai. Waheshimiwa Wajumbe sasa atachangia Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil atafuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Hamza Hassan Juma ajiandae.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii katika kuchangia hotuba hii iliyo mbele yetu. Kwa hakika Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza sana wizara hii namna ya walivyojiandaa kitaalam na kinukta katika bajeti hii. Nisije nikakosea naomba nitangulize rasmi kwamba mimi naiunga mkono bajeti hii asilimia mia moja imefanya vizuri.

Mhe. Spika, mchango wangu mimi utajikita katika kurasa mbili, ukurasa wa 38 na 39 Kitengo cha Habari. Mhe. Spika, hiki ni kitengo muhimu sana kwa namna moja au nyengine kinafaa kipewe uwezo zaidi, huu uwezo uliopewa sasa hivi ni mdogo, wawe na *cameras* na wawe wanarusha matangazo yao kila baada ya muda. Kwa hakika tukijifunza kwa wenzetu mbali ya kuwa sasa hivi wana *brochures* au vipeperushi ambavyo wanavileta mpaka Barazani kuelezea mafanikio ya nchi yetu na serikali yetu kwamba wawe na utaratibu wa kila siku kutangaza mafanikio na maendeleo yanayopatikana, serikali namna ilivyojipanga ili kusudi mwananchi aelewe leo na kesho na kesho kutwa.

Mhe. Spika, ukitembelea nchi za wenzetu kwa mfano Falme za Kiarabu kila nukta wanapopata katika televisheni ya taifa wanakuwa wanatia maelezo ya mafanikio ya nchi yao na viongozi wao. Kwa hiyo, kwa upande wetu kitengo hiki kipewe neno zaidi na wakati zaidi na uwezo zaidi kama bajeti yao iko hapo basi zaidi izidishwe. Nashuhudia kila mara kiongozi wetu akitwambia kwamba mafanikio tunayoyafanya tuyatangaze, kwa hiyo kitengo kinafaa zaidi kiyatangaze mafanikio ya Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi muda wote ili wananchi waelewe na waridhike hasa kama nchi inakwenda mbele maendeleo ni hatua kutoka hapa kwenda hapa.

Kwa hiyo, waendelee zaidi kitengo hiki kipewe uwezo na nguvu zaidi kusudi mawasiliano yaendelee kila siku na wawe wanapenyeza katika redio na televisheni yetu maendeleo yanayopatikana ambayo yanaonekana wazi. Nampongeza sana Rais Dkt. Ali Mohamed Shein namna anavyotufanyia maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, la pili upande wa hawa wenzetu wa Diaspora kwa kweli ni watu muhimu sana. Ukiangalia katika nchi za wenzetu nimesoma takwimu kwamba nchi ya Nigeria wanachangia uchumi wao kwa asilimia kubwa hawa Diaspora na nchi ya Kenya hivyo hivyo wanachangia uchumi wa nchi zao kwa asilimia kubwa. Kwa hiyo katika kuwatambua mbali ya makongamano yenye kuendelea lakini wapewe elimu ya kutosha namna wanavyoweza kusaidia uchumi wa nchi yetu. Wengine wanajua tu wanakusanya mizigo yao, makontena yao wasaidie katika sekta za elimu, lakini *at the end of the day* wanakwama kwa sababu ya kukiuka taratibu.

Kwa hiyo katika semina zinazofanywa mbali ya kuwatambua na kujitambua na kuwajua lakini pawe na elimu rasmi itolewe *Comrade* Issa Haji Ussi (Gavu) kwamba wawe wanajua *procedure* gani wanaweza wakatumia wakati wanaleta misaada katika nchi yetu wengi tu wapo. Nakumbuka miongoni mwa ziara moja ya Marekani na mimi kidogo bahati nilishiriki Mhe. Balozi Seif Ali Iddi aliwaambia haya yafuatayo: "Mkataa kwao ni Mtumwa" na wakathibitisha sisi bado ni wa kwetu na wapo tayari kusaidia uchumi wa nchi yetu, lakini taaluma ipite namna gani ya kusaidia uchumi wa nchi yao kama takwimu ilivyotoa za Nigeria na Kenya.

Mhe. Spika, kwa hayo machache mimi kama mwanzo nilitanguliza naikubali bajeti hii na kitabu hichi na nawapongeza watendaji wote namna walivyoiandaa nukta kwa nukta na uelewa mkubwa. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Ahmada kwa mchango wako. Naomba sasa nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi atafuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Shaib Said Ali ajiandae.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuichangia hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
Mhe. Spika, nichukue fursa hii kwanza kuipongeza sana hotuba hii ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa vile ilivyopangika kurasa kwa kurasa, nukta kwa nukta kama walivyotangulia kusema wenzangu. Lakini nimshukuru na nimpongeze sana mwasilishaji Mhe. Issa Haji Ussi wa ofisi hii kwa umahiri wake wa uwasilishaji. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nichukue fursa hii niipongeze sana Kamati inayoshughulikia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nao kwa kuweza kufafanua ripoti yao yenye mnasaba wa kuunga mkono ripoti hii ya bajeti. Lakini niwapongeze wote ambao wamenitangulia kwa michango yao mbali mbali katika kuiunga mkono.

Mhe. Spika, nianze michango yangu kwa kuchukua fursa pekee ya kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi mbali mbali na usimamizi wake wa majukumu katika kusimamia maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Rais wetu ni Rais msikivu, ni Rais mbunifu na ni Rais ambaye kila mara msisitizo wake ni watu kufanya kazi na kwa maana hiyo kila mara hupenda kuweza kutathmini shughuli mbali mbali zinazofanywa na watendaji wake katika Wizara mbali mbali.

Mhe. Spika, kwenye hotuba hii kwa kweli nimefurahishwa sana na Ofisi hii ya Rais kuweza kuanzisha Kitengo cha Tathmini ya Utendaji Kazi wa Taasisi za Umma.

Mhe. Spika, aliyetoa wazo hili la kuanzisha kitengo hiki katika Ofisi ya Rais kwa kweli tumpongeze sana na inawezekana nichukue fursa hii kuwapongeza wafanyakazi na watendaji katika Ofisi ya Rais na wale wanaomshauri katika mambo mbali mbali.

Mhe. Spika, Kitengo cha Tathmini ni moja kati ya kitengo muhimu sana na tunakumbuka kwamba Mhe. Rais hata alipoingia madarakani alikuwa na usemi mmoja kwamba "Tuache kufanya kazi za mazowea *(business as usually)".* Sasa kuanzishwa kwa kitengo hichi mimi nina imani sana kitamsaidia Mhe. Rais katika kutathmini utendaji kazi wa taasisi za serikali kuelewa ufanisi na changamoto, vile vile jinsi wafanyakazi wa taasisi ya serikali wanavyowajibika, lakini kuweza kujenga na kuimarisha nidhamu katika sehemu mbali mbali za sekta hizi za serikali.

Mhe. Spika, kitengo hiki najua ni kipya na inawezekana hakijaimarika vizuri, lakini niiombe sana serikali kupitia Ofisi ya Rais kuweza kukiimarisha vizuri kitengo hiki kwa kuweza kuona kwamba kina wafanyakazi wa kutosha lakini walio mahiri na wenye ujuzi na uweledi katika masuala mazima ya kufuatilia na kufanya tathmini katika utendaji wa kazi za serikali. Hii inaweza ikawa ni mafanikio makubwa na yenye kuhimiza utendaji katika taasisi zetu za serikali.

Mhe. Spika, lakini pamoja na hilo niliona katika bajeti iliyopita kwamba kitengo hichi kilipata fedha kwa asilimia 52, sasa mimi nafikiri kutokana na umuhimu wa kitengo hichi basi kwa bajeti hii kuweza kukitazama vyema. Kwa sababu kama tunataka kukiimarisha basi tuweze kuongeza hali hii ya bajeti ili ilingane na vitengo vyengine kutokana na umuhimu wake.

Mhe. Spika, nikitoka katika eneo hilo sasa nije katika ukurasa wa 81 wa bajeti hii ambapo inaelezea juu ya mafunzo ambayo yametolewa na Ofisi ya Rais juu ya utunzaji na udhibiti wa siri za serikali.

Mhe. Spika, kitendo cha Ofisi ya Rais kuweza kutoa mafunzo kwa wafanyakazi 525 wa serikali juu ya suala zima la utunzaji na udhibiti wa siri za serikali kwa kweli mimi naipongeza sana ofisi hii. Mhe. Spika, ni ukweli kwamba kwa kipindi kirefu sana taasisi mbali mbali za serikali zilikosa utunzaji na udhibiti wa siri zake. Kwa hiyo, kwa Ofisi ya Rais kuweza kuliona hili na kuweza kuanza kutoa mafunzo kwa wafanyakazi mbali mbali wa serikali juu ya suala zima la utunzaji na udhibiti wa siri kwa kweli hii itasaidia sana. Wakati mwingi si ajabu ukakuta baadhi ya maamuzi hayajatolewa katika ngazi za chini basi ukayasikia yapo mitaani yanazungumzwa na watendaji na wananchi wa kawaida, hii inaikosesha serikali siri zake kuweza kutunzwa na kudhibitiwa vizuri. Kwa hivyo, niipongeze sana Ofisi ya Rais lakini hapa isiwe mwisho katika utoaji wa mafunzo kwa sababu taasisi za serikali ni nyingi, kwa hiyo niiombe sana Ofisi ya Rais kuweza kuendelea kutoa mafunzo yahusianayo na utunzaji na udhibiti wa siri za serikali.

Mhe. Spika, hivi sasa kwa ufupi tuna tatizo kubwa sana la uzalendo na moyo wa kujitolea katika taifa letu. Kwa hiyo, pamoja na mafunzo ya aina hii ya utunzaji na udhibiti wa siri za serikali, nafikiri vile vile umefika wakati wa kuweza kuliangalia eneo hili jengine la

kuweza kurejesha suala zima la uzalendo na moyo wa kujitolea kwa wananchi wetu ili tuweze kupiga maendeleo zaidi katika nyanja mbali mbali za kiuchumi na za kijamii.

Mhe. Spika, nikiondoka katika suala hilo la mafunzo sasa nije katika programu ya kusimamia huduma na shughuli za Mhe. Rais na kuimarisha mawasiliano ya Ikulu. Mhe. Spika, katika kitabu hiki cha bajeti tumeelezwa kwamba kuna mafanikio makubwa katika kuzisemea shughuli mbali mbali za Mhe. Rais anazozifanya kupitia kitengo hiki cha mawasiliano ya Ikulu. Mhe. Spika, mimi nipongeze sana juhudi za kitengo hiki katika kuwasilisha kwa wananchi shughuli au kazi mbali mbali ambazo anazifanya Mhe. Rais zile za ndani ya nchi, lakini hata zile za nje ya nchi. Kwa kweli tumeshuhudia tofauti iliyopo kati ya kipindi cha nyuma na hivi sasa, hivi sasa shughuli mbali mbali zinazofanywa na Mhe. Rais basi zinaonekana kwa muda mfupi sana au zinazisikika kwa muda mfupi sana. Kwa kweli wananchi wameweza kujenga imani na Rais wao juu ya utendaji kazi wake kwa sababu yale anayoyafanya basi wanayaona kwa muda mfupi kwa kupitia nyanja mbali mbali zikiwemo za majarida, vipindi vya redio na televisheni, mitandao ya kijamii vile vile na magazeti.

Kwa hiyo, niombe tu kwamba inawezekana bado nakala za majarida zinazotolewa zikawa ni chache zinawafikia pengine wafanyakazi zaidi wa serikali na wale walioko maofisini. Kwa hiyo, niombe tu ikiwezekana kuweza kuongeza idadi ya nakala za majarida na magazeti ili ziwafikie wale wananchi ambao wako vijijini ili kuweza kuona shughuli mbali mbali zinazofanywa na Mhe. Rais, vile vile pamoja na watendaji wake.

Mhe. Spika, sasa nije katika ziara anazozifanya Rais zile za nje na ndani ya nchi. Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Rais kwa ziara mbali mbali anazozifanya zile za ndani na nje ya nchi, kwa kweli ziara hizi zina tija sana kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mfano, zile alizozifanya Arabuni tumeweza kuziona *live* katika vyombo vya habari. Kwa hiyo, anafanya juhudi za kila aina kuweza kuona Zanzibar…

Mhe. Spika: Bado dakika tatu mheshimiwa.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Inasogea katika maendeleo ya nyanja mbali mbali. Niombe tu pale ambapo Mhe. Rais anaona kuna nafasi, basi hata wale Waheshimiwa Wawakilishi wa majimbo anaweza kumchukua mmoja mmoja ili na wao waweze kwenda kujifunza baadhi ya mambo ambayo yanaweza kuleta tija katika majimbo yao.

Mhe. Spika, kutokana na tatizo la muda na nisije nikasahau kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Magomeni natoa shukrani sana kwa Mhe. Rais kwa ule mradi wa *ZUSP* ambao unaendelea katika jimbo langu na nina imani kwamba ukimalizika basi utakuwa umeondosha tatizo kubwa sana la kutuama kwa maji ya mvua katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Spika, nishukuru tena uongozi wote wa Ofisi ya Rais, lakini niwapongeze wajumbe wote ambao wamechangia na niwaombe wale ambao hawajachangia basi wachangie na kuweza kuunga mkono hotuba hii. Mimi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa

mia ili tuweze kuwapa nafasi watendaji wa Ofisi ya Rais kuweza kutekeleza haya ambayo wameyapanga. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Rashid Makame Shamsi, naomba sasa nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma atafuatiwa na Mhe. Shaib Said Ali na Mhe. Suleiman Sarahan Said ajiandae.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, mimi kwa upande wangu nataka niungane na wenzangu kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kutuletea hotuba yake hii ya bajeti ambayo kwa kweli kama walivyosema wenzangu kitabu kimetulia na kimeandikika vizuri, natania tu kidogo hii rangi angalau na weupe weupe japo kidogo ungelikuwemo. Mhe. Spika, kimsingi tunampongeza sana Mhe. Rais kwa kazi zake na kama walivyosema wenzangu kibinafsi kama Mhe. Rais ukiacha utendaji wa shughuli zake kwa kweli hatujawahi kuona wala kusikia dosari lake katika utendaji. Kwa hiyo, tunampongeza sana na tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie mpaka atakapomkabidhi kijiti mwanachama mwenzake wa CCM 2020 basi aendelee kuwa safi wala lisije likatokezea doa lolote, na Mwenyezi Mungu ampe afya njema.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme mambo machache sana katika hotuba hii, kwa sababu kama nilivyosema kwamba mambo mengi yapo vizuri na yapo sawa. Isipokuwa kuna mambo matatu tu muhimu nitamuomba Mhe. Waziri haya ili nisije nikamchafulia bajeti yake kwa kupiga buti. Ninaamini atanisikiliza vizuri na ninaamini atanipa jawabu ambayo itakayoridhisha moyo wangu, vile vile na wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo, pia na wananchi wa majimbo mengine ambao walinituma niwasemee mambo yao.

Mhe. Spika, kwanza nataka nianze na shukrani ndani ya jimbo langu. Hili nimelisema tangu mwaka jana sina budi kuendelea tena kusema, lakini mwaka huu inabidi nishukuru zaidi na hapa nitawachanganya pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, wewe kabla ya kuwa Spika uliwahi kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni, lakini baadae ukaja ukawa Mbunge wa Jimbo la Kwamtipura ambapo nashukuru sana tulifanya kazi kwa pamoja vizuri sana. Wakati ukiwa Mhe. Mbunge wa Jimbo la Chumbuni kutokana na kadhia ya wananchi wetu wa Jimbo la Kwamtipura kipindi kile ambayo sasa hivi ni Shaurimoyo pamoja na wananchi wa Jimbo la Chumbuni. Baada ya kuona kadhia kwamba kila zinaponyesha mvua kubwa wananchi wetu wanapata tabu, wanazama na nyumba zao inabidi wakati wa mvua wahame ikimaliza mvua warudi kutokana na mtaro ambao umepita kati kati uliogawa jimbo letu la Shaurimoyo kwa kipindi kile ilikuwa inaitwa Kwamtipura, na Jimbo la Chumbuni ambalo wewe Mhe. Spika sasa hivi ulikuwa ndio Mwakilishi pamoja na Mbunge alikuwa Mhe. Zahor na mimi Mbunge wangu alikuwa Mhe. Yussuf Kombo. Tulikaa pamoja kama utakumbuka katika Skuli ya Chekechea ya Saateni, tukakaa tukawaita wataalam wa Manispaa tukajadili ni namna gani tutaweza kuwasaidia wananchi wetu kuondokana na kadhia ya mvua masika zinavyokuja tutawaokoa vipi wananchi wetu.

Mhe. Spika, tuliwapa kazi watu wa Manispaa vile vile tukawashirikisha na watu wa Wizara ya Fedha na nyinyi ambao watu wa Chumbuni pamoja na sisi watu wa Kwamtipura, tukakubaliana tuchange fedha iandikwe mradi kwa ajili ya kupeleka Manispaa ili kuhakikisha kwamba tunaupeleka serikalini kuhakikisha kwamba mtaro ule unajengwa.

Mhe. Spika, kama utakumbuka kipindi hicho ilikuwa kwenye mwaka 2002 kama sikosei, kwa kweli mradi ule umekwenda serikalini kwa bahati nzuri serikali wakauchukua ukafanyiwa kazi kwa muda mrefu sana, lakini katika kipindi chote mradi ule ulishindwa kutekelezeka. Nimekuwa nikiendelea kupiga debe hapa Barazani na katika kampeni za uchaguzi wa mwaka 2015 Mhe. Rais nilimuona mimi mwenyewe nikazungumza kadhia za jimboni, vile vile kadhia za pamoja na Jimbo la Amani ambapo Mwakilishi wake hapa ananiangalia. Aliniahidi kwamba mheshimiwa usiwe na wasi wasi mimi nimejipanga na ninakuahidi suala la mtaro wa Jimbo la Shaurimoyo pamoja na Jimbo la Chumbuni utakuwa historia.

Mhe. Spika, nakuthibitishia na kwa bahati nzuri bado na wewe kwa upande mmoja bado unaishi ndani ya Jimbo la Shaurimoyo. Mhe. Spika, miaka yote hiyo inaponyesha mvua za masika hapa kelele zangu zinakuwa kubwa sana namkamata Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa ambapo Manispaa wapo chini yake na tukafika pahala akaniahidi, akasema wewe Mtumbatu wa chini mimi Mtumbatu wa juu nakuahidi mtaro tutaujenga. Mhe. Spika, nasema kwa kinywa kipana na wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo wamenituma nije niseme salamu hizi, miaka yote tunapiga kelele mafuriko, mafuriko, mafuriko. Kwa mwaka huu Mhe. Spika, mvua zote za masika zimenyesha maji yamekwenda zake baharini hakuna mwananchi wangu aliyezama. Kwa kweli kama sikutoa shukurani basi nadhani leo nisingeweza kurudi nyumbani ningechezea bakora kabla sijafika nyumbani. *(Makofi)*
Tunashukuru sana mtaro ule sasa hivi naweza nikasema kwa asilimia karibu 95 tayari umekamilika kazi zilizobakia ni ndogo ndogo za *finishing* na nitamsubiri Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa wakati atakapokuja nitajaribu kumchomekea majukumu yanayomhusu yeye kujaribu kuangalia vile vivuko vya zamani, vile vile yale maeneo ambayo pembeni pembeni kabla ule mradi kukamilika utiwe kifusi kidogo kwa sababu maji yanakuwa yanarudi katika nyumba za wananchi watu wanapata tabu. Mhe. Spika, kimsingi Mhe. Rais ametuokoa sana wananchi wa Jimbo la Shaurimoyo pamoja na Jimbo la Chumbuni sasa hivi hatuzami tena. Kero tu niliyoipata safari hii maana yake ilikuwa Sheha wa Shaurimoyo kila zikinyesha mvua lazima anipigie simu mheshimiwa tunazama, lakini safari hii kero aliyonipigia simu kanambia mheshimiwa mvua hizi bado tunapata tabu ya maradhi yaliyoingia maarufu yanaitwa maradhi ya "Muungano" lakini sio tena mtaro. Hili kwa kweli tunawapongeza sana.

Mhe. Spika, vile vile hili ndio maana nikasema kuna mambo matatu nitamuomba sana Mhe. Waziri anisikilize vizuri ili nisije nikaichafua hii bajeti yetu, na kuichafua kwenyewe kupiga buti kwa kutaka ufafanuzi wa ziada.

Mhe. Spika, katika ziara ya Mhe. Rais aliyokuwa anaifanya kipindi hiki, ile ziara ya kichama alipita katika Wilaya zetu mbali mbali na tunamshukuru alipokuja katika Wilaya yetu ya Amani Waswahili wanasema "Mgeni njoo mwenyeji apone".

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri katika ziara ile sisi wawakilishi hatukupata nafasi ya kusema chochote, lakini nashukuru sana viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Amani kupitia kwa Mwenyekiti wetu Mhe. Mrope alitamka kilio cha wananchi wa Jimbo la Shaurimoyo na Jimbo la Amani. Pale akamdokeza Mhe. Rais kwamba moja katika kero yetu ambayo ilikuwa ni muongozo wa Naibu Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti wetu alieleza kwamba Mhe. Rais amekuja kusikiliza changamoto ili tuzitekeleze kwa sababu ilani ya uchaguzi inasema sio tupige maneno tu, tupige kazi wananchi waione ili mwaka 2020 basi sisi kazi yetu iyena iyena tu. Kila pahala tukipita tunasema tumefanya hivi, tumefanya hivi iyena iyena watu wanatumiminia kura tunakwenda zetu mbele.

Kwa hiyo, katika mkutano ule kwa bahati mbaya Mhe. Waziri sikukuona nilifikiri labda katika ziara za Mhe. Rais kila pahala anapokwenda ungelikuwepo, lakini naamini maafisa wako hasa Idara ya Uratibu walikuwepo. Sasa hapa nakuja na suala Mhe. Rais pale alimwambia Mwenyekiti wetu wa CCM wa Wilaya ya Amani Mhe. Mrope, akamwambia suala la barabara ya Saateni, Mboriborini mpaka Darajabovu hiyo barabara imeshakuwa kila siku inasemwa, na akasema mimi huwa sipendi kwamba kila siku likawa linazungumzwa jambo hilo kwa hilo. Isipokuwa sasa nakuuliza tu Mhe. Waziri sijui salamu hizo ulizipata na Mhe. Rais alisema atamuagiza Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Dkt. Sira Ubwa Mamboya. Sasa mimi ninavyojua katika ziara za Mhe. Rais kunakuwa kuna waratibu ambao baadae wanakupa ripoti zote ili sasa yale maagizo na miongozo aliyoitoa uwaandikie mawaziri husika kwa ajili ya utekelezaji. Kwa hiyo, ndio maana nikasema kwamba nijaribu kuulizia suala hili kama Mhe. Waziri umeshalipata na kama umelipata umechukua hatua gani.

Mhe. Spika, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi juzi nimepitisha bajeti ya Wizara ya Mawasiliano nilivyoangalia katika programu zile za Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara sikuiona barabara ya Saateni, Mboririni, Amani na Darajabovu nikaona kama kitu hakikuingizwa kwenye bajeti, vile vile utendaji wetu wa serikali unaangalia bajeti na maagizo ya viongozi wakuu. Sasa hili ndio swali langu moja nililokuwa nataka niulize tu kama hii taarifa wameshakuwa nayo na tunategemea wananchi wetu tutawaambia vipi katika kadhia ya barabara yetu ya Shaurimoyo/Mboriborini hadi Darajabovu.

Jengine kuna kero ya wananchi wa Makangale. Wananchi wa Makangale juzi walikuja baadhi ya wajumbe wao na miongoni mwa watu waliwaona na mimi waliniona, wakaeleza kwamba kuna kadhia yao katika ule Msitu wa Ngezi.

Mhe. Spika: Bado dakika tatu Mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sawa ahsante Mheshimiwa nafikiri zinanitosha hizo. Katika ule Msitu wa Ngezi pale ni kwamba lile eneo lilikuwa lina mgogoro, Mhe. Rais

akatoa agizo eneo likapimwe ili lijulikane eneo la msitu ni eneo gani na eneo la wananchi ni eneo gani. Kwa bahati nzuri Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati naishukuru eneo lile wamelipima na ramani ipo na wale wananchi wakawa wanaendelea kudai haki yao.

Kulikuwa kuna mgogoro kidogo walikwenda mpaka mahakamani na mahakamani wakashinda wakaambiwa aidha walipwe fidia na mambo mengine. Lakini kikubwa ambacho walichokuwa wanakidai wao kwamba siku zimeshakuwa nyingi na wanasema sisi au wao serikali wana program, wana *vision 2022*, wana MKUZA, wana *PBB*, lakini wao wananchi MKUZA wao, rasilimali yao na wenzetu Jamhuri ya Muungano kule wamepitisha sheria ya kurasimisha rasilimali za wananchi, yaani kule wanaita MKURABITA.

Wenzetu kule kuna mpaka hati za kimila, kule kama hujapimiwa ardhi kuna hati za kimila, hati ile ukienda nayo benki unaweza ukaikopea kwa ajili ya kuendeleza shamba lako kwa ajili ya kilimo au kwa mambo mengine, lakini wananchi hawa mpaka sasa hivi hakuna *document* yoyote kutoka serikalini waliyoishika, bado wanaendelea kuhangaika. Sasa na hili nadhani Mhe. Waziri naomba alitafutie taarifa za kutosha ili aweze kutujibu na wananchi wetu waridhike.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa ili niitendee haki bajeti yako siwezi nikenda tu nikazungumza maneno bila ya kuingia kwenye mafungu. Mimi nimejaribu kuangalia ukurasa wa 19 katika Idara ya Uratibu na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mhe. Spika, kwa kweli moja katika changamoto ambayo mimi ninaihisi changamoto hii ipo kwa muda mrefu ushiriki wa wataalam wetu katika mikutano ya kimataifa. Tunaona mawaziri wetu wanakwenda wakati mwengine katika mikutano hii hasa ya mashirikiano ya kikanda na kuna baadhi ya miradi tunatakiwa kwanza tupeleke wataalam katika hatua ya awali halafu baadae najua mawaziri wao wanakwenda kwa ajili ya kuweka saini. Lakini tatizo lililojitokeza mara nyingi inajitokeza katika vile vikao vya wataalam watendaji mbali mbali katika serikali wanakuwa wakati mwengine katika wizara zao pengine fedha hazijaingizwa, *OC* inakuwa hakuna. Kwa hivyo, tunashindwa kupeleka wataalam katika vikao vya kikanda matokeo yake kuna mambo na kuna miradi ambayo inahusu Zanzibar tunashindwa kui-*present* kwa wakati ili ikaja ikaweza kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Namalizia dakika moja tu Mheshimiwa. Sasa nimejaribu kuangalia fungu hili mwaka uliopita tulipitisha shilingi 508 milioni, lakini *still* katika pesa hizo zikapatikana kama shilingi 300 milioni na kidogo hivi. Sasa Mheshimiwa kitu ambacho nakishauri kwamba fungu hili ni vyema, kwa bajeti hii najua zote zimeshapangwa, lakini naomba katika bajeti inayokuja tuangalie fungu hili liongezwe ili sasa kwa zile idara nyengine wale wataalam wanaotakiwa kwenda kama katika sekta zao hakuna fedha za kutosha Idara hii ya Ushirikiano wa Kimataifa iweze kuhakikisha kwamba wataalam wale wanafika katika maeneo hayo. Mwaka huu vile vile imetengewa kama shilingi milioni mia tano na thalathini na kitu hivi.

Kwa hivyo, naamini Mhe. Waziri amenifahamu atakuja kuweza kunitolea ufafanuzi kimsingi. Mhe. Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 95 mpaka yale majibu yangu nitakapopatiwa kwa usahihi. Ahsante sana.

Mhe. Shaib Said Ali: Mhe. Spika ahsante sana, awali ya yote kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa na kutekeleza wajibu wetu huu tuliopangiwa na wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya hapo nimshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutuletea hotuba hii ambayo ndani yake ina ufanisi na mwelekeo kabisa wa shughuli za kisiasa.

Mhe. Spika, baada ya kutoa shukrani zangu hizo pia nimshukuru tena Afisa Mdhamini wa Afisi hii Pemba kwa juhudi zake anazochukua na kuimarisha wizara hii.

Mhe. Spika, sasa niende katika mchango wangu na kwanza baada ya kukiangalia kitabu hiki nimepata masikitiko kidogo na namuomba Mhe. Waziri kama kuna ufafanuzi anisaidie la kama ni kimya basi, sisemi nitapiga buti. Katika kitabu hiki kilichopangwa ni kwamba kuna vifungu ambavyo vina upungufu wa fedha katika mwaka uliopita.

Mhe. Spika, hii ni Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Rais ambaye ametekeleza ilani kwa vitendo hakuitekeleza kwa maneno. Sasa leo katika vifungu vyake au katika ofisi yake kuwa kuna vifungu ambavyo havikutimia fedha tutamlaumu mtu ambaye anataka kufanya kazi, lakini kumbe ni sisi hatukutimiza wajibu wetu. Mimi nimuombe Waziri wa Fedha kwa dhati kabisa kwamba kuna ule msemo usemao kwamba "Kata pua uunge wajihi", basi nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha kwamba akate pua aunge wajihi lakini kwa mwaka 2018 na 2019 fedha hizi katika Ofisi ya Rais zikamilike ili Mhe. Rais aweze kufanya kazi zake kwa vile ambavyo amepangiwa.

Mhe. Spika, baada ya hapo sasa nije katika ahadi za Mhe. Rais. Mhe. Spika, wajumbe wote waliochangia kipengele hiki wamesifu kwamba Mhe. Rais ametekeleza kwa asilimia 99 ahadi zake. Mimi nasema kwa Mheshimiwa ni kweli kabisa kwa sababu katika jimbo ambalo lilikuwa na matatizo ni jimbo langu la Chonga hasa katika kijiji cha Ngomeni. Katika kijiji cha Ngomeni kulikuwa hakuna barabara, hakuna maji, hakuna skuli, kulikuwa hakuna kituo cha afya. Lakini kutokana na juhudi za Mhe. Rais na kutekeleza ilani zake hizi masuala yote haya ameyatekeleza kwa asilimia mia moja katika kijiji kile cha Ngomeni. Kwa hivyo, mimi nampongeza kwa dhati kabisa na hii ndio kazi ambayo anatakiwa Mhe. Rais aitekeleze.

Mhe. Spika, kuna bwana mmoja alisema kwamba ataigeuza Zanzibar kuwa Singapore lakini hii nchi haitaki maneno inataka vitendo. Kwa hivyo, Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein alishirikiana na Makamu wake wa Rais wameitekeleza kwa vitendo Ilani ya Chama cha Mapinduzi na hivi sasa ukienda Pemba kunang'ara kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninaloliomba zile ahadi ambazo amezisema Mhe. Rais niwaombe mawaziri na maafisa ambao wanashughulikia suala hili basi walitekeleze. Kwa sababu tunataka

mwaka 2020 zile ahadi ambazo tumeziweka zote katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ziwe zimeshatekelezwa na pasiwe tena na maneno ya kusema kwamba kijiji hakina maji, hakina skuli, hapana kituo cha afya hilo lipungue, ndio maana jana katika uchangiaji wetu wakati tunachangia hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais tulizungumza kwamba yule bwana kule asituchokonowe. Kwa sababu tayari mengi tumeshayatekeleza, asiwape mwanya wale watu ambao mwaka 2020 watapata la kusema.

Nikiondoka hapo Mheshimiwa nije katika ziara za Mhe. Rais. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Rais kwa jinsi anavyotekeleza ziara zake. Mhe. Rais anatekeleza ziara hizi akiamini kwamba kukaa ofisini sio kazi, kazi ni kutembelea wananchi na kumuona anavyotekeleza yale ambayo ana wajibu kuyafanya. Tunaomba Mheshimiwa hususan kwa wawakilishi wa Pemba zile ziara zinapofanyika za Mhe. Rais tualikwe rasmi na tutambuliwe rasmi sio kualikwa tu, tutambuliwe rasmi kwamba hawa wanaokuja pale ni wawakilishi.

Mhe. Spika, kuna mifano kadhaa ambayo tunapokwenda katika ziara za Mhe. Rais wawakilishi huwa hatuna ile hadhi ya uwakilishi kama kweli pale tumefuatana na Mhe. Rais. Mfano mzuri tulipokwenda kumpokea Mhe. Rais katika kufungua jengo la Mahakama ya Chake Chake, Pemba pale; Mhe. Rais tulianza kumpokea uwanja wa ndege lakini tukaambiwa kwamba hapa Waheshimiwa Wawakilishi hawatakiwi. Tukarudi tukaenda katika jengo la Mahakama kumsubiri kwamba pale anapofungua na sisi wawakilishi tuwepo, lakini pia tulipofika pale tukaambiwa kwamba hapa wawakilishi hawatakiwi, tukafika katika uwanja wa *tennis* pale kumngoja kabisa lakini Mheshimiwa tulichanganyika na wananchi hata wawakilishi hatukutambulika kama pale tupo na badala yake ndio tukaitwa Ikulu tukenda tukakaa na kadhalika.

Mimi niombe tu kwamba Mhe. Rais anapofanya ziara zake hizi tualikwe na tutambuliwe na basi afanye kama mwenzake Mhe. John Joseph Magufuli anapotembea na wabunge atupe angalau fursa pale anapokuwepo yeye na sisi tupate kuzungumza na wananchi sote tutatambulika.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije katika vyombo vya habari. Kwanza nivipongeze sana vyombo vya habari, vinafanya kazi kubwa sana kutangaza ilani na mambo yetu tunayoyafanya. Lakini kuna baadhi ya vyombo vya habari bado sijui vina mtazamo gani.

Jana Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame hapa alituletea Gazeti la *Citizen* akasema kwamba gazeti lile lina ukurasa ambao kuna bwana mkubwa anaiponda Zanzibar kwamba hakuna kilichofanyika na akasema kabisa basi uliokuwepo Zanzibar ni umaskini zaidi. Mimi simlaumu yule bwana mkubwa namlaumu yule mwenye gazeti kwa sababu yeye ndie aliyekwenda akachukua zile ripoti na ingelikuwa hataki kuziandika ripoti zile angelimkatalia yule bwana mkubwa kuandika ripoti zake kwa sababu yeye ndie mhariri wa gazeti lile pale. Kwa hivyo, vyombo hivi vipo Mheshimiwa. Kuna mitandao ya kijamii bado wanamtukana Rais kabisa kabisa, unapofungua mitandao mingine Mhe. Spika, utaona imani kabisa kwa jinsi yale maneno wanavyoyazungumza. Kwa hivyo, naomba kabisa baadhi ya vyombo vya habari vingi sana karibu asilimia 80 vinafanya kazi yao nzuri sana vikiongozwa na chombo chetu kitukufu cha *ZBC*.

Mhe. Spika, nasema kuna vyombo hivi ambavyo bado vinatuponda na vinatukanyaga na hususan viongozi wetu wa ngazi za juu. Kwa hivyo, vyombo hivi vichunguzwe ili masuala haya yasiendelee tena.

Nikiondoka hapo nije katika kuimarisha usalama kwa watumishi wa serikali na maeneo wanayofanya kazi. Mhe. Spika, kitengo hiki nakiomba kifanye kazi. Mimi nina mfanyakazi wangu na mpiga kura wangu tulipokuwa katika masuala yetu haya ya kampeni yumo katika kazi alianguka na pikipiki lakini mpaka leo mfanyakazi yule kila anapoomba na masuala yote anayo lakini bado hajafanyiwa mpango wowote. Kwa hivyo, kuwepo kitengo hiki nashukuru sana kwamba Mhe. Naibu hapa anasema atamlipa. Kwa hivyo, naamini kwamba kuwepo kwa kitengo hiki naamini kuwa wale wafanyakazi ambao watapata athari katika kazi basi watapata masuala hayo.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije katika masuala ya mafunzo ya utunzaji wa siri za serikali. Mhe. Rashid Makame Shamsi pale alizungumzia kidogo, lakini mimi nasema tena na natilia mkazo kwamba bado kuna wafanyakazi ambao si waaminifu na wanatoa siri za serikali nje.

Mhe. Spika, uchaguzi unaanza licha ya Mhe. Rais kusema kwamba watu wasijitokeze kugombea kwa sababu wakati bado, lakini sasa hivi ukienda majimboni tayari watu wameshakaa vizuri na makundi yao. Sasa mimi ninachokisema ni kwamba ili siri hizi zisitoke kwa sababu tunapofanya siri zetu hasa wakati wa uchaguzi siri hizi zinatoka sijui nani anayezitoa. Kwa maana hiyo, mimi nasema kuwepo kitengo hiki ni vizuri zaidi kwa sababu huenda mambo haya yakapungua.

Baada ya hapo Mhe. Spika, mimi kwa sababu hii hotuba huwezi ukazungumza sana na kwa sababu hotuba hii ukizungumza sana sijui mwisho wake utasema nini, la kusema huna, isipokuwa ni kwamba hotuba hii imemaliza na kupangika kwa kila kitu. Nimshukuru sana Mhe. Waziri na watendaji wake kwa jinsi hotuba yao walivyoipangilia na kutuletea sisi hapa.

Kwa maana hiyo basi, nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa kupata fursa hii na nimshukuru kabisa waziri pamoja na watendaji wake na niseme kwamba kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chonga tunaiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais kwa asilimia elfu mbili na ushei. Ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante. Naomba sasa nimwite Mhe. Suleiman Sarahan Said na kama muda utaruhusu Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Juma Ali Khatib) atazungumza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nashukuru na mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kitabu chake ambacho kimesheheni mambo ambayo ni sifa nzuri za Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kazi halisi ambazo anazifanya.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda na mimi niendelee kutoa busara zangu katika kitabu hiki ni kwamba kwanza nimsifu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein katika hekima na busara zake za kuiendeleza Zanzibar na wananchi wake bila ya kutumia kiburi chake au uwezo wake ambao yeye kama binaadam huwa anao, lakini Mwenyezi Mungu amempa subira na mpaka Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mhe. John Joseph Magufuli na yeye akasema kwamba lau kama ningepata hekima kama ya Dkt. Ali Mohamed Shein angalau nusu yake basi angeweza labda ikawa vizuri zaidi, lakini ndio hekima kama hizi zinapewa watu ambao Mwenyezi Mungu amewatunukia.

Mhe. Spika, pia nimsifu tena Mhe. Rais sijaona baadhi ya nchi nyingi ambazo zinaweza kuwa kuna matatizo ya wananchi kupita kama barabara na matatizo mengine akatoa ruhusa ya kufidia kwa watu wale, ili wananchi wale wasiondoke pale katika hali ya manung'uniko na ndio watu wengine huwa wanafanya mchezo, lakini Mheshimiwa wala hajali isipokuwa anaendeleza juhudi zile zile za kuweka wananchi katika hali ambayo kwa kweli Zanzibar tunajivunia.

Mhe. Spika, mimi niende kwenye maendeleo ya Pemba, mtu yeyote ambaye amekwenda mwaka 2010 Pemba akipelekwa leo haamini kabisa ilivyo, pamoja na wananchi wake na hali ya kisiasa lakini Pemba imebadilika na ni hekima na maendeleo ya Mhe. Ali Mohamed Shein.

Mhe. Spika, niendelee katika zao la karafuu. Mheshimiwa zao la karafuu lilifikia pahali pabaya sana Pemba na ilifikia mikarafuu mpaka ikawa haina maana, bora mabungo yalikuwa na maana kuliko mikarafuu au watu waliikata mikarafuu wakaona bora kuuza bungo. Matokeo yale leo karafuu imekuwa mali, lakini pia Mhe. Rais ameshajihisha kuipanda mikarafuu. Lakini sasa hivi watu wamehamasika mpaka mikarafuu au ile miche ya mikarafuu imekuwa hakuna Pemba au ni michache watu wananung'unika kwamba bado hali ya miche ya karafuu haikupatikana.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Rais akaendeleza kasi ya mikarafuu watu wameshajihika kweli kweli kuhusu miche ya mikarafuu, watu wamekuja katika mpango wa karafuu lakini karafuu ilikuwa ni michache sana. Kwa hivyo, nguvu ambayo Mhe. Rais aliitumia imezaa matunda kwenye mikarafuu hili nimsifu sana. Lakini pia nitoe juhudi za watu wa kilimo waendeleze kutoa miche ya mikarafuu kwa zaidi kwa sababu mikarafuu sasa hivi inahitajika sana Pemba.

Mhe. Spika, pia nimsifu Mhe. Rais katika suala lake la kuleta maendeleo Pemba. Ukiangalia Mhe. Spika, hivi karibuni amefungua umeme katika kisiwa cha Fundo. Hakujali kule Fundo kuna nini, kule Fundo kuna faida gani, wala kule Fundo kutatia tija gani ya umeme, yeye aliwapelekea wananchi umeme bure. Wananchi wale siku ya ufunguzi wa umeme yeye mwenyewe kwanza aliteremka maji ya kwenye kifua kwenda kufungua umeme. Lkini hakujali akaona aende kwenye wananchi wake. Wananchi walioitikia wito kule ulikuwa wa aina yake watu walifurahi kupita kiasi hawakujali chochote walimfuata Rais wetu kutokana na jitihada zake. Lakini Mhe. Spika, kule kule

alisema maneno kwamba na Uvinje nayo anataka ahakikishe umeme utapatikana wakati huo wakijitayarisha Kokota, lakini wakati huo huo na Njau wakijitayarisha.

Kwa hivyo, mimi nimsifu sana Mhe. Rais katika kuleta maendeleo kisiwa kama cha Fundo umeme ulikuwa ni kazi kubwa sana maana yake ni kazi ya umeme unapita chini ya bahari na ambayo kazi hiyo hiyo imefanywa na *ZECO*. Mhe. Spika, kwa kweli ni wenyewe wazalendo ndio wamefanya hii shughuli namshukuru sana Mhe. Rais.

Lakini katika kitabu niliona sana wageni waliomtembelea Mhe. Rais, wageni wengi sana wa kimataifa, wa kitaifa na waliomo ndani ya nchi wamemtembelea sana. Lakini na yeye alipata mualiko mwingi wa kutembea nchi za nje. Mhe. Spika, hii kuna kauli "Mgeni njoo mwenyeji apone" hapa matumaini yapo na ni ukarimu wake ndio uliomfikisha wageni wengi wakafika. Kwa hivyo, lazima hili nalo nilitie katika suala zuri ambalo Mhe. Rais alilifanya.

Mhe. Spika, nataka niende katika mwaka au msimu ambao majengo ya Afisi za Serikali. Mhe. Spika, sasa hivi serikali imejipanga kweli kweli katika kujenga afisi zake za kisasa ambazo zina uwezo wa kila kitu katika masuala, tumehangaika muda mwingi tukikodi maeneo na afisi zake zikiwa mbovu kabisa. Mhe. Rais kwa makusudi ameamu na afisi zinaonekana na nyengine zinajengwa. Mhe. Spika, hilo lazima nisifu.

Mhe. Spika, nisifu kitu chengine chochote huwezi kufanya bila ya takwimu. Mhe. Rais neno la takwimu ameliweka mbele sana ili akijua nini atafanya na ajue nini napanga. Kwa hiyo, amejenga jengo zuri sana hapo la Takwimu ili kujua kila kitu cha serikali kinaendaje katika takwimu na hata wafanyabiasha na vitu vyote ajue mipangilio ya kwenda haendi kiholela holela yule ni msomi anajua anaendesha nchi. Kwa hivyo, si maneno tu ya blaa blaa yeye anakwenda kwa takwimu na hivi ndio vitu vinavyompeleka mbele katika kujua nini athari zake.

Mhe. Spika, pia nimsifu upandishaji wa mishahara, nchi gani imepandisha mishahara asilimia mia, hakuna. Hili ni jambo kubwa sana ambalo kwa kweli watu walikuwa wanalitegemea na wengine hawalitegemei lakini amelifanya na limefika. Lakini pia bado anaendeleza kutoa ile ruzuku ya wazee ambayo mpaka sasa hivi haijatikisika, lile ni jambo ambalo la kumshukuru sana Mhe. Rais. Kwa hivyo, lazima tuangalie hilo. (*Makofi*)

Lakini mimi nizungumzie kwamba kwa asiyefahamu na watu waliokuwa hawapendi maendeleo Zanzibar hapa Unguja Mjini Magharibi imegeuka na bado *target* ya Mhe. Rais watu wengi walikuwa hawajafahamu kwenye Mnara pale wengi walipiga vita nini kitatokea na watu wengi maeneo yaliyovunjwa vunjwa wanaona hakuna lililofanyika. Lakini Mhe. Spika, kama picha za upeo wa pahala pale nini ambacho kitafanyika pamoja na "Ng'ambu Tuitakayo", mtu angefunga mdomo akasema kama ingekuwa sio Katiba yetu, Mhe. Rais alikuwa aendelee tena miaka kumi ili atuoneshe nini ambacho pale amekusudia. Lakini ni kanuni na sheria zetu tulizopanga sijui mbele itakuwa nini. Lakini nikwambie kwamba lau kama tungefahamu nini malengo yake bado tuna shida ya Rais wetu Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kuendelea na uongozi wake. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda na mimi niendelee kusema suala la Mahkama. Mhe. Rais Mahkama amepanua wigo sana watu wengi waliokuwa hawana uwezo walikuwa haki zao zinapotea ovyo. Lakini upeo wa Mahkama ya Mhe. Spika, ametoa upeo mkubwa maskini na tajiri waende kule kwenye kimbilio la haki ambalo kwa kweli limefikia katika hatua kubwa sana. Kwa hiyo, Mhe. Spika, nimsifu sana wanyonge wamepata pahala pa kukimbilia na haki zinapatikana.

Mhe. Spika, pia nisifu suala la ardhi, umeme, maji, elimu, afya na barabara Zanzibar tumepiga hatua kubwa sana, asilimia kubwa sana. Elimu yetu huwezi kwenda kilomita moja hujafika kituo cha elimu, hujafika kituo cha afya na barabara labda porini. Lakini barabara karibu asilimia 80 barabara zetu nzuri. Hili jambo la kujisifia sana lazima tuangalie maji yanapatikana sana ibakishe tu matatizo madogo madogo yako katika masuala hayo.

Lakini katika masuala ya takwimu lazima nimsifu Mhe. Rais mimi nimekaa miaka yote pale kunaitwa Chake Chake haijulikani kijiji wala mji. Mhe. Rais amepandisha Chake Chake imekuwa mji wa pili kati ya Miji Mikuu ya Zanzibar ukiachia Mjini Magharibi hapo, mji wa pili unakuwa Chake Chake. Lakini kuna miji midogo kumi na nne amefanya takwimu kwa kuipandisha miji ili iwe miji. Kwa hivyo, hili sio suala dogo mji ukipanda una vitu vyake una mambo yake lazima utakuja juu katika masuala yale.

Mhe. Spika, mimi nimsifu Mhe. Rais katika kipindi hichi amejitahidi sana bajeti yake kuitegemea mwenyewe, bajeti tegemezi mwenyewe kwa asilimia ndogo sana ndio tunategemea wahisani. Lakini ameweza ku-*balance* yeye mwenyewe kusimama kwa miguu yake kama Zanzibar na ikaweza kulipa mishahara, ikaweza kufanya vitu vyake wahisani wakatusaidia lakini tunaweza kusimama wenyewe. Kwa hivyo, ni jambo kubwa sana ambalo Mhe. Rais hili amelifanya tunahitaji tumsifu sana.

Lakini Mhe. Spika, tuangalie watu wanaoishi nchi za nje hawa Diaspora. Mhe. Rais hajapata kiburi cha kuwa wale labda wako wapi kila siku anawaita katika mikutano katika maeneo mengi ili kuhakikisha watu hawa nao ni Wazanzibari wanaoweza kutoa michango wanaoweza kurudi kwao. Lakini mimi nikasema tu Mhe. Waziri amesema kwamba "Mtu kwao ndio ngao" hili ni neno amelitumia katika kitabu chake kwa kuwaeleza wale kwamba hata kama wanaishi nje bado wanahitajika Zanzibar, hili ni suala ambalo Wazanzibari tuko hivyo.

Nimsifu sana Mhe. Rais wetu kwa kweli ni mtu mmoja peke yake ambaye katika muono wake amependa sana kuudumisha Muungano na kuimairisha Muungano, lakini pia kuyaenzi mapenzi ya Mapinduzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hili Mhe. Rais lazima katika hotuba yake analitaja kwamba lazima ni kuimarika Muungano zaidi, lakini pia ni kuyatunza na kuyaenzi Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, hili nilikuwa niliseme nisije nikalisahau.

Mhe. Spika, mimi niseme suala la michezo, Mhe. Rais ni mwana michezo. Kwa kweli michezo kwa upande wa Zanzibar kwa kipindi hichi kifupi Zanzibar imekuwa sana

kimichezo na hatimae ndio tumeona kwamba juzi tulibahatika kuwa tayari tungekuwa washindi wa kombe hili la *CECAFA*. Kwa hivyo, zawadi alizotoa si ndogo, alitoa zawadi za mshtukizo, lakini kama wananchi na wanamichezo wataonesha upeo zaidi Mhe. Rais hawezi kuwa na kigezo asiwape zawadi, sisi tujitahidi ili kuendeleza zaidi kumuonesha moyo na nini tunaweza kuifanya kwa kuitangaza Zanzibar.

Mhe. Spika, nizungumze suala moja la *ZBC*. Lengo kubwa la *ZBC* ni kuona wananchi wote wanaipata *ZBC* kutokana na kwamba chombo hichi ni cha uhakika kinachoweza kutoa taaluma na kutoa kitu chochote cha usahihi katika serikali. *ZBC* tukiangalia huko tukisema *TVZ* ya Zanzibar ni *TV* ya kwanza Afrika iliyokuwa ya rangi ambayo kwa miaka hiyo ya 1970 ndio iliyokuwepo. Mhe. Spika, hii *TV* bado maeneo mengi haionekani na bado wanataka kuona maendeleo ya Zanzibar kuliko kuona propaganda zaidi. Ningeomba sana hii *TV* ikaongezwa nguvu nyingi sana Mheshimiwa ...

Mhe. Spika: Bado dakika tatu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika. Ikaongezwa nguvu sana ili kuweza kupatikana kwa urahisi. Ingawa Mhe. Waziri anasema sasa hivi ni wakati wa *digital* na malipo. Mimi ningeona bado kuna haja ya kwamba *ZBC* iwe bure, hakuna malipo ya king'amuzi wala nini, wafanye mtambo maalum utakaoweza kurusha ikifunguliwa *TV* wewe muache afunge *TV* zote *TVZ* ipatikane au *ZBC*. Hili ni jambo muhimu sana Mhe. Spika, kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi*)

Lakini Mhe. Spika, pia nimsifu Mhe. Rais kwa kutoa uhuru wa Vyombo vya Habari isipokuwa tu vyombo vyenyewe vieleze ukweli ambavyo vitakuwa visiweze kutuletea matatizo na maafa katika nchi yetu. Mhe. Spika, ziadi ya yote nakipongeza sana kitabu hichi, lakini nampongeza pia Makamu wa Pili wa Rais katika juhudi zake, nawapongeza Mawaziri wote na Manaibu Mawaziri na Baraza la Wawakilishi katika uchangiaji. Naunga mkono hoja asilimia mia moja. Nakushukuru sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Juma Ali Khatib): Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba hii nzuri iliyotolewa na ndugu yetu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu). Kitabu hichi kimekamilika vizuri na hotuba yake ni nzuri.

Nawapongeza sana Wawakilishi wenzangu waliokuja hapa kuchangia wote walikisifu hichi kitabu. Jana tumeanza Hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais na leo tuko kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, kwanza mimi napenda kumpongeza Mhe. Rais kutokana na ahadi nyingi ambazo kazitekeleza na kazi nyingi ambazo kazifanya kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi na ndio inayofanya kazi katika serikali yetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tumeshuhudia hapa viongozi wengi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakitoa sifa kwa Mhe. Rais na mimi nawaunga mkono kweli Mhe. Rais anastahili kupata

sifa. Lakini nataka kusema na nataka kuomba kitu kimoja, Mhe. Rais kuna wasaidizi wake wa karibu ndio wanaomfanya aweze kung'ara vile anavyong'ara. Mimi nataka kuwashukuru na kuwapongeza kwanza hawa wafuatao:-

1.	Katibu Mkuu Kiongozi	-	Mhe. Abdulhamid Yahya Mzee
2.	Naibu Katibu Mkuu Kiongozi	-	Mhe. Salmin Amour Abdalla
3.	Katibu Ofisi ya Rais	-	Ndg. Salum Maulid Kibanz

Washauri wa Rais. Kwa sababu hawa Washauri wa Rais Mhe. Spika, ndio wanaomfanya Rais wetu akawa na fikra na hekima nzuri. Kwa hiyo, nawapongeza Washauri wa Rais kwa sababu wanamshauri vizuri Mhe. Rais katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kuwaletea Maendeleo Wazanzibari. (*Makofi*)

Mhe. Spika, pia nampongeza ndugu yetu Afisa Mdhamini aliyepo Pemba Maalim Amour kwa kweli anafanya kazi vizuri na ni hodari sana. Mimi nataka kuwapongeza Wawakilishi wote wa Unguja na Pemba wanafanyakazi vizuri kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu sisi tumekuwa tukipita kwenye majimbo yao kuangalia miradi ya serikali na ahadi za Rais, tumegundua kwamba mambo mengi yaliyofanywa na serikali pia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuna michango yao mikubwa kama Wawakilishi wamefanya kwenye majimbo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuna ushahidi mmoja nataka nikupe wa wazi hautaki tochi kule kijiji cha Ngomeni kuna watu hawafiki hata mia nne. Lakini awamu nyingi za serikali zimepita kwa bahati mbaya kulikuwa hakuna maendeleo, lakini awamu hii ya Dkt. Ali Mohamed Shein sasa hivi kule Ngomeni kuna maji ya kutosha. Nampongeza Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati sasa hivi kule Ngomeni kuna umeme, kuna skuli, kuna barabara mpya ya kisasa. Mhe. Spika, barabara imejengwa mwaka huu sio zamani barabara mpya kabisa, kuna Shirika la *ZSTC* wamejenga pale banda zuri la kisasa pale Ngomeni. Ukizingatia Mhe. Spika, kule ndio kunatoka karafuu nyingi sana, uchumi wetu wa Zanzibar unatoka pale. Pia Mhe. Spika, pale Ngomeni kuna Kituo cha Afya kinakaribia kumalizika sasa hivi. (*Makofi*)

Kwa hivyo, haya ukiangalia ndio zile ahadi ambazo zimetekelezwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vile vile Mhe. Spika, tumegundua kwamba katika utekelezaji wa kazi za Rais Kojani sasa hivi kuna umeme, kuna maji, Fundo kuna umeme kuna maji, kuna hospitali na tulikwenda pale Kituo cha Afya tukazungumza na madaktari wakasema kuna dawa za kutosha. Makoongwe Mhe. Spika, kuna umeme, kuna maji ni kisiwa hichi, Kisiwa Panza tumekwenda juzi tu kuna maji safi na salama yamevushwa pale na kuna umeme, kuna skuli na kuna Vituo vya Afya na kuna dawa za kutosha.

Mhe. Spika, kwa kweli tukisema kwamba tuchangie kitabu hichi kuna mambo mengi sana. Hivi ni visiwa vidogo vidogo na vijiji ambavyo kwa miaka mingi sana vilikuwa havijapata maendeleo, lakini kwa awamu hii sasa maendeleo yamekuja kwa kasi na kwa haraka. Ndio maana nikasema Rais anapong'ara, pale anapopendeza, pale anapofanya wajibu wake tusiwasahau na wale wasaidizi wake. Lakini juu ya yote lazima na sisi tujipongeze kama watendaji wa serikali, serikali hii imefanyakazi zake kwa kasi na kwa

uadilifu mkubwa sana. Leo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusanya mapato mengi sana ya serikali kuliko awamu zote zilizopita. (*Makofi*)

Tumeshuhudia serikali hii hii inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein sasa hivi wale wafanyakazi hewa kwa kiasi kikubwa sana hawapo, uvujaji wa pesa za serikali umepungua kwa kiasi kikubwa ingawa haujaisha. Lakini serikali pamoja na vyombo vyake inalifanyia kazi suala hili, hili ni jambo la kujipongeza sote watendaji wa serikali.

Mhe. Spika, wenzangu wengi sana hapa walizungumzia kuhusu ziara ya Mhe. Rais Falme za Kiarabu. Mimi nilibahatika kuwa mmoja niliyeteuliwa na Mhe. Rais kwenda kule. Nataka kuwaambia Wawakilishi wenzangu Dkt. Ali Mohamed Shein katika ziara ile alipata mapokezi ya kihistoria. (*Makofi*)

Mhe. Spika, haijapata kutokea kiongozi mgeni au Rais kutoka nchi yoyote ile ya Afrika akaenda kwenye ziara ya Falme za Kiarabu katika ziara ile akakutana na wafalme wanne pamoja, haijapata kutokea. Lakini kwa heshima kubwa sana na mapenzi makubwa aliyooneshwa Rais wetu pamoja na watu wetu wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohamed Shein alipata mapokezi makubwa kwa wafalme wote, kiasi ya kwamba walikuwa wanatamani ule muda uongezwe ili ile ziara iendelee. (*Makofi*)

Kwa hivyo, ziara hii ilikuwa na mafanikio makubwa, kwanza imeleta faida ya kuimarisha mahusiano yetu ya Falme za Kiarabu na Tanzania. Pia imeleta maslahi makubwa kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wananchi wake katika kuwaletea maendeleo Sekta ya Elimu, Sekta ya Afya, Sekta ya Barabara na Sekta ya Uchumi na mambo mengi tu ya misaada.

Kwa hivyo, mimi nataka kumpongeza Mhe. Rais amekuwa akifanya kazi kubwa sana akiitekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na akipeleka maendeleo Unguja na Pemba bila ya ubaguzi. Mhe. Spika, tulishuhudia hapa kuna kipindi tulikwenda na Mhe. Rais kwenye ziara yake kule Mbuyumaji na Mlile kulikuwa hakuna maji sasa maji yapo. Nampongeza Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati kulikuwa hakuna umeme, kulikuwa hakuna skuli, kulikuwa hakuna njia, sasa shughuli zote hizo zimefanywa. Mhe. Spika, haya ni mafanikio makubwa yaliyofanywa na Mhe. Rais pamoja na wasaidizi wake.

Mhe. Spika, pia nataka kusema kitu kimoja kwamba napenda kuipongeza Kurugenzi ya Ikulu kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya. Kazi za Rais zinazofanywa na mikutano inayofanywa wananchi wanapata ripoti kwa wakati kutokana na kwamba Kurugenzi ya Ikulu imejipanga vizuri na inafanyakazi vizuri. Nampongeza mpiga picha wa Rais Ndg. Othman yule anayepiga picha na kupeleka magazeti. Pia nampongeza ndugu yangu Omar Ahmed Mcheju yeye ni mpiga picha wa Rais, wananchi wengi wa Zanzibar wa Unguja na Pemba wanapata picha kutokana na hawa watendaji niliowataja hapa. (*Makofi*)

Kwa sababu unaweza kuwa wewe mpiga picha lakini usiwe mbunifu, lakini ndugu yetu huyu Omar Ahmed Mcheju ni mbunifu kiasi ya kwamba hata siku ya *birthday* ya Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein mimi niliona kupitia mtandao wa Mcheju ndio nikajua Mhe. Rais kumbe leo ni *birthday* yake. Kwa hivyo mimi nampongeza sana.

Vile vile Mhe. Spika, nataka kumpongeza Mkurugenzi wa Gazeti la Zanzibar Leo ambalo sasa hivi limeboreka sana, wananchi wetu hasa wale wa vijijini wanapata kuona habari na picha za matukio mbali mbali ya viongozi wa serikali ambayo yanafanyika.

Kwa kweli kiujumla vile vile nataka kuwasifu viongozi wote ambao wanamsaidia Mhe. Rais. Serikali yetu imefanya mambo mazuri imefanya mambo makubwa na kilichopo sasa ni yale anayosema Mhe. Rais tusifanye kazi kwa mazowea, tubadilike.

Kwa hivyo, kama sisi tunasema hapa tunakipongeza hichi kitabu sasa wale wasaidizi na wale wafanyakazi na wale watu wote wenye dhamana mbali mbali kwa serikali tuendeleze hii bidii. Serikali yetu iko pazuri imefanya mambo makubwa. Mhe. Spika, tunastahili kujipongeza tusingoje kupongezwa, wapo watu hawaitakii mema serikali yetu, lakini bahati nzuri uongozi mahiri wa Dkt. Ali Mohamed Shein serikali imefanya vizuri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, suala la amani na utulivu kama alivyokuja kusema ndugu yangu hapa Mhe. Machano Othman Said na Mhe. Hamza Hassan Juma walizungumza vizuri sana. Nchi yetu iko katika hali ya amani na utulivu, tunajua hali ya siasa ya nchi yetu, lakini chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein kaweza kuiweka nchi hii katika hali iliyotulia na mpaka leo sasa hivi watu wa Unguja na Pemba ni wamoja hakuna matatizo Pemba, hakuna matatizo Unguja. Mhe. Spika, sisi hivi karibuni tu tumepita sehemu mbali mbali Pemba vijijini na mijini kila mmoja anapenda maendeleo yaliopo sasa.

Mhe. Spika, nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri waliyofanya. Mhe. Spika, namalizia kwa kuwaomba Wawakilishi wenzangu wote kama wasemaji waliopita kwamba kitabu hichi cha Bajeti hii sote kwa pamoja tuipitishe bila ya kupiga buti kila kitu hapa kimejitosheleza. (*Makofi*)

Kwa hivyo, kwa heshima na kwa unyenyekevu Wawakilishi wote hutoba hii na tutakapofika pale Baraza kukaa kama Kamati tusipige buti tuipitishe kama tulivyopitisha jana Hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais basi na hii ioneshe mfano. Kwa sababu mambo yote yaliyoandikwa humu yamejitosheleza na kuna mambo mengine mazuri hayakuweza kuingia humu. Tungesema mambo yote yaandikwe humu vitabu vingekuwa vingi sana. Kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja na naunga mkono hotuba hii. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Juma Ali Khatib. Waheshimiwa Wajumbe huyo ndio aliyekuwa mchangiaji wetu wa mwisho. Naomba niwataje wachangiaji watatu watakaoanza asubuhi siku ya Jumatatu, tutaanza na Mhe. Mohamed Said Mohamed, atafuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa na baadae atafuatia na Mhe. Said Soud Said. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe kama mtakuwa mmefuatilia kwenye bajeti hii wamechangia wanaume tu, nilikuwa bado nasubiri kupata michango kutoka kwa waheshimiwa ukiacha Mhe. Panya Ali Abdalla ambaye alisoma hapa kwa niaba ya kamati.

Waheshimiwa baada ya hapo naomba pia nikukumbusheni kwamba ile shughuli yetu ya damu ipo kesho. Kwa hiyo, nahimiza sana ili tuje tushiriki tuweze kutoa damu kwa ajili ya kujiandaa na Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Baada ya matangazo machache hayo, naomba sasa niakhirishe shughuli za Baraza mpaka siku ya Jumatatu saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:52 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 14/05/2018 saa 3:00 asubuhi)